International Labour Organization

Elimu ya kifedha

Kwa wahamiaji watarajiwa na waliorejea nchini Kenya

SIMAMIA MAPATO YAKO KWA BUSARA

UKaid from the British people

Hakimiliki © Shirika la Wafanyakazi Ulimwenguni (ILO) 2021
Ilichapishwa kwanza mnamo 2021

Machapisho ya Ofisi ya Wafanyakazi Ulimwenguni yamelindwa na hakimiliki kwa mujibu wa Utaratibu 2 wa Mkataba wa Hakimiliki wa Kimataifa. Ingawa hivyo, dondoo fupi kutokana na machapisho hayo zinaweza kuchapishwa upya bila kibali, kwa kuhakikisha kwamba chanzo kinabainishwa. Kwa haki za kuchapisha upya au kutafsiri, maombi yanapaswa kutumwa kwa Machapisho ya Shirika la Wafanyakazi Ulimwenguni (ILO) (Haki na Utoaji Leseni), Ofisi ya Wafanyakazi Ulimwenguni, CH-1211 Geneva 22, Uswizi, au kwa njia ya barua pepe: rights@ilo.org. Ofisi ya Wafanyakazi Ulimwenguni inakaribisha maombi kama hayo.

Maktaba, taasisi na watumizi wengine waliosajiliwa kwa shirika lenye haki za kurudufu wanaweza kutoa nakala kwa mujibu wa leseni walizopewa kwa ajili hii. Tembelea www.ifrro.org ili kupata shirika lenye haki za kurudufu katika nchi yako.

Lugha: KIINGEREZA
ISBN: 9789220409114 (chapisho)
ISBN: 9789220409121 (PDF mtandaoni)

Lugha: KISWAHILI
ISBN: 9789220409138 (chapisho)
ISBN: 9789220409145 (PDF mtandaoni)

Uteuzi uliotumika katika machapisho ya ILO, ambayo yanawiana na desturi ya Umoja wa Mataifa, na uwasilishaji wa nyenzo zilizomo haimaanishi utoaji wa maoni yoyote kwa upande wa Ofisi ya Wafanyakazi Kimataifa kuhusu hadhi ya kisheria ya nchi, eneo au jimbo lolote. au ya mamlaka yake, au kuhusu uwekaji wa mipaka yake.

Wajibu kuhusu maoni yanayowasilishwa katika makala yaliyotiwa sahihi, tafiti na michango mingine ni wa waandishi wenyewe, na uchapishaji haumaanishi uidhinishaji wa Ofisi ya Wafanyakazi Ulimwenguni kuhusu maoni yaliyotolewa humo ndani.

Marejeleo ya majina ya kampuni na bidhaa na michakato ya kibiashara haimaanishi uidhinishaji wake na Ofisi ya Wafanyakazi Ulimwenguni, na kukosa kutaja kampuni fulani, bidhaa au mchakato wa kibiashara sio ishara ya kutoidhinishwa.

Taarifa kwenye machapisho ya ILO na bidhaa za kidijitali inaweza kupatikana kupitia: www.ilo.org/publns

SHUKURANI

Maandalizi ya kijitabu hiki cha Mkurufunzi cha Elimu ya Kifedha kwa Waliorejea na Wahamiaji watarajiwa nchini Kenya yaliongozwa na Gustavo Prepelitchi, kwa msaada na usimamizi wa jumla wa Ines Bentchikou na Yousra Hamed, kutoka Mpango wa Fedha wa Kijamii wa ILO. Juhudi hizi zimesaidiwa pakubwa kutokana na maoni muhimu ya kitaaluma na michango ya wenzetu kutoka kwa Mradi wa ILO wa Usimamizi Bora wa Uhamiaji wa Kikanda unaoendeshwa nchini Kenya na Uhabeshi, na hasa kutoka kwa Wycliffe Ouma, Kidest Getahun na Aida Awel. Maandalizi ya kijitabu hiki cha mkurufunzi pia yalichangiwa na Pauline Kieme, ambaye alitoa taarifa zaidi kuhusu muktadha wa ndani wa kijamii na kiuchumi na sekta ya kifedha nchini Kenya.

Kijitabu hiki cha mkurufunzi kimejikita kwa msururu wa nyenzo za mafunzo zilizoandaliwa na Mpango wa ILO wa Elimu ya Kifedha katika Afrika Mashariki. Kwa hivyo, maandalizi yamenufaika kutokana na msaada na michango muhimu kutoka kwa Matawi ya ILO huko Uhabeshi, Kenya na Uganda, watoaji wa huduma za kifedha, vituo vya mafunzo ya kiufundi, watoaji wa huduma za msaada wa ukuzaji wa biashara, pamoja na mashirika yasiyokuwa ya kibiashara. Mchango wa waliorejea wateule pia ulikuwa unathamini sana wakati waliposhiriki katika majadiliano ya vikundi lengwa yaliyoendeshwa mapema katika mchakato wa kutengeneza nyenzo, na ambayo yalitumika kama msingi mzuri wa urekebishaji wa kijitabu hiki cha mkurufunzi Cha mpango wa ILO wa Elimu ya Fedha.

Michoro imeandaliwa na Samba Cissé na usanifu umefanywa na Solomon Naviswa.

YALIYOMO

Utangulizi 8

1. Usuli 8
2. Uwasilishaji wa kijitabu cha mkurufunzi 9
3. Utangulizi kwa wahusika 9

Kitambulisho cha Gloria 10
Kitambulisho cha Otieno 11
Kitambulisho cha Mutua 12
Kitambulisho cha Wangari 13

A) Weka malengo na uwasiliane katika familia yako 14

1. Weka malengo yako 15
2. Tathmini gharama za malengo yako na vipaumbele vyako. 17
3. Fanya mpango wa kuweka akiba ili kutimiza malengo yako. 18
4. Zungumza na familia yako kuhusu malengo yako 21
5. Amua iwapo kuhama ndilo chaguo bora kwako 24
6. Hesabu gharama za kifedha za uhamiaji 25

B) Simamia mapato yako kwa busara 28

1. Kuwa mtumia pesa mahiri! 29
2. Unda bajeti yako! 34
3. Fuatilia na uhakikishe unabaki ndani ya bajeti yako. 43
4. Hifadhi rekodi zako za kifedha 51

Viambatisho na nyaraka muhimu 52

C) Fahamu mbinu na mipango ya kuweka akiba 54

1. Chagua mbinu ya kuweka akiba 55
2. Chagua mpango wako wa kuweka akiba kwa busara 58

Viambatisho na nyaraka muhimu 66
Majibu kwa mazoezi 67

D) Tumia mipango ya mikopo kwa busara 71

1. Tafuta mbinu ya kufadhili mipango yako 72
2. Chagua muamana wako kwa busara! 75
3. Hesabu gharama ya mkopo wako 80
4. Kuwa mwangalifu! Usichukue mikopo mingi kupita kiasi! 88

Viambatisho na nyaraka muhimu 92
Majibu kwa mazoezi 93

E) Chagua mbinu za malipo na mfumo wa kutuma pesa 98
1. Tumia mbinu ya malipo yenye usalama 99
104
110
2. Pata kuwajua waendeshaji wa huduma za utumaji pesa 109
114
3. Jinsi ya kutuma na kupokea pesa 115
Viambatisho na nyaraka muhimu
Majibu kwa mazoezi 119

F) Zifahamu taasisi za kifedha na uzitumie kwa kujiamini
1. Zifahamu taasisi za kifedha 120
2. Tumia taasisi za kifedha kwa kujiamini! 126
Majibu kwa mazoezi 139

G) Usimamizi wa Hatari na Bima 144
1. Simamia hatari 145
2. Vidokezo vya kuunda hazina yako ya dharura 149
3. Elewa mkataba wa bima yako 150
4. Tumia mkataba wa bima yako 154
158
5. Chagua bidhaa ya bima inayokufaa 160
Viambatisho na nyaraka muhimu 161
Majibu kwa mazoezi

Ujelezi 162

UTANGULIZI

1. USULI

Nyaraka uliyo nayo mikononi mwako ni kijitabu cha Mkurufunzi kuhusu elimu ya kifedha. Kimsingi inalenga wahamiaji watarajiwa na waliorejea nchini Kenya ambao wangependa kuboresha usimamizi wao wa pesa.

Kijitabu hiki cha wakurufunzi kinatanguliza ujuzi, stadi na vifaa vya kimsingi vinavyohusiana na upataji mapato, matumizi, uandalizi wa bajeti, na kutumia huduma za kifedha kama vile kuweka akiba, mkopo, utumaji wa pesa na bima.

Azma ya nyenzo za mafunzo ya Elimu ya Kifedha ni kufunza wahamiaji watarajiwa na waliorejelea masuala ya kimsingi kuhusu fedha za kibinafsi na za familia. Nyenzo zinashughulikia mada zifuatazo: kuweka malengo ya kifedha, kuwasiliana kwa kujiamini, kuhesabu gharama za kifedha za uhamiaji, kuelewa mipango muhimu ya kifedha (uwekaji hazina, mikopo, malipo, pochi la kidijitali, bima), kuelewa malipo ya kidijitali, kuelewa na kujadili na taasisi za kifedha, kutuma pesa na kusimamia hatari. Mafunzo yamelengwa kuponya kiwango cha chini cha elimu na mahusiano ya uwezo yasiyokuwa na usawa - baina ya wanaume na wanawake na baina ya vizazi vikongwe na vile vichanga - ambavyo aghalabu huathiri maamuzi yanayohusiana na pesa. Mwongozo huu mahususi unaangazia changamoto na fursa ambazo zinawakumba waliorejea na wahamiaji watarajiwa nchini Kenya.

Kifurushi cha mafunzo kimeandaliwa na Shirika la Wafanyakazi Ulimwenguni (ILO) kwa kuzingatia nyenzo mbalimbali za ILO za elimu ya kifedha zilizoundwa kwa ajili ya vikundi mbalimbali mahususi. Kijitabu hiki maalum kimefanyiwa marekebisho kwa ajili ya matumizi nchini Kenya.

Kijitabu hiki cha Mkurufunzi kinapaswa kutumiwa kwa pamoja na mwongozo wa mkufunzi. Kimeandaliwa kwa ajili ya vikundi maalum teule. Kama nyongeza kwa mwongozo wa mkufunzi, kijitabu cha mkurufunzi kinatoa taarifa zote zinazohusiana na wahusika wa kubuni, matukio kifani, mazoezi na marejeleo maalum kwa kundi lengwa. Kijitabu hiki pia kinajumuisha hoja muhimu za mafunzo na nyenzo zinazohitajika kwa kutumia na kusimamia pesa za kibinafsi kwa busara. Kimeandikiwa wanaume na wanawake wanaoshiriki katika masomo ya mafunzo haya. Kinapaswa kutumiwa kama kitabu cha mazoezi wakati wa somo na baadaye kama mwongozo wa marejeleo.

2. UWASILISHAJI WA KIJITABU CHA MKURUFUNZI

Elimu ya kifedha, inahusu nini?



Elimu ya kifedha ni ujuzi, stadi na nyenzo ambazo zinakusaidia kusimamia pesa zako vyema zaidi. Mafunzo ambayo utahudhuria yatakusaidia kupanga na kujiandaa kwa miradi yako katika siku zijazo. Elimu hii inatoa fursa ya kujifunza stadi zinazohusiana na upataji mapato, matumizi, uandalizi wa bajeti, kuweka akiba, kukopa na njia za kutumia rasilimali zako kwa manufaa zaidi.

Vilevile, utapata fursa ya kufikiri kuhusu kuwasiliana vyema zaidi kuhusu masuala ya pesa na familia yako, jamaa zako, watu unaofanya kazi nao na baadhi ya kushughulikia changamoto zinapoibuka.

Utajifunza kuhakiki baadhi ya nyenzo za kitamaduni ili kusimamia pesa zako vyema.

Elimu itashughulikia matumizi, faida na hasara ya huduma za kifedha kwa kina zaidi. Huduma za kifedha kama vile mikopo, uwekaji akiba, utumaji pesa au bima hazitakuwa siri kwako.

Jinsi ya Kutumia Kijitabu cha Mkurufunzi?

Unapaswa kutumia Kijitabu hiki cha mkurufunzi wakati wa mafunzo kuhusu elimu ya kifedha. Mpangilio wa sura unafuata masomo na vipindi vya mafunzo. Hata hivyo, uko huru kusoma sura yoyote kadri unavyopenda!

Kijitabu hiki kinajumuisha mazoezi mengi na karatasi za kufanyia mazoezi ambazo unaweza kujaza binafsi.

3. UTANGULIZI KWA WAHUSIKA

Mpangilio wa mafunzo unatumia visa na tajriba za wahusika wanne wakuu.

Huu hapa ni wasifu wao.

MHUSIKA 1
GLORIA

JINA: GLORIA

Kikundi Kinacholengwa: *Aliyerejea*

Mahali Anapoishi *Syokimau, Kaunti ya Machakos, Kenya*

Jinsia: *Mke*

Umri: *29*

Hali ya ndoa: *Gloria na mumewe Gitau walikutana huko Qatar. Waliamua kurejea Kenya wakati kandarasi yake iliisha. Walirejea miaka 4 iliyopita kutoka Qatar na wakafunga ndoa. Wanaishi pamoja na wako na watoto 2.*

Shughuli za Kiuchumi: *Anafanya kazi katika saluni ya nywele na mumewe anafanya kazi katika sekta ya ujenzi. Yeye pia ni mwanachama katika kikundi cha wanawake wanaotengeneza vifaa vya kufuma na shanga.*

Kiwango cha elimu *Kidato cha 4*

Mtazamo kwa pesa: *Anajipanga vizuri*

Sifa za Kifedha:

- *Anatumia huduma za kifedha zinazotolewa mtandaoni*
- *Kila mara anaweka malengo yake kwanza*
- *Ana mpangilio mzuri na anajaribu kuweka akiba kadri inavyowezekana*

Malengo:

- *Angependa kuwa na saluni yake*
- *Wote wangependa kutembelea wazazi wa Gloria ambao wanaishi Nakuru*
- *Angependa kufanya somo la elimu ya kifedha*
- *Angependa kununua shamba na wajenge nyumba yao*

Wahusika wadogo:

- *Gitau, mumewe Gloria*
- *Watoto wao, Kiprono na Odongo*
- *Rafiki yake, Njambi*
- *Mumo na Musau, wazazi wa Gitau*

MHUSIKA WA 2
OTIENO

JINA: Otieno

Kikundi Kinacholengwa: *Aliyerejea*

Mahali Anapoishi *Kiambu, Kaunti ya Kiambu, Kenya*

Jinsia: *Mume*

Umri: *48*

Hali ya ndoa: *Aliishi Saudi Arabia, lakini alikuwa mhamiaji haramu na akafurushwa miaka mitano iliyopita. Kwa sasa, anaishi na mke wake na watoto wao wanne.*

Shughuli za Kiuchumi: *Anaendesha biashara ya duka ndogo la kuoka kwa pamoja na mkewe, Mwende. Duka hili la kuoka limesajiliwa rasmi.*

Familia: *Anamiliki duka la kuoka, kwa pamoja na mkewe. Mwanawe mkubwa, Jabali, anapenda kupika maandazi na kuoka. Angependa kuendeleza biashara ya familia.*

Kiwango cha elimu *Kidato cha 3*

Mtazamo kwa pesa: *Mwekevu lakini ana kipato kidogo.*

Sifa za Kifedha:

- *Anavutiwa na taasisi rasmi za kifedha*
- *Anatumia mbinu za malipo ya kidijitali*

Malengo:

- *Kumnunulia bintiye baiskeli siku ya kusherehekea kuzaliwa kwake*
- *Kumnunulia mtoto wake mchanga zaidi viatu*
- *Kujifunza uokaji wa vitobosha*
- *Kununua friza kwa duka lake la uokaji ili kutoa bidhaa mpya*
- *Kununua nyenzo zinazohitajika kujenga chumba cha ziada katika nyumba yao.*

Wahusika wadogo:

- *Mke wa Otieno, Mwende*
- *Watoto wake wanne, Jabali (17), Kariuki (12), Adhra (10) na Odhiambo (5)*
- *Majirani wao, Njeri na Owuor*
- *Rafiki ya Mwende, Safia*

MUHUSIKA WA 3
MUTUA

JINA: Mutua

Kikundi Kinacholengwa: *Mhamiaji mtarajiwa*

Mahali Anapoishi *Kibera, Nairobi*

Jinsia: *Mume*

Umri: *32*

Hali ya ndoa: *Hajaoa. Anaishi na wazazi wake.*

Shughuli za Kiuchumi: *Alirejea kutoka Lebanoni, lakini anataka kurudi haraka iwezekanavyo, kwa vile sasa anajua jinsi mambo hufanyika ughaibuni. Anataka kuhamia Kuwait mara hii. Nchini Kenya hana kazi maalum. Anamsaidia rafiki yake ambaye ananunua na kuuza viatu. Ughaibuni, angependa kufanya kazi kama mlinzi ama dereva.*

Familia: *Babake anafanya kazi katika dobi na ndiye mchuma riziki mkuu katika familia yao.*

Kiwango cha elimu: *Kidato cha 1*

Mtazamo kwa pesa: *Mwekevu. Mwenye mipango*

Sifa za Kifedha:
- *Anajaribu kuweka akiba kadri awezavyo ili aende ughaibuni*
- *Anatumia pochi la kidijitali*
- *Anajipanga kwa pesa zake, lakini hawezi kukidhi mahitaji yake*

Malengo:
- *Kuhamia Kuwait kihalali ili kupata pesa zaidi*
- *Kulipia shule ya udereva, ili apate leseni ya udereva*

Wahusika wadogo:
- *Wazazi wa Mutua, Kalekye na Kyalo*
- *Rafiki yake, Opiyo*

MHUSIKA WA 4
WANGAR I

JINA: Wangari

Kikundi Kinacholengwa: *Mhamiaji mtarajiwa*

Mahali Anapoishi: *Kikuyu, Kaunti ya Kiambu, Kenya*

Jinsia: *Mke*

Umri: *24*

Hali ya ndoa: *Hajaolewa. Anaishi na wazazi wake shambani mwao.*

Shughuli za Kiuchumi: *Anafanya kazi kwa msimu katika ukulima. Angependa kuhamia Qatar kufanya kazi kama mlezi ili aweke akiba ya pesa.*

Familia:

- *Wazazi wa Wangari pia wanafanya kazi kwa msimu katika ukulima.*
- *Dadake anafanya kazi katika duka la kuuza matunda na mboga*
- *Dadake Wangari ana madeni mengi.*

Kiwango cha elimu: *Darasa la 8*

Mtazamo kwa pesa: *Kutumia pesa bila kujali*

Sifa za Kifedha:

- *Anavutiwa na taasisi rasmi za kifedha*

Malengo:

- *Angependa kuhamia Qatar kufanya kazi kama mlezi ili aweke akiba ya pesa*
- *Katika muda mrefu angependa kurejea nchini na kuwa na biashara yake mwenyewe*
- *Angependa kuendelea na masomo*
- *Anataka kupanga maisha yake ya kifedha*

Wahusika wadogo:

- *Wazazi wa Wangari, Ochieng na Akinyi*
- *Dadake, Malaika*
- *Rafiki yake, Wangi*

A

WEKA MALENGO NA UWASILIANE KATIKA FAMILIA YAKO

A1. Je, methali ifuatayo inamaanisha nini? “ Ikiwa mtu hajui anaelekea bandari gani, basi hakuna upepo utakaomfaa.”

- ☐ **a.** Unahitaji upepo ili kusafiri baharini.
- ☐ **b.** Ni rahisi kutimiza miradi ya maisha yako ikiwa unajua unakoelekea na ikiwa utaweka malengo madhubuti.
- ☐ **c.** Ni rahisi kuelekeza mashua yako wakati kuna upepo.

A2. Ni njia gani bora zaidi ya kutimiza malengo yako ya baadaye katika siku zijazo?

- ☐ **a.** Kuwa na malengo ya muda mfupi na ya muda mrefu na kuweka akiba kila mara ili kuyafikia
- ☐ **b.** Kuwa na malengo na matumaini kwa yatafikiwa. Ni muhimu kujiamini.
- ☐ **c.** Mimi bado ni mdogo sana kuwa na malengo ya siku zijazo, naweza kufikiri masuala haya baadaye.

A3. Wazazi wako wanakupigia simu kuomba pesa tena kwa ajili ya sherehe iliyoko kijijini

- ☐ **a.** Nitawatumia pesa mara moja kwa kuwa unastahili kufanya kile wazazi wanataka kila mara.
- ☐ **b.** Sikubaliani kamwe na nitakataa kutuma pesa zozote.
- ☐ **c.** Nitajadili nao ili kuelewa mahitaji yao vyema zaidi na kutafuta njia ya kuwasaidia huku nikizangatia kwamba nina malengo yangu na mpango wangu wa kuweka akiba.

A4. Mpango wa kuweka akiba ni nini?

- ☐ **a.** Ni bidhaa ya kifedha.
- ☐ **b.** Mpango ambapo unaweza kuona malengo yako, gharama zake, tarehe ambapo ungependa kutimiza malengo yako, na kiasi ambacho sharti uweke akiba ili uyafikie.
- ☐ **c.** Ni kisanduku cha pesa.

A5. Nini unapaswa kufanya kabla ya kuamua iwapo unapaswa kuhama?

- ☐ **a.** Napaswa kwenda benki na kuangalia iwapo ninaweza kukopa pesa za kuhama.
- ☐ **b.** Napaswa kuorodhesha manufaa na udhaifu wote, kuhesabu kiasi ambacho itagharimu, na kufanya uamuzi wa busara.
- ☐ **c.** Napaswa kusikiliza tu na kuwaamini watu ambao wamehama tayari.

A6. Je, unawezaje kuhesabu gharama ya kifedha ya uhamaji?

- ☐ **a.** Kwa kuorodhesha gharama zote za maandalizi, gharama wakati wa safari, gharama baada ya kufika, na gharama za familia yangu niliyoiacha nyumbani.
- ☐ **b.** Kwa kukadiria gharama ya kusafiri hadi nchi unakosafiri.
- ☐ **c.** Kwa kusikiliza masimulizi ya wahamiaji na waliorejea.

Majibu: A1:b; A2:a; A3:c; A4:b, A5:b, A6:a

1. WEKA MALENGO YAKO

UJELEZI

Lengo ni kitu ambacho unataka kufanya. Kuweka malengo hukusaidia kufafanua kile ambacho ungependa kufanya katika maisha na kwa hivyo kujua kile unachohitajika kufanya ili kutimiza malengo yako.

Hebu tupate kumfahamu Gloria, mmojawapo wa wahusika wetu.

Uchunguzi Kifani N°1

SIMULIZI YA GLORIA

Gloria ana umri wa miaka 29. Alihamia Qatar miaka 7 iliyopita. Huko alikutana na Gitau, ambaye pia alikuwa amehamia kutoka Kenya. Sasa ni miaka 4 tangu walipoamua kurejea nchini kwa sababu kandarasi ya Gitau ilikuwa imeisha na Gloria alikuwa akiugua sana, hakuweza kufanya kazi. Waliporejea Kenya, aliolewa na Gitau na sasa wako na watoto wawili, Kiprono na Odongo, ambao wana umri wa miaka 4 na 1 mtawalia.

Gloria anafanya kazi katika saluni iliyoko karibu. Yeye pia ni mwanachama katika kikundi cha wanawake wanaotengeneza vifaa vya kufuma na shanga. Katika kikundi hicho, wanawake hushiriki usanifu, mitindo, na nyenzo. Kisha wanauza vifaa vya kufuma katika duka la sanaa [1] au kwa wanawake wengine. Ana talanta sana. Gitau hufanya kazi mara moja katika sekta ya ujenzi, lakini sasa hivi hali ni ngumu sana.

Wakati wa usiku, baada ya watoto kulala, wao huketi pamoja sebuleni na kuzungumza kuhusu mipango yao katika siku zijazo. Gloria ana malengo mengi. Angependa kununua nyenzo mpya ili kutengeneza usanifu tofauti kwa bidhaa zake za kufuma. Pia angependa kufanya kozi ya elimu ya kifedha ili kuboresha usimamizi wake wa pesa. Gitau angependa kununua simu maizi kwa sababu simu yake ni kuukuu na tayari amepoteza kazi fulani kwa sababu simu yake haifanyi kazi vizuri. Zaidi ya hayo, wote wawili wanataka kuwatembelea wazazi wa Gitau ambao wanaishi Nakuru, kwa kuwa hawajawatembelea tangu Odongo alipozaliwa.

Kwa muda mrefu, Gloria ametamani kuwa na saluni yake mwenyewe na ameazimia kutenga kiasi fulani cha pesa ili kutimiza lengo hili hivi karibuni. Wote wawili pia wana ndoto ya kununua ploti na kujenga nyumba yao binafsi.

Ndoto za Gloria ni zipi? Ziandike hapa!

KISAIDIZI CHA MAFUNZO A.1.1.

Malengo yangu

Je, umewahi kutafakari juu ya malengo yako?

Ikiwa ndiyo, yaandike au uyachore hapa!



Ya muda mrefu

Ya muda mfupi



n Malengo ya Kibinafsi

Ya muda mrefu

Ya muda mfupi



n Malengo ya Familia

KUMBUKA

Malengo yako yote ni muhimu! Baadhi ya malengo yanaweza kutimizwa kwa haraka kuliko mengine.

⚠ **MUHIMU: usimamizi mzuri wa pesa zako unaweza kupunguza viwango vyako vya msongo**

2. TATHMINI GHARAMA ZA MALENGO YAKO NA VIPAUMBELE VYAKO

Je unajua gharama ya malengo yako?

Je unajua gharama ya malengo yako? Ikiwa unajua, andika gharama hizo kando ya malengo ambayo umeandika au kuchora hapo juu. Ikiwa hujui, ni muhimu sana kujua gharama husika. Hii ndio njia ya pekee ya kujua kiasi cha pesa ambacho unahitaji ili kutimiza malengo yako. Kwa sasa, unaweza kuonyesha gharama ya kukadiria ambayo unaweza kusahihisha baadaye.

Kisha weka vipaumbele kwa malengo ukionyesha 1 kwa lengo lililo muhimu zaidi, 2 kwa lengo la pili kwa umuhimu na kadhalika.

NAMBARI	LENGO LA KIBINAFSI AU LA FAMILIA	LENGO	GHARAMA YA KUKADIRIWA

KUMBUKA

Kwa jumla, ni rahisi kutimiza malengo ikiwa utapanga mapema na kukusanya taarifa zote ambazo unahitaji ili kufanya uamuzi wa busara. Ni muhimu tutathmini itagharimu kiasi gani kutimiza malengo yetu. Utafiti wa kina wakati mwingine ni muhimu (kusaka taarifa kutoka kwa wasambazaji, kutafitia mielekeo ya soko n.k.).

Unapaswa kuchunguza bei ya malengo yako kila mara. Kumbuka kuangalia masoko mtandaoni. Wakati mwingine huenda hata ukapata bidhaa nzuri sana za mitumba.

Usisahau kwamba bei huongezeka kadri ya wakati! Kwa hivyo, weka nafasi, yaani weka akiba zaidi, ikiwa gharama za kutimiza malengo yako zitaongezeka katika miaka michache ijayo

3. FANYA MPANGO WA KUWEKA AKIBA ILI KUTIMIZA MALENGO YAKO

Uchunguzi Kifani N°2

MPANGO WA OTIENO WA KUWEKA AKIBA

Otieno ana umri wa miaka 48. Aliishi Saudi Arabia lakini alikuwa mhamiaji haramu na akafurushwa miaka mitano iliyopita. Kwa sasa, anaishi na mke wake Mwende na watoto wao wanne, Jabali (17), Kariuki (12), Adhra (10) na Odhiambo (5). Kwa sasa anaendesha biashara ya duka ndogo la kuoka kwa pamoja na mkewe, Mwende. Duka hili la kuoka limesajiliwa rasmi.

Wakati mwingine jioni, wakati watoto wanacheza, Otieno na Mwende huzungumza kuhusu maisha yao ya baadaye. Wako na malengo mengi, lakini wote wanajua kwamba itakuwa changamoto kuyatimiza yote. Otieno anajua kwamba bintiye Andra amekuwa akitamani baiskeli kwa muda mrefu, kwa hivyo walitaka kumnunulia baiskeli kwa siku yake ya kuzaliwa inayofuata. Mwende angependa kumnunulia viatu mwanaye mdogo zaidi, Odhiambo. Kufikia sasa Odhiambo amekuwa akivaa nguo na viatu vya ndugu zake wakubwa, lakini amekua sana na viatu hivyo havimtoshi tena. Isitoshe, wote wawili wako na ndoto ya kununua friza kwa duka lao la kuoka na kusomea uokaji wa vitobosha ili kuandaa bidhaa mpya. Mwishowe, Otieno anataka kujenga chumba cha ziada katika nyumba yao. Kwa kuwa anajua masuala ya ujenzi, anahitaji tu kununua nyenzo za ujenzi huo.

Otieno amekadiria gharama ya kila lengo na amegundua kwamba friza ni ghali mno, kwa hivyo wameamua kuahirisha lengo hilo kwa sasa. Wameweka tarehe mpya ambapo wanaweza kutimiza malengo yote yaliyosalia. Amehesabu kiasi cha pesa wanachohitaji kuweka akiba kila mwezi kwa ajili ya lengo hili. Ametengeneza kile tunachokiita mpango wa kuweka akiba. Hii imempa taswira bayana ya kile ambacho Otieno na Mwende wanahitaji kuweka akiba kila mwezi ili kutimiza malengo yao.

Kwa hivyo, hebu tuangalie mpango wa Otieno wa kuweka akiba!

Kwa hivyo, hebu tuangalie mpango wa Otieno wa kuweka akiba!

MPANGO WANGU WA KUWEKA AKIBA

Malengo yangu	Tarehe ambayo nataka kutimiza Lengo langu	Gharama ya lengo langu	Idadi ya miezi kabla ya tarehe ya kutimiza lengo langu	Vyanzo vingine vya ufadhili (ikiwa inahusika)	Kiasi ninachohitaji kuweka akiba kwa mwezi ili kutimiza lengo langu
Malengo ya muda mfupi (chini ya miezi 12):					
Kumnunua Odhiambo vipya vipya	Novemba mwaka huu	3,900	Miezi 3		Shilingi 1,300
Malengo ya muda wa wastani (mwaka 1 hadi 3):					
Kununua baiskeli Adhra	Septemba Mwaka ujao	10,000	Miezi 12	Atapokea kipunguzo cha asilimia 25% ikiwa atatoa baiskeli nzee kama sehemu ya malipo. Watafanya hivi kwa kutumia baiskeli nzee ya Jabani.	Shilingi 635
Malengo ya muda mrefu (zaidi ya miaka 3):					
Kununua nyenzo za kujenga chumba cha ziada katika nyumba yao	Januari, ndani ya miaka 3	54,000	Miezi 36		Shilingi 1,500
Jumla ya pesa ninazohitaji kuweka akiba kila mwezi ili kufikia malengo yangu yote (Jumla ya pesa katika safu wima ya mkono wa kulia):					Shilingi 3325

⚠ **MUHIMU: Baada ya Otieno kufikia malengo yake ya muda mfupi, atahitaji kurekebisha mpango wake wa kuweka akiba na pesa ambazo anahitaji kutenga kila mwezi ili kufikia malengo yake mengine.**

KISAIDIZI CHA MAFUNZO A1.2

Mpango wangu wa kuweka akiba

Sasa ni zamu yako!

Sasa hebu tuandae muhtasari na kujaza jedwali lililopo hapa chini kwa taarifa ambayo umeifikiria: malengo, vipaumbele, tarehe ambapo unataka kutimiza malengo yako, na vyanzo vingine vya ufadhili.

MPANGO WANGU WA KUWEKA AKIBA					
Malengo yangu	Tarehe ambapo nataka kutimiza malengo yangu	Gharama ya kufikia lengo langu	Idadi ya miezi iliyosalia ili kutimiza lengo langu	Vyanzo vingine vya ufadhili (kwa hiari)	Kiasi ninachohitaji kuweka akiba kila mwezi ili kufikia lengo langu
Malengo ya muda mfupi (chini ya miezi 12)					
Malengo ya muda wa wastani (mwaka 1 hadi 3):					
Malengo ya muda mrefu (zaidi ya miaka 3):					
Jumla ya pesa ninazohitaji kuweka akiba kila mwezi ili kufikia malengo yangu yote (Jumla ya pesa katika safu wima ya mkono wa kulia):					

ZAMU YAKO

Nahitaji kuweka akiba

.. . .

kila mwezi ili kutimiza malengo yangu yote.

Kuwa mwangalifu! Kama haiwezekani kwako kuweka akiba ya kiasi hicho kila mwezi, unahitaji kurekebisha malengo yako

kwa kupunguza gharama zake, au kwa kuondoa baadhi ya malengo kwa sasa, au kwa kuahirisha tarehe ambapo ulitaka kutimiza baadhi ya malengo yako.

Unaweza kufanya hivyo kwa kuangalia jinsi ulivyotoa vipaumbele kwa malengo yako: kwa mfano, hutabadilisha malengo yako ya 1 na 2 lakini huenda ukahitaji kubadilisha malengo yako 3 na 4.

KIDOKEZO: Kutengeneza mpango wako wa kuweka akiba kidijitali, kwa mfano kwa kutumia ukurasa wa Excel, unaweza kuwa mzuri sana ili kufuatilia na kurekebisha hali yako inapobadilika

⚠ MUHIMU

Kutengeneza mpango wa akiba kunaweza kusababisha mfadhaiko fulani, hasa ikiwa huwezi kuweka akiba ya kiasi ulichotaka Usijisukume! Kila mara kumbuka unaweza kurekebisha mpango wako wa kuweka akiba.

MUHTASARI

4. ZUNGUMZA NA FAMILIA YAKO KUHUSU MALENGO YAKO!

USHAURI WA KUJADILI MALENGO YAKO NA FAMILIA YAKO

- Tafakari vizuri kuhusu kile unachotaka (na kwa nini unakitaka) kabla ya kuzungumza na familia yako.
- Usiogope kuzungumza kuhusu malengo yako. Wanaume na wanawake wote - vijana au wazee- wana haki ya kujiwekea malengo.
- Tafuta marafiki katika familia yako: watu ambao unaweza kuzungumza nao kabla na ambao wanaweza kukusaidia, watu ambao wanaheshimika katika familia.
- Kuzungumza kuhusu malengo yako na mwenzi wako na/au watu wengine wa familia, chagua wakati unaofaa, tenga muda ambapo wanapatikana.
- Jiamini unapozungumza kuhusu malengo yako na usikilize maoni ya watu wengine bila kukatiza.
- Heshimu watu wa familia yako na usiwe na misimamo mikali.
- Kama kuna kutokubaliana, chunguza suala na utafute suluhu yenye mwafaka ambayo itawanufaisha watu wote katika familia hiyo.

CHA KUFANYA...	CHA KUTOFANYA
• Jiamini • Eleza wazi kile unachotaka • Sikiliza mwenzi wako • Usiwe na msimamo mkali na uwe mtulivu • Eleza maoni yako, hata kama unaheshimu mtu huyo mwingine. • Usikose makini au kuwa mwenye kiburi • Usipayuke • Usikatize	• Tambua mitazamo ya mtu huyo mwingine • Onyesha heshima • Usikasirike • Usiwe mpyaro au mwenye matusi • Usirudie hoja ile ile mara kadhaa • Usiyakatae maoni ya mtu huyo mwingine mara moja • Usionyeshe kujikinga • Usikose subira

Muhimu: Kuzungumza kuhusu pesa kunaweza kuibua hisia nyingi. Jaribu kutafuta mtu ambaye unamwamini uzungumze naye kuhusu hili. Kutozungumza kuhusu hisia zako kutakuwa na athari hasi kwa afya yako ya akili.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO A2.1

Zoezi la maonyesho ya maigizo: mgogoro na majadiliano

MGOGORO 1

Gloria kila wakati hujaribu kutenga pesa ili atimize malengo yake. Siku chache zilizopita, rafiki yake, Njambi aliuliza ikiwa angemkopesha pesa fulani alipie madeni fulani. Gloria angependa kumsaidia rafiki yake lakini pia anafikiria kuhusu kuweka akiba kadri awezavyo. Je, anapaswa kufanya nini?

Andaa onyesho la maigizo likionyesha maingiliano baina ya watu walioelezwa pamoja na suluhu ambayo mtapata. Angalau mmoja wa wahusika katika onyesho la maigizo lazima ajaribu kutumia kanuni za mawasiliano yenye ufanisi.

MGOGORO 2

Rafiki wa karibu wa Mwende anafanya harusi hivi karibuni. Mwende anajadili na marafiki zake kuhusu zawadi ambayo wanapaswa kununua. Marafiki zote wanaamini kwamba wanastahili kuchanga pesa nyingi kwa sababu ni zawadi ya harusi. Mwende anataka kumchangia rafiki yake kadri awezavyo, lakini anaamini kwamba kiasi wanacholenga kiko juu sana kwake. Anaogopa kwamba marafiki wake watamfikiria kuwa anajipenda, hasa kwa vile yeye na Otieno wanaendelea vyema katika duka lao la kuoka. Je, anapaswa kufanya nini?

Andaa onyesho la maigizo likionyesha maingiliano baina ya watu walioelezwa pamoja na suluhu ambayo mtapata. Angalau mmoja wa wahusika katika onyesho la maigizo lazima ajaribu kutumia kanuni za mawasiliano yenye ufanisi.

MGOGORO 3

Mutua anataka kuhamia Kuwait haraka iwezekanavyo, kwa hivyo anahitajika kuweka akiba kadri awezavyo ili kuwa na kiasi cha fedha atakapofika na kukaa huko. Hana kazi maalum na yeye humsaidia rafiki yake Opiyo, ambaye hununua na kuuza viatu. Katika wiki chache zilizopita, Opiyo amekuwa akimhimiza Mutua kuwekeza akiba yake katika kuanzisha biashara naye na aachane na wazo la kuondoka. Mutua yuko wazi kuhusu lengo lake, lakini hataki kumkatisha tamaa rafiki yake kwani huwa anamsaidia sana. Mutua anahofia kwamba rafiki yake atamkasirikia akisema la. Je, Mutua anapaswa kufanya nini?

Andaa onyesho la maigizo likionyesha maingiliano baina ya watu walioelezwa pamoja na suluhu ambayo mtapata. Angalau mmoja wa wahusika katika onyesho la maigizo lazima ajaribu kutumia kanuni za mawasiliano yenye ufanisi.

MGOGORO 4

Wangari anataka kuhamia Qatar kufanya kazi, lakini kwa sasa, anaishi na wazazi wake, Ochieng na Akinyi. Dadake Wangari, Malaika, anafanya kazi katika duka la mboga na matunda karibu na nyumba ya wazazi wa Wangari. Siku moja jioni baada ya kazi, Malaika alienda kumtembelea dadake Wangari. Malaika anamshinikiza kwamba anapaswa ampe pesa fulani za kununulia nguo mpya, kwa vile imekuwa muda mrefu tangu aliponunua nguo mpya. Wangari angependa kumsaidia dada yake lakini pia anafikiria kuhusu kuweka akiba kadri inavyowezekana. Je, anapaswa kufanya nini?

Andaa onyesho la maigizo likionyesha maingiliano baina ya watu walioelezwa pamoja na suluhu ambayo mtapata. Angalau mmoja wa wahusika katika onyesho la maigizo lazima ajaribu kutumia kanuni za mawasiliano yenye ufanisi.

Uchunguzi Kifani N°3

MATATIZO YA GLORIA

Wakiwa wanakunywa chai na rafiki yake, Njambi, Gloria anamweleza kwamba ameamua kumwambia meneja wa saluni kwamba angependa kufanya kazi zamu ya asubuhi pekee. Anapofanya kazi zamu za usiku, anafika nyumbani usiku sana, akiwa amechoka na watoto wake wanampeza sana, hasa yule mdogo zaidi.

Anajaribu kuweka akiba zaidi kwa ajili ya siku zijazo ikiwa meneja wake hatamwelewa, na atafanya kazi saa chache. Ilikuwa vigumu kumwambia Gideu kuhusu hali hii, kwa kuwa kwa sasa hali ni ngumu kifedha, lakini anamwelewa na kumuunga mkono.

Njambi anashiriki naye kwamba aliamua kutojadili changamoto zake na mumewe. Kwa sasa anafanya kazi ya ziada katika hoteli ambapo anafanya kazi kwa sababu anahitaji kulipa madeni fulani na amelazimika kupunguza gharama zake za kibinafsi hadi kiasi cha chini zaidi ili kuendelea kuchangia bajeti ya familia.

Hata baada ya kupunguza matumizi yake ya kibinafsi, wakati mwingine hana pesa za kutosha kulipia mahitaji yake yote. Hali hii inamtatiza, lakini hataki kushiriki changamoto zake na mumewe.

UJUMBE MUHIMU

- Ni rahisi kufikia mipango yako ya maisha ikiwa unajua kile unataka na kujiwekea malengo mahususi ili kuyatimiza.
- Baadhi ya malengo yanaweza kutimizwa haraka; mengine yatachukua miaka au hata miongo. Malengo yanahitaji kubainishwa kuwa ya muda mfupi, muda wa wastani au muda mrefu.
- Malengo ya watu hubadilika kadri ya mpito wa maisha na watu tofauti katika familia watakuwa na malengo tofauti. Ni muhimu kufanya malengo tofauti ya watu wa familia yapatane na kila mmoja.
- Mawasiliano mazuri yanahitajika katika familia zote, haswa katika familia zilizo na jamaa wanaoishi katika mji wa mbali au eneo au nchi ya mbali.
- Kubainisha malengo yako na kueleza tofauti baina ya mambo ya kufikirika na ukweli katika kuweka malengo hurahisisha kuyafikia.
- Ni muhimu kutafuta taarifa ya kutegemewa katika kutathmini thamani na gharama ya kufikia malengo yako. Hakikisha umeangalia masoko na watoa huduma mbalimbali mtandaoni.
- Unahitaji pia kuweza kurekebisha malengo yako ikiwa ni ghali mno, na kukubali mabadiliko (katika hali ambapo mabadiliko yanatokea katika hali yako ya kifedha au kijamii).
- Kuwa na mpango wa kuweka akiba kidijitali katika ukurasa wa Excel ni wazo nzuri ili kuweza kufanya marekebisho kwa urahisi.
- Kuzingatia malengo yako ni njia yenye uhakika ya kufanikiwa.
- Kuweka mpango wa kuweka akiba kunakusaidia kuyatimiza malengo kwa urahisi zaidi.

5. AMUA IWAPO KUHAMA NDILO CHAGUO SAHIHI KWAKO

Uchunguzi Kifani N°4

MTAZAMO WA MAMAKE WANGARI KUHUSU UHAMAJI WA BINTIYE

Akinyi, mama ya Wangari na Malaika, anakutana na rafiki yake sokoni na kushiriki naye maoni kuhusu wazo la Wangari kuhamia Qatar. Miaka mitano iliyopita, Malaika alihamia Qatar. Akinyi alikuwa na furaha sana kwa fursa ambayo bintiye amepata. Hata hivyo, bado alikuwa na hofu kwamba bintiye atahitajika kuishi ughaibuni, mbali na nyumbani. Malaika aliwatumia pesa kila mwezi na ziliwasaidia sana katika miezi iliyokuwa migumu. Wakati huo pia, Wangari alikuwa mdogo sana na hakuwa akifanya kazi nao. Kwa hali hiyo, uamuzi wa Malaika kuhama ulikuwa baraka ya kifedha kwao.

Hata hivyo, ilimaanisha pia kwamba walikuwa na usaidizi mdogo nyumbani na Wangari alilazimika kushughulikia baadhi ya majukumu nyumbani.

Tangu Malaika aliporejea, haishi nao tena, lakini sasa ni Wangari ambaye anataka kuhamia Qatar. Akinyi ana uhakika kwamba atampeza sana na anataka Wangari ajifanyie maamuzi, lakini anajua kwamba itakuwa vigumu kwake na babake ikiwa Wangari ataamua kuondoka.

⚠ **TANBIHI: Mara nyingi watu hufikiria tu kuhusu manufaa ya kuhama. Lakini uhamiaji pia una hasara zake.**

Manufaa na hasara za uhamiaji (Kutoka mtazamo wa mhamaji)

Manufaa	Hasara
• Kupata pesa zaidi. • Kuweza kusaidia familia kutimiza mahitaji ya kimsingi: chakula, afya, elimu, umeme... • Kujifunza stadi mpya. • Kufanya kazi mpya na kupata tajriba za maisha. • Kuwa na hisia za uhuru na kujitegemea.	• Uhamiaji huenda ukahusisha kuchukua madeni ambayo huenda ikawa vigumu kuyalipa. • Huenda ikachukua muda kupata kazi ughaibuni. • Gharama ya juu ya maisha katika nchi unayohamia. • Hofu ya kila mara ya kufurushwa (ikiwa upo katika nchi hiyo kwa njia haramu) • Hatari za kimazingira za kazi hatari na tishio la dhuluma ya kingono (hasa ikiwa upo katika nchi hiyo kwa njia haramu). • Matarajio ya familia kwamba utakuwa unapata pesa nyingi. • Upweke na kutengwa. • Unyanyapaa wa kijamii unaporudi kutoka ughaibuni

UJUMBE MUHIMU

- Watu huamua kuhama kwa sababu mbalimbali: kupata pesa zaidi, kuwa na tajriba tofauti, kusoma, kupata stadi mpya, kuondokea migogoro katika nchi wanazotoka...
- Unahitaji kuelewa manufaa ya kuhamia, yaani, kile unachoweza kufikia kupitia uhamiaji. Vilevile unahitaji kuchanganua hasara au gharama, yaani, kile ambacho wewe na familia yako mnaweza kupoteza kutokana na uhamiaji.
- Manufaa na hasara hizi za uhamiaji zinaweza kuhusishwa na pesa lakini pia kwa mahusiano ya kijamii na ya familia.
- Taarifa nyingi zisizokuwa za ukweli zinasambazwa kuhusu uhamiaji: kinyume na kile watu wanasema, pesa haziokotwi popote, nyumbani au ughaibuni!

6. HESABU GHARAMA ZA KIFEDHA ZA UHAMIAJI

Uhamiaji ni ghali, lakini je, unajua gharama halisi ya kuhama? Je, unaweza kutofautisha baina ya gharama tofauti?

MUHTASARI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO A3.1

Uchanganuzi wa kina wa Gharama za kifedha za uhamaji

Nafikiria Kuhama: ....

....

....

Ninakolenga:..

	ITAGHARIMU NINI?	NITALIPIA VIPI?
Gharama za maandalizi		
Gharama wakati wa safari		
Gharama katika mji au nchi ninakohamia		
Gharama baada ya kurejea		
Gharama za familia yangu nyumbani		
Jumla ya gharama za uhamiaji		

MUHIMU: Ni muhimu sana kukadiria manufaa dhidi ya hasara, kwako na kwa familia yako, kabla ya kuzungumza kuhusu uamuzi wa kuhama.

Ujumbe muhimu

- Jedwali hili ni kifaa muhimu ambacho wewe na familia yako mnaweza kutumia kukadiria kiasi ambacho itagharimu kuhamia.
- Ikiwa unajua gharama, basi upo katika nafasi bora ya kukadiria ikiwa manufaa yanapiku hasara, na iwapo itakuwa ya manufaa kwa mtu wa familia kwenda kufanya kazi ughaibuni (au kwa mhamiaji kurejea nyumbani).
- Kumbuka kwamba ni vigumu kujua gharama halisi ya uhamiaji wa mfanyakazi. Ili kufanya makadirio sahihi kadri iwezekanavyo, na kuwa na taswira kamili ya fursa na changamoto za kwenda kuishi na kufanya kazi ughaibuni, familia zinaweza kutafuta taarifa kutoka vyanzo mbalimbali: taasisi za umma kama vile Vituo vya Rasilimali za Wahamiaji, miungano ya wafanyakazi, Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na wahamiaji waliorejea.
- Usisikilize kila kitu watu wanasema kuhusu uhamiaji; kuna hadithi nyingi ambazo si za kweli na wakati mwingine watu hawaelezi ukweli kamili kwa sababu wanataka kujikinga. Kinyume na fununu, barabara hazijaundwa kwa dhahabu, iwe nyumbani au ughaibuni!

MUHTASARI

B

KUSIMAMIA MAPATO YAKO KWA BUSARA

B1. Ni mwisho wa mwezi; ndio nimepokea mshahara wangu:

☐ **a.** Nakimbia sokoni kununua jaketi nzuri niliyoiona siku nyingine.
☐ **b.** Natenga sehemu ya mshahara wangu kufikia malengo yangu.
☐ **c.** Nanunua zawadi kubwa kwa siku ya kuzaliwa ya rafiki yangu.

B2. Bajeti ni:

☐ **a.** Kifaa cha kuamua, kupanga na kutumia pesa ili kufikia malengo yako.
☐ **b.** Karatasi ya kurekodi matumizi.
☐ **c.** Ni jedwali.

B4. Je, ni sehemu gani tatu kuu za bajeti?

☐ **a.** Tarehe, mapato na matumizi.
☐ **b.** Mapato, matumizi na akiba.
☐ **c.** Matumizi, mapato na sahihi.

B5. Nitafanya nini ili kufuata bajeti yangu?

☐ **a.** Niko na majukumu mengi kiasi kwamba siwezi kufuata bajeti yangu.
☐ **b.** Sifanyi bajeti yoyote kwa sababu naamini kudura.
☐ **c.** Natumia karatasi za ufuatiliaji ili kurekodi matumizi na mapato yangu.

1. KUWA MTUMIA PESA MAHIRI!

MASWALI

- Je, wewe ni mtu ambaye anapenda kutumia pesa au mtu ambaye anapenda kuweka akiba?
- Kwa mfano, je, wewe mara nyingi huacha kufanya mambo unayotaka?

UJELEZI

Uwekaji akiba una maana ya kutotumia pesa zote na kutenga sehemu yake kwa ajili ya malengo maalum siku zijazo. Inamaanisha kutenga sehemu ndogo au kiasi kikubwa cha pesa, kila wakati au mara kwa mara.

ZOEZI

Kulingana na hali yako binafsi, chagua kati ya matumizi muhimu (tunayaita mahitaji) na matumizi ya hiari (tunayaita matamanio)! Zungushia mviringo picha zinazolingana na mahitaji ili uweze kuzitofautisha na matamanio.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B1.1

Kadi za picha za matamanio na mahitaji

Ningependa kununua…

Mahitaji yangu	Yatagharimu kiasi gani?
Jumla ya mahitaji	
Matamanio yangu	**Yatagharimu kiasi gani?**
Jumla ya matamanio	

TANBIHI!

Kuwa mwangalifu! Wakati mwingine, kitu kinaweza kikawa ni mahitaji kwa mtu fulani lakini matamanio kwa mtu mwingine. Kwa mfano, rununu, mtu anaweza kuhitaji kwa ajili ya biashara, huku wengine wakihitaji tu kuwasiliana na jamaa na marafiki.

Je, niko na pesa za kutosha kununua vitu vyote nilivyoorodhesha?

☐ Ndiyo ☐ La

Ikiwa sina pesa za kutosha, nitaamua kuacha matamanio yafuatayo:

MUHTASARI

MUHIMU: Unaweza kutumia pesa kujipa raha. Watu fulani hueleza hisia hii kama ulevi wa muda. Lakini utahisi hivi kwa muda mfupi tu. Kuwa mwangalifu! Ikiwa bajeti yako hairuhusu, tumia muda kila mara kutofautisha baina ya mahitaji na matamanio. Vinginevyo kutokuwa na pesa za kutosha baadaye kukidhi mahitaji yako kunaweza kukupa mfadhaiko.

Soma masimulizi ya wahusika hawa na utafakari kuhusu kile kinachowafanyikia. Nini wangefanya tofauti?

Uchunguzi Kifani N°1

FAMILIA YA MUTUA INAKABILIWA NA DHARURA

Tangu Mutua aliporejea kutoka Lebanon, amekuwa akiishi na wazazi wake Kalekye na Kyalo. Kyalo anafanya kazi katika dobi na ndiye mchuma riziki mkuu katika familia yao.



Wiki jana, Kyalo alianza kuugua. Hangeweza kupumua vyema na alikuwa na homa kidogo. Mutua na Kalekye wako na wasiwasi na wanahitaji kununua dawa kwa dharura. Waliamua kwenda kwenye duka la dawa lililo karibu ili wazinunue haraka. Kwa kuwa ilikuwa mwisho wa mwezi Kyalo alikuwa apokee mshahara wake wiki inayofuata, Mutua alihitaji kukopa pesa kutoka kwa rafiki yake, Opiyo.

Opiyo anamkopesha Mutua Shilingi 800 na wanakubaliana kwamba Mutua atamlipa mwisho wa mwezi zikiwa shilingi 900. Mutua ametumia pesa hizo kununua dawa kutoka duka la kuuza dawa. Kyalo anapata nafuu haraka baada ya kumeza dawa hizo.

Uchunguzi Kifani N°2

NJERI, RAFIKI YA OTIENO NA MWENDE, YUKO NA TATIZO

Otieno na Mwende wako na uhusiano wa karibu na majirani wao, Njeri na Owuor. Njeri anaendesha biashara ya duka ndogo katika njia iliyo karibu na nyumba yao. Duka la Njeri limekuwa likiendelea vyema siku za hivi karibuni. Amejua jinsi ya kuwa na nidhamu katika kutumia pesa na amekuwa akipata faida nyingi kwa muda sasa. Kwa kuwa haelewi taasisi za kifedha, amekuwa akimpa mumewe, Owuor, sehemu ya mapato yake mara kwa mara, ili aweke katika akaunti ya benki. Siku moja, anarudi nyumbani, akifikiria kumwomba Owuor pesa fulani kutoka kwa akaunti ya biashara, kwa kuwa anataka kununua bidhaa mpya kwa duka lake. Anapofika, anagundua kwamba mumewe amenunua gari kuu kuu. Anapoomba pesa za duka, mumewe anasema kwamba haiwezekani kutumia pesa hizo kwa sasa. Njeri anakasirika na kwenda benki moja kwa moja kuangalia akaunti na kutoa pesa zilizosalia katika akaunti hiyo.
Anapozungumza na afisa wa benki, anapata kujua kwamba akaunti imesajiliwa katika jina la mumewe na kwamba hawezi kutoa kiasi kidogo cha pesa zilizosaliwa katika akaunti hiyo. Anakasirika sana.

VIDOKEZO VYA KUWEKA AKIBA

- Tenga kiasi kidogo cha pesa kila siku au kila wiki.
- Usinunue vitu vipya ikiwa ulivyonavyo bado vinafanya kazi au ikiwa vinaweza kurekebishwa.
- Nunulia familia yako zawadi chache. Zungumza na familia yako kwanza na mkubaliane kuhusu usaidizi wako.
- Ikiwezekana, tumia pesa chache kwa sherehe za kitamaduni au kijamii.
- Weka pesa kidogo kwenye pochi lako - unaweza kuanza kutafuta mbinu za kufanya malipo kama vile pochi za kidijitali na kadi za benki.
- Ikiwa utawatumia wazazi wako pesa au jamaa wengine, usiwatumie pesa zote, weka sehemu yako kwa ajili ya mahitaji na dharura zako binafsi.
- Kila siku kumbuka malengo yako ya muda mrefu kama kichocheo cha kuweka akiba!

UJUMBE MUHIMU

- Unapaswa kuweza kutofautisha baina ya matumizi ya msingi na ya hiari.
- Kuweka akiba kwa ajili ya dharura: kuweka akiba ni muhimu, na hitaji la msingi zaidi.
- "Simamia vyema kile ambacho wengine wamechuma"
- Kuweka akiba ina maana ya kujinyima matamanio ya sasa ili uwekeze na kutimiza lengo katika siku zijazo.
- Uwekaji akiba unakupatia usalama.

MUHTASARI

2. UNDA BAJETI YAKO!

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.2.1

Picha za kuunda bajeti (kwa vikundi vilivyo na ujuzi finyu wa kusoma na kuandika)



KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.2.2

Bajeti tupu ya Mhusika

Hebu tupate kujua zaidi kuhusu Gloria na jinsi anaunda bajeti yake.

BAJETI YA FAMILIA YA GLORIA

VYANZO VYA MAPATO	
Mapato ya Kudumu	
Mchango wa Gloria kwa bajeti ya familia	
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	
Mapato yanayobadilika	
Mchango wa Gitau kwa bajeti ya familia	
Mapato kutokana na kuuza samani kuu kuu	
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	
JUMLA YA MAPATO	
MATUMIZI	
Mahitaji ya kimsingi (mahitaji)	
Kodi	
Gesi, umeme na maji	
Chakula	
Usafiri na usafirishaji (gari au usafiri wa umma)	
Huduma za Afya/madawa	
Mawasiliano (gharama za simu)	
Jumla ndogo (mahitaji)	16400
Matumizi ya hiari (matamanio)	
Safari ya Nakuru	
Mlo usio ghali katika hoteli ya pale mtaani	
Jumla ndogo (matamanio)	3000
JUMLA YA GHARAMA	19400
MAPATO -MATUMIZI	1100

Uchunguzi Kifai N°3

BAJETI YA FAMILIA YA GLORIA - SEHEMU YA 1

Jana ilikuwa siku ya mwisho ya mwezi na Gloria na Gitau waliamua kukagua mapato yao. Kwanza, wanaangalia mapato na gharama za bajeti ya kibinafsi ya Gloria. Wanafikia hitimisho kwamba mapato halisi ni Shilingi 11,800. Kama ilivyokuwa miezi iliyopita, Gloria aliamua kuchangia kiasi cha kudumu cha Shilingi 10,000 kwa matumizi ya familia na kuweka Shilingi 1,800 kwa bajeti yake ya kibinafsi.

Mapato ya Gitau kutokana na kazi zake za kila siku katika ujenzi si thabiti na hubadilika kutoka mwezi mmoja hadi mwingine. Katika mwezi huu, anatarajia ataweza kuchangia jumla ya Shilingi 8,500 kwa bajeti ya familia. Pia waliuza meza ya zamani iliyojengwa kwa mbao ambayo Gitau alikuwa amekarabati katika muda wake wa mapumziko. Jirani aliinunua kwa Shilingi 2,000.

Uchunguzi Kifani N°4

BAJETI YA FAMILIA YA GLORIA - SEHEMU YA 2

Baada ya Gloria na Gitau kuchunguza mapato yao kwa mwezi ujao, wanaanza kupanga jinsi watatumia pesa hizo. Kwanza, watalipa kodi yao (Shilingi 7,000) Baada ya hapo, wanatambua kwamba watatumia Shilingi 1,500 kwa umeme na huduma nyinginezo. Wanakadiria Shilingi 4,500 kwa chakula, Shilingi 800 kwa usafiri, na ada ya Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya ya Shilingi 2,000. Gharama zao za malipo ya simu ni takriban Shilingi 600.
Safari ya kuwatembelea wazazi wa Gitau itagharimu Shilingi 1,800. Pia wangependa kwenda kwenye hoteli ya hapo mtaani kwao, ambapo vyakula sio ghali na iko na huduma nzuri. Itagharimu angalau Shilingi 1,200.

Gloria anatenga sehemu ya mapato yake halisi kwa ajili ya matumizi ya kibinafsi. Baada ya kuchangia bajeti ya familia, anapanga kutumia shilingi 900 kujinunulia nguo mpya.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.2.3

Bajeti ya familia ya mhusika

BAJETI YA FAMILIA YA GLORIA

VYANZO VYA MAPATO	
Mapato ya Kudumu	
Mchango wa Gloria kwa bajeti ya familia	10000
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	10000
Mapato yanayobadilika	
Mchango wa Gitau kwa bajeti ya familia	8500
Mapato kutokana na kuuza samani kuu kuu	2000
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	10500
JUMLA YA MAPATO	20500
MATUMIZI	
Mahitaji ya kimsingi (mahitaji)	
Kodi	7000
Gesi, umeme na maji	1500
Chakula	4500
Usafiri na usafirishaji (gari au usafiri wa umma)	800
Huduma za Afya/madawa	2000
Mawasiliano (gharama za simu)	600
Jumla ndogo (mahitaji)	
Matumizi ya hiari (matamanio)	
Safari ya Nakuru	1800
Mlo usio ghali katika hoteli ya pale mtaani	1200
Jumla ndogo (matamanio)	3000
JUMLA YA GHARAMA	19400
MAPATO - MATUMIZI	1100



KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.2.4

Bajeti ya kibinafsi ya mhusika

BAJETI YA KIBINAFSI YA GLORIA	
VYANZO VYA MAPATO Mpato ya kudumu	
Mapato ya Gloria kutokana na kazi yake katika saluni	11000
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	11000
Mapato yanayobadilika	
Mapato halisi kutokana na uuzaji wa bidhaa za kufuma	
	800
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	800
JUMLA YA MAPATO	11800
MATUMIZI Mahitaji ya kimsingi (mahitaji)	
Mchango kwa bajeti ya familia	10000
Jumla ndogo (mahitaji)	10000
Matumizi ya hiari (matamanio)	
Nguo mpya	900
Jumla ndogo (matamanio)	900
JUMLA YA GHARAMA	10900
MAPATO-MATUMIZI	900

MASWALI

- **Je, umeshaunda bajeti?**

  ☐ **Ndiyo** ☐ **La**

- **Ikiwa umeshaunda, je umeiandika au umeiweka akilini?**

  ☐ **Nimeiandika** ☐ **Nimeiweka akilini**

UJELEZI

Bajeti ni Kifaa cha kufanyia uamuzi, kupanga na kutumia pesa ili kufikia malengo yako.

MUHIMU: Ikiwa hauendelei vizuri au una huzuni kidogo kwa sasa, huenda ikawa kazi nzito kuunda bajeti. Zungumza kuhusu jinsi unavyohisi na wapendwa wako au mtu unayemwamini na ujaribu kutafuta msaada ili kuanza kufanya bajeti yako pole pole. Usijiweke shinikizo nyingi.

ZOEZI

Umeona katika mafunzo jinsi Gloria na familia yake waliunda bajeti yao. Sasa ni zamu yako! Unda bajeti yako sasa!

Kuwa mwangalifu! Sehemu « Mapato – matumizi » kwenye sehemu ya chini ya jedwali lazima iwe chanya. Kama sio chanya, inamaanisha huna mapato ya kutosha na pesa za kutosha kwa matumizi yako yote. Pia inamaanisha kwamba huna pesa zozote za kuweka akiba ili kufikia malengo yako.

Ikiwa unatazamia matumizi makubwa katika miezi michache ijayo, anza kuweka akiba wakati wowote unapoweza, ili uweze kumudu gharama hizi kubwa na kusalia ndani ya bajeti yako.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.3.5

Bajeti yangu

BAJETI YANGU

VYANZO VYA MAPATO	Kiasi
Mapato ya Kudumu	
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	
Mapato yanayobadilika	
Jumla ndogo ya mapato yanayobadilika	
JUMLA YA MAPATO	
MATUMIZI	
Mahitaji ya kimsingi (mahitaji)	
Jumla ndogo (mahitaji)	
Matumizi ya hiari (matamanio)	
Jumla ndogo (matamanio)	
JUMLA YA GHARAMA	
MAPATO-MATUMIZI	

Hebu tuendelee na kisa cha Gloria

Uchunguzi Kifani N°5

BAJETI YA FAMILIA YA GLORIA (SEHEMU YA 3)

Inaonekana Gloria na Gitau wanakabiliwa na masuala fulani. Licha ya kuwa walikuwa wamepanga bajeti yao vyema, ujenzi katika mojawapo wa eneo ambapo Kabebe alikuwa anafanya kazi umesimamishwa kwa muda. Badala ya kuweza kuchangia Shilingi 8,500 kwa bajeti ya familia, sasa ataweza kuchangia Shilingi 7,800. Isitoshe, jirani aliamua kurejesha samani kwa kuwa haikumridhisha, kwa hivyo walilazimika kumrejeshea Shilingi 2,000 ambazo alikuwa amelipa.

Katika kiwango cha matumizi, matumizi yao ya chakula yameongezeka hadi Shilingi 5,000 badala ya Shilingi 4,500 walizokuwa wamepangia.

MUHTASARI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.2.6

Bajeti ya mhusika iliyorekebishwa

BAJETI YA FAMILIA YA GLORIA

VYANZO VYA MAPATO	
Mapato ya Kudumu	
Mchango wa mapato ya Gloria kwa bajeti ya familia	10000
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	10000
Mapato yanayobadilika	
Mchango wa Gitau kwa bajeti ya familia	7800
kutokana na kuuza samani kuu kuu	0
Jumla ndogo ya mapato ya kudumu	7800
JUMLA YA MAPATO	17800
MATUMIZI	
Mahitaji ya kimsingi (mahitaji)	
Kodi	7000
Gesi, umeme na maji	1500
Chakula	5500
Usafiri na usafirishaji (gari au usafiri wa umma)	800
Huduma za Afya/madawa	2000
Mawasiliano (gharama za simu)	600
Jumla ndogo (mahitaji)	17,400
Matumizi ya hiari (matamanio)	
Safari ya Nakuru	1800
Mlo usio ghali katika hoteli ya pale mtaani	1200
Jumla ndogo (matamanio)	3000
JUMLA YA GHARAMA	20400
MAPATO - GHARAMA	-2600

UJUMBE MUHIMU

- Kuna nyenzo inayotumiwa kusimamia mapato yako – bajeti.
- Ili kuunda bajeti yako, unahitaji kuhesabu mapato na matumizi yako. Kupitia kwa hesabu hii, unaweza kubainisha uwezo wako wa kuweka akiba, yaani kiasi ambacho unaweza kutenga kila mwezi.
- Katika hali ya dharura au kukiwa na mabadiliko katika hali yako ya kifedha, itabidi ufanye marekebisho kwenye bajeti yako ili kuweza kukidhi matumizi na kuweka akiba kwa malengo yako.
- Bajeti inaweza kukusaidia kuamua jinsi ya kutumia pesa zako na kuweka akiba ili kutimiza malengo yako.
- Kumbuka kwamba unaweza kuunda bajeti ya kidijitali kwa urahisi kwa kutumia ukurasa wa Excel. Pia kuna programu nyingi za kukusaidia kuunda bajeti yako. Ni njia nzuri ya kulinganisha kile ambacho umepanga na kile ambacho kilitokea.

3.



FUATILIA NA UHAKIKISHE UNASALIA NDANI YA BAJETI YAKO

Uchunguzi Kifani N°6

USIMAMIZI WA BAJETI YA GLORIA

Gloria na Gitau wako na mipango mingi. Wanahitaji kuweka akiba kadri wawezavyo ili waweze kuitimiza. Jana, Gitau alipokea simu kutoka kwa mamake, Mumo. Mumo alimuomba amtumie pesa kwa sababu babake, Musau, alihusika katika ajali na hakuwa na pesa za kulipia gharama za matibabu. Gloria na Gitau wako na wasiwasi kuhusu Musau na wanatuma pesa ambazo waliombwa.

Wakati wa mchana, Gloria na Gitau wanakagua bajeti yao na kugundua kwamba hawataweza kuwa na bajeti yenye usawa kutokana na matumizi haya ya ziada. Wanazungumza na kuamua kuahirisha safari ya Nakuru lakini pia wajaribu kuokoa pesa kadri wawezavyo katika matumizi ya chakula na usafiri.

Uchunguzi Kifani N°7

USIMAMIZI WA BAJETI YA OTIENO

Mwezi uliopita, Otieno aligundua kwamba hakuwa na pesa nyingi, na kwamba anastahili kuchunga matumizi yake. Jana, jirani yake, Owuor, alitaka kumuomba Pesa fulani kwa sababu gari lake jipya lilikuwa limeharibika na hakuwa na pesa za kulirekebisha. Otieno alisita: alikumbuka kwamba hakuwa na pesa za ziada katika bajeti yake na kwamba akiba yake yote ilikuwa inahitajika ili kutimiza malengo yake.

Anapotafakari kuhusu hili, anakumbuka kwamba jirani huyu, Owuor, alikuwa amemsaidia yeye na familia yake mara nyingi hapo mbeleni, hasa wakati alikuwa Saudi Arabia na Mwende alikuwa akiwatunza watoto peke yake, kwa hivyo anaamua kumkopesha pesa. Baadaye wiki hiyo, mwanawe, Kariuki, aliugua na akahitaji dawa za bei ghali. Otieno hakuwa na pesa za kutosha kununua dawa na Owuor hakuwa na pesa za kumlipa deni. Otieno analazimika kukopa pesa kutoka kwa mkopeshaji asiye rasmi.

MASWALI

•Je, Gloria alifanya nini ili kusalia ndani ya bajeti yake?

Kuna njia nyingi za kuhakikisha kwamba unasalia ndani ya bajeti yako. Unaweza kutumia ukurasa wa Excel, au programu, kama watu wengi wanavyofanya siku hizi! Kuna programu mbalimbali ambazo zinaweza kukusaidia kufuatilia pesa zako. Chukua muda ukague baadhi ya programu hizi.

Hebu sasa tujue jinsi ya kusalia ndani ya bajeti.

MUHIMU: Desturi zinaweza kuwa za manufaa katika kudumisha afya nzuri ya akili wakati mambo hayaendi vizuri. Kufuatilia bajeti yako huenda kukawa zoezi nzuri la kuzingatia na kuangalia jinsi unavyoendelea katika suala la kusalia ndani ya bajeti yako.

KIDOKEZO

Kuna programu nyingi ambazo zinaweza kukusaidia kusalia ndani ya bajeti yako. Ziangalie!

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.3.1

Karatasi ya kufuatilia mapato

KARATASI YA KUFUATILIA MAPATO

Jina:

Mwezi:

TAREHE	MAELEZO KUHUSU CHANZO CHA MAPATO	KIASI CHA MAPATO
JUMLA YA MAPATO		

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.3.2

Karatasi ya kufuatilia matumizi

KARATASI YA KUFUATILIA MATUMIZI

Jina:

Mwezi:

TAREHE	MAELEZO YA GHARAMA	KIASI KILICHOTUMIKA	IMEPANGIWA AU HAIJAPANGIWA	
			NDIYO	LA
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐

JUMLA YA GHARAMA	
JUMLA YA MAPATO	
AKIBA (=MAPATO-GHARAMA)	



VIDOKEZO VYA KUSALIA NDANI YA BAJETI YAKO

- Jikumbushe kila mara kile ulipanga kutumia.
- Weka pesa katika bajeti kushughulikia mahitaji yasiyotarajiwa.
- Weka akiba mbali ili usiitumie.
- Fuatilia kile unachotumia.
- Hakikisha hujatumia zaidi ya kile ulichopangia katika bajeti.
- Ikiwa utatumia zaidi kwa kitu kimoja, basi tumia pesa kidogo zaidi kwa kitu kingine
- Andaa orodha ya njia za kupunguza gharama zilizopangiwa.
- Shirikisha familia katika kuandaa na kufuata bajeti.
- Kumbuka kuangalia programu zilizopo za kufuatilia bajeti yako.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.3.3

Kadi za Muamala
Familia ya Gloria

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 1 Februari, Gloria alichangia Shilingi 10,000 kwa bajeti ya familia.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 1 Februari, Gitau alichangia Shilingi 7,800 kutoka kwa mapato aliyopata katika ujenzi.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 1 Februari, wanalipa Shilingi 1,500 kwa gharama za umeme na maji.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 1 Februari wanaweka Shilingi 5,500 katika bahasha kwa ajili ya gharama za chakula mwezi mzima.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 2 Februari wanaweka Shilingi 800 katika bahasha kwa ajili ya gharama za usafiri.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 10 Februari, walilipa Shilingi 7,000 za kodi.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 12 Februari wanatenga Shilingi 2,000 kwa ada ya NHIF.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 12 Februari, wanatumia Shilingi 600 kwa mawasiliano.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 15 Februari walienda katika hoteli ya hapo mtaani na kutumia Shilingi 1,200.

FAMILIA YA GLORIA

Mnamo tarehe 15 Februari, familia ya Gloria ilihitaji kurekebisha friji kwa Shilingi 400.

ZOEZI

Unaweza kutumia karatasi mbili zilizoko hapo juu zenye anwani ya "karatasi ya kufuatilia mapato na matumizi" ili kufuatilia mapato na matumizi. Hebu tuone nini kilifanyika kwa Gloria na familia yake.

KARATASI YA KUFUATILIA MAPATO

Jina: Familia ya Gloria
Mwezi: Februari

TAREHE	MAELEZO	KIASI CHA MAPATO
01.02	Mchango wa Gloria	Shilingi 10,000
01.02	Mchango wa Gitau	Shilingi 7,800
JUMLA YA MAPATO		Shilingi 17,800

KARATASI YA KUFUATILIA MATUMIZI

Jina: Familia ya Gloria
Mwezi: Februari

TAREHE	MAELEZO YA GHARAMA	KIASI KILICHOTUMIKA	IMEPANGIWIA AU HAIJAPANGWA: NDIYO	LA
01.02	Umeme na maji	Shilingi 1,500	X	
01.02	Chakula	Shilingi 5,500	X	
02.02	Usafiri	Shilingi 800	X	
10.02	Kodi	Shilingi 3,400	X	
12.02	Ada za NHIF	Shilingi 2,000	X	
12.02	Mawasiliano	Shilingi 600	X	
15.02	Hoteli ya mtaani	Shilingi 1,200	X	
15.02	Kurekebisha friji	Shilingi 400	X	
				X
JUMLA YA GHARAMA		Shilingi 15,400		
JUMLA YA MAPATO		Shilingi 17,800		
AKIBA (= MAPATO - GHARAMA)		Shilingi 2,400		

Sasa ni zamu yako.

Katika Viambatisho na hati muhimu mwishoni mwa Somo hili utapata karatasi za kufuatilia Mapato na Matumizi ambazo unaweza kutumia kufuatilia mapato na matumizi yako mwenyewe. Kwa njia hii utasalia katika bajeti yako na hatimaye utatimiza malengo yako.

UJUMBE MUHIMU

- Jikumbushe kila mara kile ulipanga kutumia.
- Weka pesa katika bajeti kushughulikia mahitaji yasiyotarajiwa.
- Shirikisha familia katika kuandaa na kufuata bajeti.
- Unastahili kujua jumla ya mapato yako. Kujua kiasi ambacho unachuma ni hatua muhimu katika kuchukua udhibiti wa pesa zako na hukusaidia kupangia matumizi mapema.
- Unahitaji pia kujua kiasi cha jumla ya gharama zako. Ni muhimu kudhibiti bajeti yako.
- Unaweza kurekebisha matumizi yako wakati unaona kwamba unatumia zaidi ya kile ulitarajia.



Kuwa mwangalifu! **Ikiwa una mapato yasiyotabirika, yaani kila mwezi unapata kiasi tofauti cha pesa, unaweza kuandaa bajeti kwa kutumia mapato ya wastani na kisha kuweka akiba wakati unapata zaidi ili kusawazisha wakati unapopata kidogo.**

4. HIFADHI REKODI ZAKO ZA KIFEDHA

Uchunguzi Kifani N°8

MUTUA ANAPOTEZA BAADHI YA RISITI

Mutua hununua bidhaa kwa deni kutoka duka la mtaani kwake. Kila mara anaponunua kitu, mwenye duka huandika alichonunua kwenye sajili yake na kumpa risiti ya kumwezesha kufuatilia gharama zake dukani. Mutua haoni haja ya kuweka risiti zake, kwa kuwa ana kumbukumbu nzuri na anakumbuka kila kitu anachonunua. Siku moja, mwanzoni mwa mwezi, alipokuwa anahitaji kulipa deni la mwenye duka, anaelezwa kuwa kiasi anachohitajika kulipa ni Shilingi 2,300. Hii ilikuwa Shilingi 300 zaidi ya kile Mutua alifikiri alihitajika kulipa. Anamweleza mwenye duka kwamba ana uhakika kuna kosa mahali. Mwenye duka anamweleza kwamba hakuna kosa, kwa kuwa hicho ndicho kiasi kilichoonyeshwa katika sajili yake, lakini ikiwa anataka, wanaweza kujumlisha risiti ambazo alimpa kama ushahidi. Wakati Mutua anasema kwamba huwa haweki risiti hizo, mwenye duka anamweleza kwamba anahitajika kulipa kiasi chote. Mutua anakasirika kwa kutoweka hati hizo.

KIDOKEZO

Kuhama kutoka malipo ya pesa taslimu hadi malipo ya kidijitali kunaweza kukusaidia sana katika kuweka rekodi za kifedha kila mara unapotumia pesa.

Uchunguzi Kifani N°9

WANGARI HUHIFADHI HATI ZAKE ZA KIFEDHA

Wakati Wangari na wazazi wake wanapokea bili ya umeme kwa nyumba yao kila mwezi, yeye huenda kwenye kampuni ya umeme na kufanya malipo. Siku moja, aligundua kwamba walikuwa wamekatiwa umeme! Kwa hasira, alienda kwenye ofisi ya kampuni ya umeme kulalamika. Akiwa pale, mfanyakazi anamweleza kuwa hajalipia umeme kwa miezi 2 sasa. Yeye ana uhakika kwamba alilipa bili zote. Mfanyakazi anamuuliza kuhusu bili iliyopigwa muhuri wa "IMELIPWA" ili kuchunguza hali hiyo. Wangari anarudi nyumbani na kuangalia katika sanduku ambapo yeye huweka rekodi za kifedha, bili, na hati muhimu. Hapo, anapata bili ya umeme iliyopigwa muhuri wa "IMELIPWA". Wangari anarejea kwenye ofisi za kampuni na kumpa mfanyakazi ushahidi wa malipo. Kampuni inarejesha umeme. Wangari anafurahi sana kwamba alihifadhi hati za kifedha kwa matukio kama haya.

MUHIMU: Ikiwa una wasiwasi mwingi unaweza kuhisi kuwa kuangalia akaunti yako ya benki, akaunti ya pochi la kidijitali au hata kukagua matumizi yako kunaweza kuonekana kuwa shughuli ambayo itakuletea mfadhaiko na usumbufu zaidi. Lakini kumbuka: kupuuza au kutofikiria kuhusu pesa kunaweza kufanya mambo kuwa mabaya zaidi siku zijazo.

VIAMBATISHO NA HATI MUHIMU

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.4.1

Karatasi ya kufuatilia mapato

KARATASI YA KUFUATILIA MAPATO YANGU

Jina:

Mwezi:

TAREHE	MAELEZO KUHUSU CHANZO CHA MAPATO	KIASI CHA MAPATO
JUMLA YA MAPATO		

KISAIDIZI CHA MAFUNZO B.4.2

Karatasi ya kufuatilia matumizi

KARATASI YA KUFUATILIA MATUMIZI YANGU

Jina:

Mwezi:

TAREHE	MAELEZO YA GHARAMA	KIASI KILICHOTUMIKA	IMEPANGIWA AU HAIJAPANGIWA	
			NDIYO	LA
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐
			☐	☐

JUMLA YA GHARAMA	
JUMLA YA MAPATO	
AKIBA (=MAPATO-GHARAMA)	

C

UFAHAMU MBINU NA MIPANGO YA KUWEKA AKIBA

C1. Je, kwa maoni yako, ni njia ipi bora zaidi ya kuweka akiba?

- ☐ **a.** Naweka pesa zangu kwenye bweni au nyumbani kwangu kwa kuwa ni rahisi zaidi
- ☐ **b.** Naweka pesa zangu benki kwa kuwa ni salama zaidi
- ☐ **c.** Naweka pesa katika chama kwa vile nina marafiki huko.
- ☐ **d.** Kila mbinu ina manufaa na hasara zake. Ninazikagua kwa makini kabla ya kuamua mbinu ambayo ni faafu zaidi kwa mahitaji yangu.

C2. Umelimbikiza akiba fulani. Ungependa kutumia akiba hii kuanzisha biashara yako ndani ya miaka michache ijayo. Je, ni akaunti gani ya akiba ambayo ni faafu zaidi kwako?

- ☐ **a.** Akaunti ya akiba ya kawaida.
- ☐ **b.** Akaunti ya akiba ya kimkataba.
- ☐ **c.** Akaunti ya amana ya muda maalum.

C3. Mojawapo ya kigezo cha kuzingatia wakati wa kuchagua mbinu ya kuweka akiba ni usalama.

- ☐ **a.** Ni kweli
- ☐ **b.** Si kweli

Majibu: C1:d; C.2:c; C3:a

1. CHAGUA MBINU YA KUWEKA AKIBA!

Kwa vile sasa umeunda bajeti yako ya kibinafsi (au bajeti ya familia yako), unajua kiasi ambacho unaweza kuweka akiba kila mwezi na kiasi cha akiba ambacho lazima uweke kwa kila lengo lako.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO C.1.1

Mbinu za Kuweka Akiba

Gloria anapendelea kuweka akiba yake kwa kutumia akaunti ya pochi la kidijitali. Kwa njia hiyo, hashawishiki kutumia pesa ambazo tayari ametenga.

Otieno ana uzoefu wa kutumia taasisi za kifedha na huwa anaweka akiba yake yote katika akaunti ya benki. Hiyo ndio mbinu bora zaidi kwake kuhakikisha usalama wa pesa hizo na asishawishike kuzitumia.



Mutua alijiunga na chama (kikundi cha kuweka akiba ndogo) na anapenda kuweka akiba yake hapo. Anapanga kutumia pesa hizo huko Kuwait.

Wangari anaweka akiba yake chini ya godoro

MASWALI

- Je, ni mbinu gani za kuweka akiba ambazo zimetumiwa na wahusika hapo juu?
- Je, mbinu hizi ni rasmi, rasmi kwa kiasi fulani au sio rasmi?
- Kila mbinu ina manufaa na hasara zake. Mwishoni mwa somo hili, katika Sehemu ya Majibu kwa mazoezi utapata jedwali ambalo linatoa muhtasari wa manufaa na hasara za kila mbinu za kuweka akiba.

KIDOKEZO

Uwekezaji katika *cryptocurrency* umekuwa uamuzi unaotumiwa na watu wengi. Hata kama uwekezaji huu unadhibitiwa na unafanywa kupitia kwa taasisi rasmi, ni muhimu sana wewe kuelewa hatari ya juu inayohusika katika mbinu hii ya uwekezaji. Ukurasa ufuatao wa wavuti kutoka kwa Benki Kuu ya Ufilipino unatoa maelezo ya haraka na Majibu kwa Maswali ya Mara kwa Mara kuhusu sarafu za kidijitali.

Kumbuka kwamba ili kujumuisha wahusika wengi zaidi katika jedwali, unaweza kufikiria kuhusu:

- Usalama wa pesa zako huko,
- Uwezekano wa kutoa pesa zako unapohitaji,
- Uwezekano wa kucheleweshwa katika kutoa pesa zako,
- Uwezo wa kuweka akiba ya kiasi kikubwa au pesa kidogo tu,
- Uwezekano wa kupata mkopo kwa kutumia akiba yako,
- Uwezekano kwamba akiba yako itazalisha pesa fulani (riba)

MUHIMU: Kuchagua mbinu salama ya kuweka akiba kunaweza kukufanya uhisi vyema zaidi. Ikiwa una wasiwasi kila mara kuhusu usalama wa pesa zako, fikiria ni suluhu gani uko nalo la kuondoa hisia hii.

FAHAMU MBINU NA MIPANGO YA KUWEKA AKIBA

ZAMU YAKO!

Najua manufaa na hasara za mbinu mbalimbali za kuweka akiba. Kwa kuangalia malengo yangu na bajeti yangu tena, nafikiri mbinu bora zaidi kwa miradi yangu ni:
Mbinu ya kuweka akiba

Malengo yangu	Mbinu ya kuweka akiba

UJUMBE MUHIMU

- Kuweka akiba kunakupatia usalama iwapo kutatokea dharura.
- Baadhi ya mahitaji/dharura huenda zikatazamiwa, zingine haziwezi. Kuweka akiba kunakuwezesha kupangia mahitaji au miradi ya siku zijazo.
- Wakati kila kitu kiko shwari, kuweka akiba pia kunakusaidia kupanga kwa ajili ya mambo ambayo ungependa kufanya au vitu ungependa kuwa navyo.
- Unahitaji kufahamu mbinu mbalimbali za kuweka akiba ili uchague mbinu ambayo ni faafu zaidi kwa mahitaji yako.
- Zingatia kwamba kuna watoaji wengi wa huduma za kifedha wanaotoa suluhu za kidijitali ambazo zimerahisisha ufunguzi wa akaunti ya akiba kuliko ilivyokuwa hapo awali.

2. CHAGUA MBINU YAKO YA KUWEKA AKIBA KWA BUSARA

Mpango wa kuweka akiba ni kama vile, akaunti ya akiba ya kawaida ambayo hutoa riba ya asilimia 1% au akaunti ya amana ya muda maalum (uliobainishwa) kwa miaka mitano. Kuna watoaji tofauti wa huduma za kifedha kukiwa na mipango mbalimbali ya kuweka akiba ambayo unaweza kuchagua.

UJELEZI

Mpango wa kuweka akiba ni mbinu ya kuweka akiba ambayo tunajua sifa zake kama vile:

- *Wepesi wa kufikia, utoaji pesa kwa urahisi*
- *Ufaafu na wepesi wa kutumia*
- *Mahitaji ya kufungua akaunti ya akiba*
- *Usalama*
- *Kiwango cha riba na manufaa ya ushuru*
- *Gharama ya akiba (ada):*
- *Uwezo wa kupata pesa*
- *Ufikiaji mtandaoni*
- *Azma na lengo la mkakati wako wa kuweka akiba*
- *Huduma kwa wateja*

Zifuatazo ni aina tatu kuu za mipango ya akiba inayotolewa na taasisi za kifedha

Akaunti ya akiba ya kawaida inatumiwa wakati unataka kuweka au kufikia pesa zako wakati wowote. Hii ndiyo akaunti ya akiba ambayo inatumika zaidi.

Akaunti ya akiba ya kimkataba inaunganisha akiba uliyoweka kwa utekelezaji wa mradi maalum. Katika akaunti ya aina hii, mmiliki anawajibika kufanya malipo ya mara kwa mara na/au kwamba fedha hazitatolewa kwa kipindi fulani kilichobainishwa. Kiwango cha malipo aghalabu huwekwa mapema. Mifano ya akaunti za akiba za kimkataba ni kama vile mpango wa kuweka akiba ya makazi unaolenga kufadhili uwekezaji katika ujenzi wa nyumba.

Akaunti ya amana ya wakati (uliobainishwa) hutumiwa ikiwa unataka kukuza pesa zako kwa ajili ya malengo ya muda mrefu zaidi (unaweka kiasi kikubwa cha pesa ambacho unaahidi kwamba hutatoa kwa kipindi fulani cha wakati).

Kila aina ya mpango una manufaa na hasara zake (kwa mfano, viwango tofauti vya riba au uwezekano wa kufanya miamala mtandaoni).

Katika kurasa zinazofuata utapata brosha tatu, moja kwa kila mojawapo ya mipango hii. Kufikia mwishoni mwa somo hili, kwenye Sehemu ya Majibu kwa mazoezi utapata jedwali linganishi ambalo linatoa muhtasari wa taarifa katika kila brosha.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO C.2.1

Brosha ya Akaunti ya Akiba ya Kawaida

Ni njia rahisi, sahili na faafu ya kuweka na kutoa pesa zako wakati wowote unapozihitaji. Hii ndio akaunti ya kwanza kabisa ya benki ambayo unaweza kufungua na kutumia kutoka kwa Programu ya simu. Manufaa ya akaunti ya kidijitali yameunganishwa na uzoefu na ujuzi wa benki yetu.

SIFA

- Unaweza kuweka pesa wakati wowote, mara nyingi utakavyo. Unaweza kufanya hivi kupitia kwa pochi ya kidijitali, kupitia kwa mtandao wa mawakala na kupitia kwa matawi na Mashine za ATM za Benki ya ABCD.
- Akiba yako inakua kwa kiwango chetu cha juu cha riba ya asilimia 3% kwa mwaka.
- KUTOA PESA BILA MALIPO. Furahia kutoa pesa BILA MALIPO ikiwa utatumia mashine zetu za ATM. Pia unaweza kutoa pesa bila malipo mara moja katika mashine nyingine za ATM .
- Taarifa ya akaunti ya kielektroniki BILA MALIPO. Kwa uwajibikaji wako mwenyewe, utapokea taarifa za akaunti bila malipo kila robo ya mwaka na uko huru kuongeza muda wa kutumwa kulingana na upendeleo wako.
- Hakuna malipo ya kufungua na kufunga akaunti yako. Fungua akaunti yako ya akiba kuanzia kiasi cha chini cha Shilingi 1000.
- Pata Kadi ya malipo bila kulipia ili uweze kuweka au kutoa pesa kutoka kwa mashine za ATM. Pokea kadi yako katika anwani yako ya posta.

USTAHIKI NA HATI

- Uraia: Raia wa Kenya/ Mkazi
- Mahitaji ya umri: Miaka 18 na zaidi
- Kitambulisho / nakala ya kitambulisho cha kitaifa, au Pasipoti halali.
- Picha / *Selfie* / Picha ndogo

KISAIDIZI CHA MAFUNZO C.2.2

Akaunti ya Akiba ya Malengo/ ya Kimkataba

NJIA KUU YA KUKUWEZESHA KUWEKA AKIBA

KWA AJILI YA MALENGO YAKO MAKUBWA

Akaunti hii inakusaidia kuweza kukaribia malengo yako ya kuweka akiba. Inakuruhusu kuweka pesa kwa kasi yako, kukiwa na chaguo la kutimiza wajibu wako wa kila mwezi mapema. Utapata riba kadri unavyoweka akiba. Licha ya iwapo una ndoto ya kujipatia au kuwapa watoto wako elimu bora zaidi, kununua gari, kwenda likizo au kuweka akiba pole pole ili kununua kipande cha ardhi, Akaunti yetu ya Malengo itakusaidia kugeuza ndoto zako kuwa malengo ya kweli.

SIFA

- Unaweza kuchagua vipindi unavyolenga kuanzia mwezi 1 hadi 12.
- Kiasi cha chini cha amana ya Shilingi 500 ili kufungua akaunti hii.
- Unaruhusiwa kutoa pesa kwenye Akaunti ya akiba ya Malengo alimradi utatoa pesa zote ulizoweka akiba. Jumla ya riba kwa pesa ulizoweka akiba inahesabiwa siku ya kutoa pesa.
- Viwango vya riba hadi asilimia 4% kwa mwaka.
- Hakuna malipo yanayotozwa kufungua, kufanya miamala na kufunga akaunti yako.
- Baada ya wakati fulani, unaweza kupata mikopo moja kwa moja ili kufadhili miradi yako.

MAHITAJI

- Kuwa mteja wetu
- Kitambulisho / nakala ya kitambulisho cha kitaifa, au Pasipoti halali.
- Uthibitisho wa makazi na picha

KISAIDIZI CHA MAFUNZO C.2.3

Brosha ya Akaunti ya Amana ya Muda Maalum (Uliobainishwa).

ZIDISHA KABISA UWEZO WA UKUAJI WA PESA ZAKO, BILA HATARI

Linda maisha yako ya baadaye na akaunti ya amana ya muda maalum inayokupa uwezo mkubwa wa ukuaji wa juu wa pesa zako kukiwa na mazao yenye uhakika. Pesa unazowekeza katika akaunti hii zinafungiwa na ni bora kwa uwekezaji wa siku zijazo na gharama kubwa ambazo unapangia. Ni akaunti bora kabisa ili usishawishike kutumia akiba yako huku ukipata riba nzuri kwa mtaji wako

SIFA KUU

- Kipindi cha kufungiwa kinajumuisha miezi 3, miezi 6, miezi 9 au miezi 12 na kiwango cha chini ni Shilingi 500.
- Hakuna malipo yanayotozwa kufungua, kufanya miamala na kufunga akaunti.
- Amana za wakati wowote: unaweza kuongeza pesa katika akaunti yako wakati wowote unaotaka.
- Imarisha historia yako ya kuweka akiba nasi na utapata mikopo kwa miradi yako.
- Ikiwa utatoa pesa zako kabla ya kipindi kilichobainishwa, basi hutapata riba kutokana na pesa zako.

MAHITAJI

- Kuwa mteja wetu
- Kitambulisho halali (Kitambulisho cha taifa au hati nyingine halali ya utambulisho)
- Uthibitisho wa makazi na picha

	Miezi 3	Miezi 6	Miezi 9	Miezi 12
Shilingi 100,000 - 1,999,99	1.00%	1.75%	3.25%	4.50%
Shilingi 2,000,00 - 1,999,99	1.10%	2.00%	3.50%	4.75%
Shilingi 10,000,00 - 19,999,99	1.20%	2.25%	3.75%	5.00%

Kwa kuwa sasa unajua mengi zaidi kuhusu mipango tofauti ya kuweka akiba, wasaidie wahusika wetu kuamua ni akaunti gani ya akiba wanapaswa kufungua ili kuwasaidia kutimiza malengo yao

KISAIDIZI CHA MAFUNZO C.2.4

Kadi za kulinganisha malengo na mpango wa akiba

KADI ZA HALI

KULINGANISHA MALENGO NA MPANGO WA AKIBA

HALI YA 1

Gloria angependa kuwa na saluni yake katika miaka michache ijayo. Hataki kushawishika kutumia pesa hizi kwa malengo mengine na anazingatia akaunti rasmi ya kuweka akiba ambayo inaweza kumsaidia kufikia lengo hili. Tayari ameweka akiba ya kiasi kikubwa na ikiwezekana, angependa kufungua akaunti ambapo anaweza kupata riba nyingi kadri awezavyo, hata kama hataweza kuzitoa kwa muda mrefu.

›› **Je, anaweza kuchagua aina gani ya akaunti**

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA

HALI ZA KULINGANISHA MALENGO NA MPANGO WA AKIBA

HALI YA 2

Mojawapo ya malengo ya Otieno ni kununua nyenzo za kujengea chumba cha ziada katika nyumba yake. Ili kufikia lengo hili, anataka kufungua akaunti ambayo itamruhusu kuweka na kutoa pesa ikiwa atapata nyenzo anazihitaji kwa bei nzuri:

›› **Je, anaweza kuchagua aina gani ya akaunti ya kuweka akiba?**

ELIMU YA KIFEDHA



KADI ZA HALI
KULINGANISHA MALENGO NA MPANGO WA AKIBA

HALI YA 3

Opiyo na Mutua walihudhuria mafunzo ya elimu ya kifedha mwezi uliopita. Walijifunza kuhusu aina tofauti za akaunti za akiba zilizopo. Opiyo amekuwa na nia ya kununua gari kwa muda sasa na anafikiria kuhusu aina ya akaunti ambayo anapaswa kufungua. Angependa kutenga kiasi fulani cha pesa kila mwezi kwa muda wa miaka miwili. Hataki kushawishika kutumia pesa hizi kwa malengo mengine.

Je, anaweza kuchagua aina gani ya akaunti ya kuweka akiba?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA HALI
KULINGANISHA MALENGO NA MPANGO WA AKIBA

HALI YA 4

Wangari anahudhuria masomo ya elimu ya kifedha. Baada ya hapo, Wangari anahisi kwamba akiba yake sio salama ikiwa nyumbani katika soksi kuu kuu kama pesa taslimu. Anajiuliza iwapo itakuwa vyema kuweka pesa zake katika benki. Hataki kushawishika kutumia pesa hizi. Pia anataka kuweka akiba ya kutosha ikiwapo kutakuwa na dharura:

Je, anaweza kuchagua aina gani ya akaunti ya kuweka akiba?

ELIMU YA KIFEDHA

VIDOKEZO

Kila aina ya mpango iko na manufaa na hasara (kwa mfano, viwango tofauti vya riba). Ili kuchagua mpango wa akiba, unastahili kujua sifa za mipango tofauti. Unapaswa pia kujielewa vizuri kwa kuuliza maswali yafuatayo:

- Hali yako ya kibinafsi: una mapato kiasi gani? Matumizi yako (ikiwemo malipo ya mkopo)? Je, umeweka akiba kiasi gani? Je, unatenga kiasi gani wakati hali ni nzuri? Je, unaweza kutenga kiasi gani kwa kusimamia pesa zako vyema zaidi? Je, ikiwa wewe ni mhamiaji au raia anayeishi ughaibuni unaweza kufungua akaunti ya akiba katika taasisi ya kifedha?

- Malengo yako: unaweka akiba kwa azma gani? Kwa ajili ya dharura? Elimu? Ili kuwekeza katika biashara yako au kuanzisha biashara mpya? Ili kurejea nyumbani? Kwa ajili ya malazi? Kwa ajili ya kustaafu?

- Upeo wako: Je, unataka kuweka akiba / kutogusa pesa zako kwa muda gani?

- Mwenendo wako: Je, unataka kukubali hatari au la? Usikubali kuingia katika uwekezaji wenye hatari sana ikiwa hujui vyema soko la kifedha!

Tahadhari dhidi ya matangazo ya biashara ambayo si ya kweli! Kumbuka kwamba mpango wa kuweka akiba unaweza kukuhakikishia faida ya juu bila hatari, hasa katika muda mfupi.

Ni maswali gani unafaa kuuliza taasisi ya kifedha kabla ya kuchagua mpango wako wa kuweka akiba?

- *Je, naweza kutoa pesa nikitaka?*
- *Kuna kiasi gani cha riba?*
- *Je, nahitaji kulipia riba ushuru? Ikiwa ndiyo, kiasi gani?*
- *Je, ninaweza kufikia akaunti yangu mtandaoni?*
- *Je, naweza kuchukua mikopo dhidi ya akiba yangu?*
- *Je, ratiba ya kuweka akiba inaweza kubadilika? (Yaani, je, lazima niweke amana ya kiasi fulani tarehe maalum?*
- *Je kuna kiwango cha chini cha amana unapofungua akaunti ya akiba au kiwango cha chini ambacho unastahili kuwa nacho katika akaunti yako?*
- *Je, nitatozwa ada kwa kutoa pesa inayotarajiwa? Ikiwa ndiyo, kiasi gani?*
- *Je, watu kwa kawaida hutumia vipi aina hii ya akaunti?*
- *Kama raia kutoka nchi nyingine, je naweza kufungua akaunti hapa? Je, ni stakabadhi gani zitahitajika?*

UJUMBE MUHIMU

- Kwa kila lengo la kuwekewa akiba kuna mpango faafu wa kuweka akiba.

MUHIMU: Kuingia katika taasisi ya kifedha au kupiga simu kuuliza maswali haya kunaweza kukufanya ukawa na wasiwasi. Kumbuka unaweza kumuuliza rafiki au mwenzako kazini kuandamana nawe hadi uweze kujiamini kwenda peke yako. Kumbuka kwamba unaweza kuondoa tashwishi nyingi kwa kuangalia tovuti zao.

VIAMBATISHO NA NYAKARA MUHIMU

SIFA ZA KUZINGATIA WAKATI WA KUCHAGUA MBINU YA KUWEKA AKIBA

Wepesi wa kufikia, utoaji pesa kwa urahisi

Hii inarejelea wepesi au ugumu wa mtu kutoa akiba yake. Kwa mfano, mwenye akaunti anaruhusiwa kutoa pesa mara ngapi kutoka kwenye akaunti hiyo kila mwezi, au ikiwa benki au taasisi ya kifedha iko na mashine za ATM au matawi katika sehemu zote za nchi hiyo (hivyo kumrahisishia mwenye akaunti ufikiaji wa akaunti yake).

Ufaafu na wepesi wa kutumia

Ufaafu na wepesi wa kutumia: Wateja wanapenda ufaafu na wanataka kuweza kutoa pesa haraka iwezekanavyo. Baadhi ya watu, kwa mfano, wanataka benki yao kuwa wazi kila wakati ambao wao wenyewe hawako kazini.

Mahitaji ya kufungua akaunti ya akiba

Watu wengi wanafikiri unahitaji kuwa tajiri ili ufungue akaunti ya benki. Hii si kweli. Baadhi ya benki zinahitaji amana ndogo sana (au hata huenda zisihitaji kamwe) ikiwa unataka kufungua akaunti ya akiba. Hata hivyo, mahitaji huenda yakajumuisha kitambulisho cha kitaifa, ithibati ya makazi na/au huduma ambazo mtu huyo amelipia ambazo huenda watu wengi wasiweze kutimiza. Kufungua akaunti ya bengi mtandaoni kumerahisisha mchakato huu sana.

Usalama

Watu wanapochagua kuweka pesa zao nyumbani, kuna hatari ya kuibiwa au kupotea. Baadhi ya taasisi za kifedha zinazothibitiwa na serikali hutoa hakikisho kwa watu wanaoweka akiba ndogo. Yaani, ikiwa taasisi hizi zitafilisika, hutapoteza akiba yako.

Kiwango cha riba na manufaa ya ushuru

Unapoweka akiba katika taasisi rasmi (au yenye urasmi kwa kiasi fulani), unazawadiwa kwa kuweka pesa zako kwenye taasisi husika. Tuzo, au riba, kwa jumla ni asilimia ya pesa ambazo umeweka. Aidha, huenda kukawa na nafuu za ushuru kwa kuweka akiba katika taasisi rasmi.

Gharama ya akiba (ada)

Taasisi rasmi huenda zikakutoza ada kwa kutuma, kutoa pesa kupitia mashine za ATM, n.k. Ikiwa unahitaji kufikia pesa kwa haraka, huenda ikawa bora kuwa na mpango wa kuweka akiba ambao unakuruhusu kufikia pesa zako bila kucheleweshwa sana.

Uwezo wa kupata pesa

Je, unaweza kutoa akiba yako kutoka kwa akaunti yako? Vipi na masharti ni gani? Ikiwa unahitaji pesa haraka, mbinu ya kuweka akiba ambayo umechagua inakuruhusu kutoa pesa zako zote ndani ya muda mfupi? Ikiwa umeweka akiba katika mali (kwa mfano jengo, shamba, au mifugo), huenda ukahitajika kusubiri siku, au miezi kabla ya kuuza mali na kupata pesa taslimu.

Ufikiaji mtandaoni

Ni kwa kiwango gani unaweza kutumia huduma hizi kwa kutumia vifaa vya kielektroniki kama vile tarakalishi, tarakilishi kibao, au simu. Kwa baadhi ya watu, wazo la kushughulikia akiba yao mtandaoni kikamilifu ni muhimu sana ili wasitegemee saa za kufunguliwa au kujaza karatasi ili kufanya miamala.

Azma na lengo la mkakati wako wa kuweka akiba

Kulingana na sababu ya kuweka akiba, baadhi ya mbinu zitakufaa vyema zaidi kuliko zingine (kwa mfano, kuweka akiba ili kununua nyumba, ambapo kiasi kikubwa cha pesa kinahusika, mbinu rasmi itafaa zaidi kuliko mpango wa mtandaoni au kuweka pesa zako chini ya godoro).

Huduma kwa wateja

Watu wengi hutegemeza uamuzi wao kwenye huduma kwa wateja, ambayo ndiyo sababu wanafurahi wakati taasisi inatoa huduma ambazo zinawaruhusu kuwasiliana na ajenti wa huduma kwa wateja ili kushughulikia shauku au matatizo. Baadhi ya taasisi hutoa huduma kwa wateja kupitia kwa barua pepe au arafa, taasisi nyingine hutoa mawasiliano ya simu au hata ya ana kwa ana katika matawi yake.

MAJIBU KWA MAZOEZI:

Manufaa na hasara za mbinu tofauti za kuweka akiba (C1)

Mbinu ya	Manufaa	Hasara
Rasmi •Benki	• Chaguo salama zaidi. •Faragha (hakuna mtu isipokuwa mwenye akaunti ya mpango wa kuweka akiba ambaye anajua ni kiasi gani kipo kwenye akaunti hiyo).	•Hazipatikani kwa watu wenye mapato ya chini, wasiojua kusoma na kuandika, watu waliohamishwa kwa nguvu. •Huenda ukahitaji Kitambulisho au ithibati ya makazi ambayo si rahisi kupata kwa Watu Waliohamishwa kwa Nguvu (FDPs).
•Taasisi ndogo za kifedha zilizosajiliwa. • Posta	•Ushawishi mdogo wa kutoa pesa (ni rahisi kukataa maombi). Unaweza kupokea riba.	• Wafanyakazi wa benki mara nyingi ni wafanyakazi wa mauzo wanaolenga kuuza huduma, kwa hivyo wanaweza Kujali maslahi ya benki kwanza badala ya maslahi ya wateja.
• Chama cha Ushirika cha akiba na mkopo kilichosajiliwa	. Unaweza kufikia mipango mingine ya kifedha (akaunti ya matumizi, akaunti ya akiba ya kustaafu, mikopo, n.k.)	. Viwango vya malipo hutofautiana kutoka mpango hadi mwingine. Vinaweza kuwa chini sana.
• Kampuni za bima (kwa akiba ya kiwango cha chini cha amana kwa muda mrefu kama vile bima ya maisha	. Njia bora zaidi ya kusimamia pesa zako (taarifa ya akaunti ya akiba).	. Baadhi ya mipango huenda ikahitaji amana ya chini zaidi ili kufungua akaunti, jambo ambalo linaweza kuwa kizuizi.
• Pochi za kidijitali	. Hurahisisha ulipaji wa bili.	. Huenda ukahitajika kulipa ada za akaunti
• Teknolojia za kifedha	. Wakati benki inatoa huduma kupitia kwa mtandao, huduma za simu au akaunti ya akiba mtandaoni, unaweza kuangalia salio lako na kusimamia akiba yako saa 24 kwa siku.	. Kupoteza muda kupanga foleni . Mipango tofauti na ada ni changamano; hofu ya kufanya makosa
• Programu za simu		
	. Benki nyingi zinaendesha shughuli zake kupitia kwa Mawakala wa Benki ambao hufanya huduma zao kufikiwa zaidi.	. Saa za ufunguzi zilizozuiliwa (zimefungwa jioni na wikendi)
	. Watoaji wengi wa kidijitali pia wanaruhusu kukagua salio na kusimamia akiba yako saa 24 kwa siku.	. Athari za udhibiti wa kiuchumi au kisiasa: migogoro ya kifedha, sarafu kupoteza thamani . Kuzuia utoaji wa pesa nje ya nchi (udhibiti wa Ubadilishaji). . Mawakala wa benki huenda wasiwe na fedha Za kutosha kukuhudumia

Mbinu ya kuweka akiba	Manufaa	Hasara
Rasmi kwa kiasi fulani •Vikundi vya kuweka akiba •Vikundi vya kujisaidia •Benki za kijiji •Mashirika ya Kijiji ya Akiba na Mikopo (VSLAs) •Taasisi ndogo za kifedhaa ambazo hazijasajiliwa. •Vyama vya ushirika vya akiba na mikopo ambavyo havijasajiliwa •Taasisi za mipoko ambazo hazijasajiliwa.	•Wepesi wa ufikiaji . Kwa kuwa unaweka akiba mara kwa mara inamaanisha unaweza kupata mkopo. •Unaweza kupata riba kwa mikopo iliyotolewa kwa akiba. •Kanuni za kikundi cha kuweka akiba kuhusu matumizi na kiasi cha kuweka huhamasisha uwekaji akiba. •Nidhamu •Huleta mshikamano na kuimarisha mahusiano ya kijamii miongoni mwa wanachama.	•Hakikisho ndogo. • Huna uhakika wa kupata riba kutokana na akiba yako. • Mikopo finyu au ukosefu wa mikopo. • Kuweza kuweka akiba au kutoa pesa kunategemea idhini ya wanachama wengine. • Hatari kwamba wanachama watakosa kuzingatia kanuni (k.m. Mtu anaweza kutoroka baada ya kupokea pesa kutoka kwenye kikundi). • Kulingana na kiwango cha urasmi, huenda isiwezekane kuhusisha polisi ikiwa kuna tatizo. • Hatari ya mwanachama wa kikundi cha kuweka akiba kufa. • Unahitaji kuwa sehemu ya mtandao ili kujiunga na kikundi cha kuweka akiba. • Vikundi vya kuweka akiba vina hatari kubwa zaidi ya kuanguka (hakuna usimamizi wa mamlaka)
Isiyo rasmi Nyumbani (pesa taslimu, katika sefu au kijisanduku cha pesa) Katika vitu (dhahabu, vito, mifugo, ardhi, majengo n.k.). Kumwaminia rafiki, jamaa au mwanabiashara pesa zako.	•Wepesi wa kufikia. •Thamani ya mali uliyonunua huenda ikaongezeka •Lazima uuze mali yako ili upate pesa zako (kwa kutegemea sheria za soko). •Rafiki, jamaa au mwanabiashara anapatikana kila wakati. •Kuna manufaa mengine ya kuweka akiba katika mali: uzalishaji au uuzaji wa maziwa (ikiwa ni ng'ombe), vito vinaweza kuvaliwa katika hafla muhimu. •Ikiwa utaweka akiba katika vitu (mifugo, majengo) huenda ukaweza kupata pesa (kuuza nyama/ maziwa, kodi...)	. Si salama: thamani huenda ikapungua kadri wakati unavyopita, hatari ya wizi, ugonjwa au kifo) ikiwa ni mifugo). . Huenda kukawa na ushawishi mkubwa wa kuzitumia (ikiwa utaweka pesa nyumbani) •Ni vigumu kugeuza kuwa pesa taslimu katika hali ya dharura (kuuza mali huchukua muda) • Gharama zinazohusiana na kuweka akiba kwa njia hii: chakula na gharama za daktari wa mifugo, matengenezo ya majengo.

MUHTASARI

MAJIBU KWA MAZOEZI: *Jedwali linganishi la mipango ya kuweka akiba kwa kutumia brosha za kubuni C2.*

Jedwali linganishi la mipango ya kuweka akiba kwa kutumia brosha za kubuni

	Akaunti ya akiba ya kawaida	Akaunti ya Kimkataba/Akiba ya Malengo	Akaunti ya Amana ya Muda Maalum
Je, inawezekana kufungua ikiwa wewe ni mhamiaji?	Inaonekana inawezeka na	Inaonekana inawezeka na	Inaonekana inawezeka na
Je, kuna amana ya chini unapofungua akaunti hiyo?	Ndiyo. Shilingi 2,000	Ndiyo. Shilingi 500	Ndiyo. Shilingi 500
Je, unaweza kutoa pesa wakati wowote? Je, iko na gharama zozote au ada za adhabu?	Ndiyo, unatoa pesa bila malipo ikiwa utatumia mashine ya ATM yao. Pia unaweza kutoa pesa bila malipo mara moja katika mashine nyingine za ATM.	Ndiyo, lakini utapoteza riba	Ndiyo, lakini utapoteza riba
Je, kuna kiasi gani cha riba?	Asilimia 3%	hadi 4%	kulingana na muda. Asilimia 1% hadi 5%
Je, unaweza kukopa pesa ikiwa utafungua akaunti ya akiba?	La	Ndiyo, baada ya muda fulani (haijabainishwa ni lini)	Ndiyo, lakini unaweza kupoteza riba
Je, ratiba ya akiba inaweza kubadilishwa au lazima uweke amana ya kiasi fulani tarehe maalum?	Inaweza kubadilishwa	Inaweza kubadilishwa	Inaweza kubadilishwa
Je, ninaweza kuweka amana au kutoa akiba yangu katika mashine ya ATM?	Ndiyo	Hakuna taarifa	Hakuna taarifa

MAJIBU KWA: *Kadi za kulinganisha malengo na mpango wa akiba(KISAIDIZI CHA MAFUNZO ASM C.2.4)*

MAJIBU HALI 1

Gloria anapaswa kujaribu kufungua akaunti ya amana ya muda ili asishawishike kutumia pesa hizo ambazo ameweza kutenga na atapata riba ya juu zaidi kwa pesa zake.

MAJIBU HALI 2

Otieno anapaswa kujaribu kufungua akaunti ya akiba ya kawaida. Katika akaunti ya aina hii, ataweza kutenga pesa fulani kila mwezi ambazo anaweza kutumia kwa lengo lake.

MAJIBU HALI 3

Akaunti ya akiba ya kimkataba itamruhusu Opiyo kuweka amana maalum kila mwezi na kuweka akiba kwa kipindi maalum. Baadhi ya taasisi zinatoa akaunti ya akiba ya kimkataba kwa malengo mahususi, kama vile kununua nyenzo za kujenga nyumba au kununua gari.

MAJIBU HALI 4

Wangari anapaswa kujaribu kufungua akaunti ya kawaida ya benki. Kwenye akaunti hii ya benki, ataweza kutenga pesa fulani kila mwezi ambazo anaweza kutumia kwa dharura, au ambazo baadaye anaweza kuziweka na kwenda nazo kwa safari yake kwenda Qatar.

D

KUTUMIA MIPANGO YA MIKOPO KWA BUSARA

D1. Je, unafikiri ni njia gani bora zaidi ya kufadhili mradi?

- ☐ **a.** Kukopa pesa
- ☐ **b.** Kutumia akiba yako
- ☐ **c.** Kukopa pesa na kutumia akiba yako
- ☐ **d.** Kuchanganua mahitaji yako na rasilimali na uchague chaguo lililo bora zaidi

D2. Ni nini cha muhimu zaidi unapochagua mpango?

- ☐ **a.** Kiasi cha riba
- ☐ **b.** Masharti ya kurejesha pesa.
- ☐ **c.** Hakuna kigezo ambacho ni muhimu kuliko vingine, lazima tuvikague vyote na kuchagua mkopo na mkopeshaji ambaye analingana na mahitaji yetu na hali zetu kibinafsi.
- ☐ **d.** Umbali wa kijiografia kutoka kwa mkopeshaji.

D3. Je, ni masharti gani ambayo yanapaswa kuwepo katika masharti ya mkopo?

- ☐ **a.** Kiasi cha riba.
- ☐ **b.** Dhamana.
- ☐ **c.** Bajeti
- ☐ **d.** Ada za adhabu

Majibu: D1:d; D.2:c; D.3:a

1 CHAGUA MBINU YA KUFADHILI MIRADI YAKO

Baada ya kupitia mbinu tofauti za kuweka akiba katika somo lililotangulia, sasa tutalinganisha njia tofauti za kupata pesa ili kutimiza malengo yetu ya kifedha na kufadhili miradi yetu.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.1.1

Masimulizi kuhusu ufadhili

MASIMULIZI KUHUSU UFADHILI

GLORIA NA GITAU

Imekuwa muda sasa, na Gitau na Gloria wameweza kuishi ndani ya bajeti yao na kuweka akiba ya pesa nyingi kuliko walivyotarajia. Amepata duka linalouza simu mahiri kwa bei nzuri. Gitau anaamua kutumia akiba yake kununua simu.

ELIMU YA KIFEDHA

MASIMULIZI KUHUSU UFADHILI

OTIENO

Hivi karibuni, Friji ya Otieno ya nyumbani iliharibika na anahitaji kununua nyingine mpya. Baada ya kutafakari, anaamua kuomba pesa kutoka kwa taasisi ya kifedha ili kununulia friji yenye friza, ambayo wanaweza kutumia kwa mahitaji ya familia na ya duka la kuoka.

ELIMU YA KIFEDHA

MASIMULIZI KUHUSU UFADHILI

WANGARI

Simu ya Tiriha ni kuu kuu sana. Wakati mwingine, wakati dadake anampigia simu, simu inakatika bila sababu. Hawezi kupiga simu ya video kwa kutumia simu hiyo. Hana akiba ya kutosha kumwezesha kununua simu mpya. Anaamua kuuza simu hiyo kuu kuu na samani kutoka kwa Rahwa ambayo hatumii tena. Atatumia pesa hizo kununu simu bora zaidi.

E

LIMU YA KIFEDHA



MASIMULIZI KUHUSU UFADHILI

MUTUA

Mutua anazidi kukaribia kuweza kuhamia Kuwait. Kutokana na tajriba za marafiki wengine, anaamini ataweza kupata kazi kama dereva, lakini ili aweze kufaulu, anahitaji kupata leseni ya udereva. Wakati wa chaji, mamake anamwambia kwamba amesikia kuwa kuna shule mpya ya udereva ambayo imefunguliwa karibu na kwao, ambayo itawapa kipunguzo wale watakaojisajili kwa masomo ya udereva wiki ijayo. Kwa kuwa Mutua hana pesa sasa hivi, anakopa pesa kwa mkopeshaji asiye rasmi ili alipie usajili.

ELIMU YA KIFEDHA

Kwa jumla, kuna njia nne ambazo watu hutumia kupata pesa za kufadhili mradi:

1 Kuuza mali, kama Wangari.

2 Kutumia akiba ya kibinafsi, kama Gitau.

3 Kukopa pesa kutoka kwa wakopeshaji wasio rasmi, kama Mutua.

4 Kukopa pesa kutoka kwa taasisi ya kifedha kama vile benki, kama Otieno

Kufikia mwishoni mwa somo hili, katika Sehemu ya Majibu kwa mazoezi Utapata Kisaidizi cha Mafunzo D.1.3, kama jedwali linaloeleza manufaa na hasara ya kila mbinu ya ufadhili.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.1.2

Masimulizi ya biashara mbili

MWENDE

Wewe ni Mwende na unaendesha duka ndogo la kuoka pamoja na mume wako Otieno. Leo unaenda kumtembelea rafiki yako, Safia, ambaye anamiliki mkahawa mdogo.
Unamuuliza rafiki yako maswali mengi kuhusu jinsi anavyofadhili biashara yake. Rafiki yako pia anataka kujua vile unavyofanya.

Hivi ndivyo umeanzisha na kupanua biashara yako:

Wewe na Otieno mlianza kwa Shilingi 25,000 ambazo Otieno alikuwa ameweka akiba baada ya kufanya kazi miaka mingi huko Saudi Arabia. Wewe pia ulikuwa na Shilingi 8,000 kutokana na mauzo ya samani kuu kuu. Ingawa biashara yenu ni ndogo sana, uko na mpango wa kuipanua kidogo kidogo.

Unajaribu kutenga Shilingi 2,000 kila wiki katika akaunti ya akiba mahususi kwa biashara yako, ambayo umefungua hivi karibuni. Kwa njia hii, kila miezi 3 au 4 utakuwa umeweka akiba ya kutosha kuboresha biashara yako (vyombo bora vya jikoni ya kufanyia kazi, nyenzo bora zaidi za kufungia bidhaa) na kuipanua. Sasa unaweza kununua bidhaa unazotumia katika biashara yako kwa wingi na kuanza kutengeneza bidhaa unazouza. Umekuwa pia ukifikiria kusomea uokaji wa vitobosha ili kutoa bidhaa mpya.

Kadri utakavyopata faida zaidi, ndivyo utaweza kuweka akiba zaidi na ndivyo utaweza kufanya uwekezaji mkubwa zaidi katika biashara hii.

SAFIA

Wewe ni Safia na unaendesha biashara ya mkahawa mdogo. Rafiki yake Mwende anamiliki duka la kuoka. Leo atakutembelea. Ungependa kujua jinsi rafiki yako anafadhili na kupanua biashara yake. Mwende pia anataka kujua vile unavyofanya.

Hivi ndivyo umeanzisha na kupanua biashara yako:

Ulianza kwa Shilingi 5,000 ambazo ulikuwa umeweka akiba na mkopo wa Shilingi 30,000 kutoka benki.

Mkopo huu ulikuwezesha kukarabati mkahawa ambao umekodisha. Kutokana na ukarabati huu, umeweza kupokea wateja zaidi katika mkahawa wako wa kupendeza katika mtaa wenye utulivu. Ulilipia gharama zako zote za kila wiki kwa wakati, ikiwemo malipo ya mkopo. Lakini unaweza kuweka akiba ya Shilingi 800 pekee kila wiki.

Siku moja, nafasi ya duka ndogo ilipatikana kwenye barabara yenye watu wengi zaidi jijini. Nafasi hiyo ya duka ni ya kukodisha. Hii inaonekana kama fursa nzuri ya kibiashara: unafanya hesabu kwamba mapato yako yataongezeka maradufu ikiwa utakodi duka hilo. Kwa hivyo, unafanya uamuzi wa haraka, kabla mtu kwingine kulipia duka hiyo. Kwa hivyo unakopa Shilingi 12,000 kutoka kwa shemeji yako.

MASWALI

- Je, Mwende na Safia walipanua vipi biashara zao?
- Ni yupi kati ya wanabiashara hawa wawili ana uwezekano mkubwa wa kufaulu? Kwa nini?
- Ni yupi anachukua maamuzi ya hatari zaidi?
- Je, ni ushauri gani unaweza kuwapa Mwende na Safia?

MUHIMU: Kuwa na majukumu mengi ya kifedha kunaweza kusababisha msongo na kuathiri afya ya akili yako. Ikiwa utahisi kuzidiwa, usisite kuomba msaada.

MUHTASARI

ZAMU YAKO!

Kwa kuangalia malengo yangu na bajeti, nafikiri chaguo bora zaidi la kufadhili malengo yangu ni:

Malengo yangu	Chaguo bora zaidi la ufadhili

UJUMBE MUHIMU

- Kuna chaguo mbalimbali za kufadhili malengo yako.
- Kila chaguo liko na ubora na udhaifu wake. Ni muhimu kuelewa na kukagua kila chaguo kwa makini ili uchague chaguo ambalo linalingana vyema zaidi na mahitaji yako na hali yako ya kibinafsi.
- Aidha, unaweza kuunganisha chaguzi kadhaa za ufadhili (kukopa na akiba)
- Zungumza kuhusu chaguzi za ufadhili na familia yako, hasa jamaa katika familia yako ambao wanahusika katika malengo yako (mwenzi, wazazi, watoto, ndugu…).

2. CHAGUA MKOPO WAKO KWA BUSARA!

Kuna vyanzo mbalimbali vya mkopo. Baadhi, kama vile benki, na taasisi ndogo za kifedha au kampuni za kipekee za kutoa mikopo, ni sehemu ya uchumi rasmi na huweka masharti mahususi kwa mtu yeyote au taasisi inayotaka kuomba mkopo.

Baadhi hujaribu kurahisisha upataji wa mkopo, hata kwa watu masikini. Vyanzo vingine vitakuhitaji uwe sehemu ya kikundi, kama vile bima ya malipomwaka au kwamba tayari uwe na pesa ulizoweka akiba.

UJELEZI

Mkopo: Ni zoezi la kutoa pesa, mali au vitu vingine kwa mhusika mwingine ili baadaye ulipwe kiasi ulichotoa pamoja na riba au ada zingine za kifedha.

Muamana: Makubaliano ya kimkataba ambapo anayeomba anapokea kitu cha thamani sasa na anakubali kumlipa mwenyewe siku fulani wakati ujao, kwa jumla pamoja na riba.

Riba: Ni bei ya matumizi ya pesa za mkopeshaji kwa kipindi fulani.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.2.1

Istilahi na ujelezi unaohusiana na muamana/mikopo

Linganisha kila istilahi ya muamana na ujelezi wake. Usiwe na wasiwasi ikiwa huna uhakika. Mwishoni mwa somo hili katika sehemu ya Majibu kwa mazoezi utapata majibu sahihi.

Istilahi	Ujelezi
RIBA	Mtalamu anayeaminiwa na wateja wake kuwatafutia mikopo inayowafaa zaidi na/au ya nafuu zaidi (kwa jumla mikopo ya rehani) kutoka benki na taasisi zingine za kifedha.
DALALI WA MUAMANA:	Kiasi cha pesa ambacho mkopaji hulipa mkopeshaji, zaidi ya kulipa kiasi cha mkopo wenyewe, ili kuweza kutumia pesa za mkopeshaji.
ADA ZA ADHABU	Kiasi cha mkopo ambacho kinatolewa na mkopeshaji, bila kujumlisha riba
KIASI CHA	Mtu atakayelipa mkopo wako ikiwa utashindwa kufanya hivyo. Mtu huyu anaweza kuombwa kutia sahihi yake kwenye makubaliano na mkopeshaji. Dhamana pia inaweza kuwa katika mfumo wa mali.
MDHAMINI/ DHAMANA	Pesa ambapo mkopaji atahitajika kumlipa mkopeshaji ikiwa atashindwa kulipa mkopo wake (k.m. Kutwaliwa kwa mali, gari, akiba...)
KIPINDI CHA NYONGEZA	Kulipa sehemu ya mkopo au mkopo wote kabla ya muda wa makubaliano
KUTAFAKARI UPYA	Sehemu ya ufadhili kwa mradi wako ambayo unamiliki kabla ya kukopa pesa zaidi kutoka kwa taasisi ya kukopesha. Mchango huu utajumuisha zaidi pesa taslimu na akiba yako.
MALIPO YA MAPEMA	Muda unaoruhusiwa baina ya kupokea mkopo na malipo ya kwanza (nunua sasa, lipa baadaye)
REHANI	Kubatilisha makubaliano ya muamana bila ada ya adhabu. Muda wa "kujituliza" unakukinga dhidi ya kununua vitu kiholela
MCHANGO WA KIBINAFSI	Kuweka dhamana ya mali unayomiliki kama dhamana ili kupata mkopo kutoka kwa taasisi ya kifedha. Ikiwa malipo yatakosa kufanywa, mkopeshaji anaweza kuchukua/au kutwaa mali inayohusika na kuiuza ili kupata pesa ambazo alikuwa amekopesha pamoja na ada. Mmiliki hapotezi umiliki wa mali iliyowekwa rehani alimradi anatimiza mahitaji yake ya kufanya malipo.

MASWALI

- Kwa maoni yako, nini utachambua wakati unachagua mkopeshaji?

Sifa muhimu za kuzingatia wakati wa kuchagua mkopeshaji

- Kiasi cha riba (imebainishwa au inabadilika)
- Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (APR), gharama halisi ya kuchukua mkopo (ikiwemo ada za usimamizi, bima ya lazima)
- Kiasi cha pesa ambacho unaweza kukopa
- Wepesi wa kupata mkopo (k.m. Kiasi ambacho lazima uwe umeweka akiba kabla ya kupewa mkopo, kiasi cha dhamana...)
- Mahitaji (karatasi unahitajika kuwasilisha, uwezekano kwamba watanipa muamana)
- Utapata pesa haraka kiasi gani
- Ada za adhabu ikiwa nitachelewa kulipa
- Umbali kutoka nyumbani kwangu
- Aina za ukusanyaji wa deni ikiwa nitachelewa kulipa (kisheria, vitisho...)
- Kipindi cha nyongeza
- Wajibu wa kutumia mkopo kwa matumizi maalum (ujenzi, uwekezaji wenye mapato...)
- Uwezekano wa kuongeza muda wa malipo au kipindi cha nyongeza
- Uwezekano wa kufikia huduma nyingine za kifedha, akaunti ya matumizi, utumaji wa pesa, kadi ya malipo huduma za rununu au intaneti...)
- Mipango ikiwa kutatokea kifo, ugonjwa au mabadiliko katika hali ya anayeomba.

UJUMBE MUHIMU

- Ili kutumia mipango ya mikopo kwa ufanisi, unahitaji kuelewa vyema istilahi za muamana.
- Anayekopa anawajibikia kulipa mkopo kulingana na ratiba ya kulipa pesa.
- Kuchukua mkopo ni suala la dhati. Usilichukulie kimzaha.
- Kuna methali inayoeleza kwamba, tajiri ni mtu anayelipa madeni yake!
- Ili kuchagua mkopo na mkopeshaji kwa busara, kwanza unahitaji kujua mipango iliyopo na wakopeshaji ni nani, kwa kukusanya taarifa nyingi kadri uwezavyo. Ukiwa na taarifa hiyo, utaweza kuchagua mpango ambao unafaa zaidi kwa mahitaji yako.
- Mkopeshaji utakayechagua atategemea hali ya mradi wako, k.v. Lengo ambalo ungependa kufikia kwa kuchukua mkopo.

3. HESABU GHARAMA YA MKOPO WAKO

Uwezo wa kulipa

Tuchukulie kuwa baada ya kufikiria vyema, uliamua kuchukua mkopo kufadhili mradi wako. Hongera! Unajua kiasi ambacho unahitaji, na unahisi kuwa tayari kutembelea taasisi za kifedha ili kupata mpango unaokufaa. Kabla ya kuwatembelea, utahitaji kuchukua muda kuhesabu uwezo wako wa kulipa muamana.

Hebu tuangazie mikopo ya kibinafsi kwa mujibu wa sheria iliyopo katika nchi nyingi, mtu hawezi kulipa zaidi ya asilimia fulani ya mapato yake kwa mwezi. Kutegemea nchi, asilimia hii inatofautiana baina ya 30% na 40% ya mapato kwa mwezi. Tukipita asilimia hii, kuna hatari kubwa ya kuwa na madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa. Isitoshe, taasisi ya kifedha inayotoa muamana kwa mtu ambaye atahitajika kulipa zaidi ya asilimia hiyo ya mapato yake kwa mwezi inaweza kufunguliwa mashtaka.

Lakini tahadhari! Hii ndiyo asilimia ya juu zaidi inayoruhusiwa, sio asilimia iliyopendekezwa ambayo ni badala ya 30%.

Kama mfano, tutahesabu uwezo wa kibinafsi wa Otieno wa kulipa.

Uchunguzi Kifani N°1

UWEZO WA OTIENO WA KULIPA

Otieno anajipanga vizuri katika hesabu zake. Amejitengea mshahara thabiti kila mwezi kutoka kwa duka lake la kuoka wa Shilingi 10,000. Ingawa wao ni wamiliki, yeye na Mwende wanajilipa mshahara kwa kazi yao. Anapata pesa zako kando na faida za duka hilo la kuoka. Wakati mwingine duka lao huwa na biashara nzuri sana, na wanapata mapato ya ziada. Lakini akiwa na mfumo huu wa kiasi kilichobainishwa anaweza kupanga maisha yake ya kifedha vyema zaidi. Mapato yanayobadilika kutokana na faida hayazingatiwi kwa ajili ya hesabu hii.

Mapato kwa mwezi: Shilingi 10,000.00

Uwezo wa kufanya malipo kwa mwezi: Otieno anapanga kuchukua mkopo wa kibinafsi.
Asilimia 30% ya mapato kwa mwezi › Shilingi 3,000

Kulingana na hesabu hii, basi Otieno hawezi kuahidi kulipa zaidi ya Shilingi 3,000 kwa mwezi (kwa mikopo yote ambayo huenda akawa amechukua).

UWEZO WA KIBINAFSI

Sasa, ni zamu yako! Hesabu uwezo wako binafsi wa kulipa mkopo.

Mapato kwa mwezi: 100%

Uwezo wa kufanya malipo kwa mwezi: . . . . Asilimia 30% ya mapato

⚠ **MUHIMU: Kukopa pesa kwa kuzingatia uwezo wako wa kulipa kutakusaidia kutuliza akili yako.**

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.3.1

Kuhesabu gharama ya Mkopo wa mhusika

Otieno amehesabu kwamba atahitaji Shilingi 45,000 kununua friji yenye friza. Amefanya utafiti wa mipango ifuatayo inayolenga mahitaji yake mahususi. Anajaribu kuhesabu ni mpango gani wa nafuu zaidi kati ya yote aliyopata.

JINA LA MPANGO	BENKI YA NDANI	SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI	POCHI LA KIDIJITALI
Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (APR)	16%	20%	18%
Muda wa kulipa mkopo	36	24	12
Kiasi cha kulipa kila mwezi (ada kwa mwezi)	Shilingi 1,582.07	Shilingi 2,290.31	Shilingi 4,125.60
Kiasi cha jumla cha kulipa (Muda wa kulipa mkopo x ada kwa mwezi)	Shilingi 1,582.07 x 36 = Shilingi 56,954.52		
Gharama halisi ya mkopo (kiasharia cha jumla cha kulipa ukiondoa kiasi cha mkopo ambacho Otieno ameomba)	Shilingi 55,423.80 - Shilingi 45,000 = Shilingi 11,954.52		

Sasa ni zamu yako!

Je, gharama halisi ya mkopo unaotolewa na shirika lisilo la kiserikali ni ipi? (1)

Je, gharama halisi ya mkopo unaotolewa na POCHI LA KIDIJITALI ni ipi? (2)

Hivyo basi, ni mkopo gani wenye nafuu zaidi ambao Otieno anapewa? (3)

⚠ **Tahadhari! Mkopo nafuu zaidi sio lazima uwe ndio bora zaidi kwa mahitaji ya Otieno. Kwa mfano, mkopo wenye Kiwango cha chini cha Asilimia kwa Mwaka (APR) huenda ukahitaji uwe mteja wa taasisi hiyo kwa muda mrefu kabla ya kuweza kupata mkopo, au pengine uwezo wa kufanya malipo hautoshi.**

1. Kiasi cha jumla cha kulipa = Shilingi 2,290.31 x 24 = Shilingi 54,967.44 Gharama halisi ya mkopo = Shilingi 54,967.44 - Shilingi 45,000 KSh = Shilingi 9,967.44

2. Kiasi cha jumla cha kulipa = Shilingi 2,620.16 x 12 = Shilingi 49,507.20 Gharama halisi ya mkopo = Shilingi 49,507.20 Shilingi - 45,000 KSh = Shilingi 5,507.20

(3) Jibu sahihi ni POCHI LA KIDIJITALI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.3.2

Boresha za kubuni zinazotangaza mikopo

BENKI YA NDANI

MKOPO WA KIBINAFSI ULIO BORA ZAIDI
KWA MAHITAJI YAKO TOFAUTI

KIKOKOTOO CHA MKOPO

Kiasi cha pesa: Shilingi 45,000

Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (APR): 16%

Muda wa kulipa mkopo: Miezi 36

Malipo kwa mwezi: Shilingi 1,582.07

Kipindi cha nyongeza: La

Kiasi cha juu zaidi cha mkopo Shilingi 100,000.00

Muda wa kuidhinishwa: ndani ya siku 5 za kazi kwa wateja wa benki.

Masharti:

- Kitambulisho kimoja (1) kinachotolewa na serikali
- kwa mkopo huu wa kibinafsi, uwezo wa kulipa utachambuliwa.

SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI

MKOPO UNAOKUFAA

Kiasi cha pesa: Shilingi 45,000

Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (APR) 20%

Muda wa kulipa mkopo: Miezi 24

Malipo kwa mwezi: Shilingi 2,290.31

Kiasi cha juu zaidi cha mkopo: Shilingi 50,000.00

Muda wa Kuidhinishwa: Siku 30.

Masharti:

- Kitambulisho kimoja (1) kinachotolewa na serikali
- Kuhudhuria mafunzo ya elimu wa kifedha kwa miezi 3
- Kujiunga na shirika lisilo la kiserikali

POCHI LA KIDIJITALI

POCHI BORA ZAIDI LA KIDIJITALI SASA LINAKUPA

MKOPO WA HARAKA ZAIDI

HESABU MKOPO

Kiasi cha pesa:
Shilingi 45,000

Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (APR):
18%

Muda wa kulipa mkopo:
Miezi 12

Malipo kwa mwezi:
Shilingi 4,125.60

Kiasi cha juu zaidi cha mkopo
Shilingi 100,000.00

Muda wa Kuidhinishwa:
Ufikiaji wa haraka wa mkopo wako ulioidhinishwa ikiwa wewe tayari ni mteja wetu huduma kwa wateja saa 24 kwa wiki kupitia kwa mpango wa soga ya huduma kwa wateja.

Masharti:

- Inapatikana tu kwa wateja wa pochi letu la kidijitali.
- Watumiaji wawe wametumia pochi la kidijitali kwa angalau miezi 6

WWW.DIGITALWALLET.COM

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.3.3

Jedwali lenye muhtasari wa masuala yaliyomwathiri mhusika katika kuchagua mkopeshaji na mkopo (wazi)

VIPENGELE	BENKI YA NDANI	SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI	POCHI LA KIDIJITALI
Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (APR)			
Wepesi wa kufikia mkopo / masharti			
Kiasi cha pesa anazoweza kukopa			
Matukizi ya kufanya malipo			
Usaidizi na upatikanaji wa huduma zisizo za kifedha			

ELIMU YA KIFEDHA

Zamu yako!

Kwa kuangalia malengo yangu, bajeti yangu, na uwezo wangu wa kulipa, je, nahitaji muamana?

☐ **Ndiyo** ☐ **La**

Ikiwa ndiyo, kwa lengo gani? ....

Kiasi gani? ....

Sasa tafuta taarifa katika taasisi za kifedha karibu nawe na ujaze Jedwali la Otieno, lakini kwa lengo ambalo umeamua unahitaji muamana.

Tahadhari! Ili uweze kulinganisha mipango ya muamana, utahitaji kuuliza gharama ya jumla ya mkopo huo (yaani, kiasi ambacho utalipa juu ya kiasi ambacho umekopa). Hii inajumuisha kiwango cha riba kwa jumla ua pesa zilizokopwa, lakini pia gharama za usimamizi, bima, na huduma nyingine zinazotolewa. Kama Otieno, tahadhari dhidi ya viwango vya chini, ambavyo kwa muda mrefu huenda vikawa ghali sana!

VIPENGELE			
Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (APR)			
Muda wa kulipa mkopo			
Wepesi wa kufikia mkopo / masharti			
Kiasi cha pesa anazoweza kukopa			
Matukizi ya kufanya malipo			
Usaidizi na upatikanaji wa huduma zisizo za kifedha			

Mpango bora zaidi kwa mahitaji yangu ni: . ...

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.3.4

Hali ya kununua nyumba kwa kutumia ufadhili wa kawaida na ufadhili wa Kiislamu

UFADHILI WA KAWAIDA

Mwanamke mmoja kutoka jumuiya pokezi anataka kununua nyumba inayogharimu vizio 100 vya sarafu.

Anachukua mkopo kutoka benki na kununua nyumba hiyo. Anapata nyumba hiyo haraka. Anahitajika kulipa vizio 120 vya sarafu katika kipindi cha miaka 20. Gharama ya mkopo ni vizio 20 vya sarafu, ikihesabiwa ifuatavyo: **(120 – 100 = 20)**

UFADHILI WA KIISMLAMU

Mwanamke mmoja wa Kiislamu kutoka jumuiya pokezi anataka kununua nyumba inayogharimu vizio 100 vya sarafu.

Benki yake inanunua nyumba hiyo kwa vizio 100, na kujitwika hatari zinazohusika (k.m. Uwezekano kwamba nyumba hiyo inaweza kuchomeka). Nyumba hiyo sasa inamilikiwa na benki hiyo. Benki inamuuzia nyumba kwa vizio 120 vya sarafu na kuhamisha umiliki wa nyumba baada ya siku 90. Amekubali kulipa pesa za benki kwa muda wa miaka 20. Gharama ya mkopo ni vizio 20 vya sarafu. **(120-100 = 20)**

UJUMBE MUHIMU

- Ili kutumia mpango wa muamana vizuri, unapaswa kuelewa vyema masharti ya muamana husika.
- Ukopaji unaleta uwajibikaji wa kulipa na kulipa kwa wakati.
- Kukopa ni shughuli ya dhati. Usichukulie kimzaha!
- Ili kuchagua mpango wako wa muamana, unahitajika kufahamu mipango tofauti, na kukusanya taarifa kuhusu sifa za kila mpango. Kwa kutumia taarifa hii, utahitaji kuchagua mpango wa muamana ambao ni faafu zaidi kwa mahitaji yako.

4. TAHADHARI! USIJITWIKE MADENI MENGI KULIKO UNAVYOWEZA KULIPA!

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.4.1

Jedwali la madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa

SEHEMU YA 1	Malaika na familia yake wanafanya mazungumzo baada ya chamcha.
Malaika	Asante mama kwa chamcha, lakini nahitaji kutembelea taasisi ndogo ya kifedha. Leo asubuhi wataamua kuhusu mkopo niliokuwa nimeomba. Najua wameuidhinisha kwa sababu niliomba pesa kidogo kuliko mara hiyo nyingine.
Wangari	Lakini, Malaika, kwa nini unaomba pesa kutoka kwa Taasisi ndogo ya Kifedha tena? Je, umesahau kwamba wiki ijayo unapaswa kunilipa pesa nilizokukopesha?
Malaika	Sijasahau dadangu. Nitakulipa...baada ya kulipa pesa nilizokopa kutoka kwa bosi wangu kazini kama malipo ya mapema ya mshahara.
Ochieng	Unasema nini? Tena unaomba malipo ya mapema ya mshahara? Binti yangu, lazima ulipe madeni yako. Mumeo anafikiri nini kuhusu hali hii?
Malaika	Baba usijali. Anakubaliana nami. Hata yeye ndiye aliniomba kuchukua mkopo kupitia kwa pochi la kidijitali mwezi jana na kuahidi kunisaidia kuulipa.
Wangari	Kwa hivyo una deni la pochi la kidijitali, la taasisi ndogo ya kifedha, la bosi wako na langu? Ah Malaika, sijui utawezaje kutulipa sote.
Malaika	Usijali, nikipata tatizo, bado naweza kukopa kutoka kwa shirika lisilo la kiserikali au mkopesha asiye rasmi, nimewaomba hapo mbeleni na walinikopesha. Najua inaonekana kuwa hali mbaya, lakini sio mbaya vile. Kukopa ni rahisi na hakuna mkopeshaji anayejali iwapo nachukua mkopo ili kulipa mkopo mwingine. Samahani, inanibidi kuondoka, kwaheri!
SEHEMU YA 2	Malaika anafika kwenye Taasisi ndogo ya Kifedha kuzungumza na afisa wa mikopo ambaye atamfahamisha kuhusu uamuzi wa mkopo aliokuwa ameomba.
Malaika	Hujambo, nimekuja kutoa pesa kutokana na mkopo niliokuwa nimeomba.
Afisa	Samahani, lakini ombi lako lilikataliwa. Tuligundua kwamba umeomba mikopo kadhaa kutoka kwetu na hujawahi kulipa kwa wakati. Kwa hakika, bado una mkopo wetu ambao hujalipa na umechelewa kufanya malipo yako.
Malaika	Naam, najua, lakini ni miezi 3 tu ambayo sijalipa. Huwezi kuzingatia upya? Kwa hakika nahitaji mkopo huu.
Afisa	Samahani sana, lakini la, uamuzi umeshafanywa tayari. Lazima ulipe mkopo ulionao nasi haraka, la sivyo, ada za adhabu zitaongezeka na hutaweza kupata mkopo kwetu tena.

MASWALI

- Malaika anafanya nini?
- Je, kwa nini anakopa kutoka kwa wakopeshaji kadhaa?
- Je, Malaika anafikiri nini kuhusu wakopeshaji mbalimbali ambao anawakopa pesa?
- Je, unafikiri nini kitafanyika kwa Malaika?

UJELEZI

Kuwa na madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa ni wakati mtu anashindwa kutimiza wajibu wa kulipa madeni yake ya kibinafsi ikiwemo mikopo ya benki (huku akidumisha hali nzuri ya maisha kwake na kwa familia yake).

MUHIMU: Huenda ukahisi aibu kwa kuwa na madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa na hii inaweza kuathiri uhusiano wako na familia na marafiki. Usijitenge, badala yake jadili shida zako na watu unaowaamini.

VIDOKEZO VYA KUTOJIINGIZA KATIKA MADENI KULIKO UNAVYOWEZA KULIPA

- Kopa tu kiasi cha pesa ambacho unaweza kulipa. Kuwa mwangalifu hasa kwa mikopo ya kidijitali inayopatikana kwa wepesi na ambayo inaweza kukushawishi kukopa zaidi ya uwezo wako wa kulipa.
- Kuhesabu uwiano wako wa deni kwa mapato. Hesabu jumla ya mapato yako kwa mwezi na malipo kwa mwezi ambayo unahitajika kulipa kwa mikopo yako (wajibu wako wa madeni kwa mwezi). Linganisha takwimu hizi mbili na uhesabu uwiano. Kwa kawaida, ikiwa malipo yako yanafika silimia 30 ya mapato yako kwa mwezi, hupaswi kuchukua mikopo zaidi. Unaweza kutumia vifaa vingi vya kidijitali vinavyopatikana kwa ajili hii.
- Ikiwa huwezi kufanya malipo ya mkopo kwa wakati, wasiliana na mkopeshaji wako na ueleze sababu za changamoto hiyo.
- Sikiliza ushauri wa mkopeshaji wako, marafiki na familia kuhusu jinsi ya kulipa mikopo yako.
- Punguza baadhi ya gharama zako za kila siku ili uweze kulipa madeni yako.
- Kila wakati weka akiba kidogo kwa ajili ya dharura ili uweze kukabiliana na dharura bila kuathiri malipo yako ya mikopo.
- Chukua hatua! Nenda uzungumze na meneja wa akaunti yako katika taasisi ya kifedha. Usisubiri hadi ukawa umechelewa sana kuomba usaidizi.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.4.2

Kadi za Maigizo

KADI. ZA MAIGIZO

KADI

Nyinyi ni wanachama wa Shirika Lisilo la Kiserikali ambapo Malaika ameomba mkopo. Kuna uvumi mtaani kwamba Malaika ana deni la benki, la taasisi ndogo ya kifedha na la familia yake.

Mnawaza iwapo mtamkopesha pesa licha ya sifa yake. Andaa maelezo mafupi ambapo utajadili hali hiyo na kuamua kuhusu Malaika.

ELIMU YA KIFEDHA

KADI. ZA MAIGIZO

KADI

Wewe ni jamaa wa Malaika (dada, mama, baba) Una wasiwasi kuhusu Malaika. Umesikia kwamba Malaika amekopa pesa kutoka kwa watu wengine wa familia na wenzake kazini, na kwamba wote wamemkasirikia sana.

Andaa maelezo mafupi ambapo utajadili hali hiyo na kuamua utakachofanya kuhusu Malaika.

KADI ZA MAIGIZO

Wewe ni jamaa wa Malaika (dada, mama, baba) Una wasiwasi kuhusu Malaika. Umesikia kwamba Malaika amekopa pesa kutoka kwa watu wengine wa familia na wenzake kazini, na kwamba wote wamemkasirikia sana.

Andaa maelezo mafupi ambapo utajadili hali hiyo na kuamua utakachofanya kuhusu Malaika.

ZAMU YAKO!

Je, uko na madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa?

Je, wajibu wako wa madeni kwa mwezi umezidi asilimia 30 ya mapato yako Kwa mwezi?

Ndiyo ☐ La ☐

Je, unatumia sehemu kubwa ya mikopo yako kulipia gharama zako za maisha ya Kila Siku?

☐ Ndiyo ☐ La

Je, unaomba kuongezewa muda mara kwa mara kwa matumizi yako ya kila mara (kodi ya nyumba, bili ya umeme ...)?

☐ Ndiyo ☐ La

Je, huwa unachukua mikopo ya Kujirudia mara kwa mara (muamana Unaojirudia)?

☐ Ndiyo ☐ La

Ikiwa umejibu NDIYO kwa angalau moja katika ya maswali haya, kuwa makini! Huenda ukawa katika hatari ya kwa na madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa. Jirekebishe kwa kuandaa bajeti na kuzungumza na wakopeshaji wako ili ulipe madeni yako haraka iwezekanavyo na uepuke kuingia katika lindi la madeni.

Baadhi ya suluhu

Ikiwa tayari una madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa, zifuatazo ni suluhu ambazo zinaweza kutolewa na taasisi inayokukopesha:

- Kubadilisha ratiba ya deni: kupunguza kiasi kinacholipwa kila mwezi na kuongeza muda wa kulipa mkopo.
- Kukatiza malipo kwa muda fulani.
- Kuuza mali ili kulipa deni lako lililo ghali zaidi (yaani, madeni ambayo yanatoza riba ya juu zaidi).

Usisite kuulizia kuhusu huduma za upatanisho za taasisi ya muamana!

UJUMBE MUHIMU

- Kulipa ni uamuzi ambao utafanya wakati unaamua kukopa.
- Epuka kukopa ili ulipe mkopo!
- Pesa kutokana na muamana si zako!

VIAMBATISHO NA HATI MUHIMU

MASWALI YA KUMUULIZA MKOPESHAJI MTARAJIWA

- Je, mnatoa mikopo ya aina gani? Mnafadhili miradi ya aina gani kupitia kwa mikopo hii (ununuzi wa nyumba, kuanzisha biashara, kununua gari...)?
- Je, kuna kiasi gani cha riba?
- Mnatoza ada gani na ada za adhabu?
- Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (yaani gharama kamili ya mkopo, ikiwemo ada)?
- Je, ninaweza kutoa dhamana kwa mkopo uliotolewa? Ikiwa ndiyo, dhamana gani?
- Je, masharti ya dhamana ni tofauti ikiwa mimi ni mfanyakazi mhamiaji?
- Je, nahitajika kuchangia kiasi gani, ikiwa inahitajika?
- Je, malipo ya riba yanafanyika kwa matukizi gani?
- Je, kila malipo yanahitaji kufanywa vipi? (mwanzoni mwa mwezi...)
- Je, ni ada gani za adhabu zinazotozwa ikiwa nitachelewa kufanya malipo?
- Je, malipo yanahitaji kufanywa wapi?
- Je, inachukua muda gani kutoa mkopo na kupokea pesa?
- Je, nitahitaji kuja hapa mara ngapi ili kuhitimisha ombi la mkopo?
- Je, nahitaji kuwasilisha hati gani kwa mkopeshaji ili nipewe mkopo?
- Je, nitahitajika kulipa riba iliyosalia ikiwa nitalipa mkopo wote kabla ya muda kuisha?
- Je, kuna mipango ya bima ya lazima au ya hiari ikiwa nitachukua mkopo huu? Ikiwa ndiyo, bima itagharimu kiasi gani?
- Je, kuna mipango ambayo pia inawafaa wafanyakazi wahamiaji?
- Je, ofisi iko umbali gani na mahali ninapohitajika kufanya malipo kutoka mahali ninapoishi / kwa biashara yangu?
- Je, nahitajika kuhudhuria mikutano ili nipate muamana?
- Mikutano hii inadumu kwa muda gani?
- Je, huwa mnaangalia iwapo niko na mikopo mingine na taasisi zingine?

MAJIBU KWA MAZOEZI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.1.3: Manufaa na hasara za njia tofauti za kupata pesa

MANUFAA NA HASARA ZA NJIA TOFAUTI ZA KUPATA PESA

	Manufaa	Hasara
Kuuza mali	• Unaepuka deni na gharama zinazohusika • Unatumia tu rasilimali zako mwenyewe • Uhuru zaidi wa kufanya maamuzi kuhusu uwekezaji wako.	• Hatari ya mali kupoteza thamani • Ikiwa ni mali inayoleta mapato, huenda familia ikapata gharama za ziada au ikahitajika kutumia pesa zaidi kila siku Thamani ya kuuza huenda ikawa chini kuliko thamani ya kununua.
Akiba	• Ufikiaji wa haraka • Hakuna riba ya kulipwa • Uhuru zaidi wa kufanya maamuzi kuhusu uwekezaji wako. • Hatari ndogo katika uwekezaji ikiwa umejifadhili, kwa kuwa unaweza kufikia pesa chache kwa wakati mmoja. • Hakuna haja ya kufanya malipo ya mkopo baadaye • Epuka masharti na/ au mahitaji	• Unapunguza akiba yako • Pesa lazima ziwekwe akiba kwa muda mrefu, kwa hivyo huenda usiweze kutimiza mahitaji yako yote. • Hatari: hupaswi kutumia fedha zako za dharura, hata kama unatumia rasilimali zako mwenyewe • Huenda ukakosa rasilimali za kifedha kukiwa na dharura. • Haiwezekani kutumia fursa fulani za biashara
Kukopa kutoka kwa mkopeshaji asiye rasmi (familia, mwenye duka...)	• Haraka • Muamala wa ndani • Hakuna utaratibu wa utekelezaji • Ikiwa ni kutoka kwa familia, huenda kusiwe na riba na unyumbufu wa kufanya malipo	• Aghalabu huwa ghali sana (isipokuwa familia au marafiki) • Hatari: ikiwa utakosa kulipa, mkopeshaji huenda akatumia mbinu “katili”, ikiwemo vitisho • Hakuna ulinzi wa kisheria iwapo kuna uonevu kutoka kwa mkopeshaji • Ni rahisi kujiingiza katika deni • Huenda usipate pesa zote unazohitaji • Ikiwa ni mtu wa familia, unaweza kupoteza uhusiano kwa kutolipa.

Kukopa kutoka kwa taasisi ya kifedha (benki, taasisi ndogo ya kifedha, au Shirika la Muungano la Akiba na Mikopo)	• Haraka (kutegemea mtoaji) • Ufikivu • Imesajiliwa kwa mujibu wa mahitaji ya kisheria • Sehemu ya kikundi ambacho kinaweza kutoa maoni (vipengele vya • kijamii/msaada wa pamoja) • Baadhi huwa na dhamana zenye unyumbufu au bila dhamana Kupata kiasi kikubwa cha pesa za kutekeleza mradi husika	• Katika baadhi ya taasisi, huenda usipate pesa zote unazohitaji • Huenda zisiwe na mpango unaofaa kwa mradi wako • Viwango vya riba wakati mwingine viko juu • Baadhi huhitaji uwe kampuni iliyosajiliwa • Dhamana rasmi huenda zikahitajika (hati za malipo ya mshahara, rehani) Huenda tukatengwa kutokana na usuli wa kibiashara. • Ada za adhabu ikiwa hutalipa

MUHTASARI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.2.1

Istilahi na ujelezi unaohusiana na mikopo ya muamana

- RIBA
- ADA ZA ADHABU
- DALALI WA MUAMANA:
- KIASI CHA
- MDHAMINI/ DHAMANA
- MCHANGO WA KIBINAFSI
- REH ANI
- MALIPO YA MAPEMA
- KUTAFAKARI UPYA
- KIPINDI CHA NYONGEZA

- Kiasi cha pesa ambacho mkopaji hulipa mkopeshaji, zaidi ya kulipa kiasi cha mkopo wenyewe, ili kuweza kutumia pesa za mkopeshaji.
- Kiasi ambacho mkopaji atahitajika kumlipa mkopeshaji ikiwa atashindwa kulipa mkopo (k.m. kutwaliwa kwa mali, gari, akiba...)
- Mtalamu anayeaminiwa na wateja wake kuwatafutia mikopo inayowafaa zaidi na/au ya nafuu zaidi (kwa jumla mikopo ya rehani) kutoka benki na taasisi zingine za kifedha.
- Kiasi cha mkopo ambacho kinatolewa na mkopeshaji
- Mtu atakayelipa mkopo wako ikiwa utashindwa kufanya hivyo. Mtu huyu anaweza kuombwa kutia sahihi yake kwenye makubaliano na mkopeshaji. Dhamana pia inaweza kuwa katika mfumo wa mali.
- Sehemu ya ufadhili kwa mradi wako ambayo unamiliki kabla ya kukopa pesa zaidi kutoka kwa taasisi ya kukopesha. Mchango huu utajumuisha zaidi pesa taslimu na akiba yako.
- Kuweka dhamana ya mali unayomiliki kama dhamana ili kupata mkopo kutoka kwa taasisi ya kifedha. Ikiwa malipo yatakosa kufanywa, mkopeshaji anaweza kuchukua/au kutwaa mali inayohusika na kuiuza ili kupata pesa ambazo alikuwa amekopesha pamoja na ada. Mmiliki hapotezi umiliki wa mali iliyowekwa rehani alimradi anatimiwa wajibu wake wa kufanya malipo.
- Kulipa sehemu ya mkopo au mkopo wote kabla ya muda wa makubaliano
- Kubatilisha makubaliano ya muamana bila ada ya adhabu. Muda wa "kujituliza" unakukinga dhidi ya kununua vitu kiholela
- Muda unaoruhusiwa baina ya kupokea mkopo na malipo ya kwanza (nunua sasa, lipa baadaye)

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.3.1

Kuhesabu gharama ya mkopo wa Otieno (imekamilika)

JINA LA MPANGO	BENKI YA	SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI	POCHI LA
Kiwango cha Asilimia kwa	16%	20%	18%
Muda wa kulipa	36	24	12
Kiasi cha kulipa kila mwezi (ada kwa mwezi)	Shilingi 1,582.07	Shilingi 2,290.31	Shilingi 4,125.60
Kiasi cha jumla cha kulipa (Muda wa kulipa mkopo x ada kwa mwezi)	Shilingi 1,582.07 x 36 = Shilingi 56,954.52	Shilingi 2,290.31 x 24 = Shilingi 54,967.44	shilingi 2,620.16 x 12 = Shilingi 49,507.20
Gharama halisi ya mkopo (kiasi cha jumla cha kulipa ukiondoa kiasi cha mkopo ambacho Otieno ameomba)	Shilingi 55,423.80 - Shilingi 45,000 = Shilingi 11,954.52	Shilingi 54,967.44 - Shilingi 45,000 = Shilingi 9,967.44	Shilingi 49,507.20 - Shilingi 45,000 = Shilingi 5,507.20

MUHTASARI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO D.3.3

Jedwali lenye muhtasari wa masuala yaliyomwathiri Mhusika katika kuchagua mkopeshaji na mkopo (imekamilika)

KIGEZO CHA OTIENO CHA KUCHAGUA MKOPESHAJI NA MKOPO

VIPENGELE	BENKI YA NDANI	SHIRIKA LISILO LA KISERIKALI	POCHI LA KIDIJITALI
Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka (APR)	• Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka cha chini zaidi • Gharama halisi ya juu zaidi ya mkopo	Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka cha juu zaidi • Gharama halisi ya wastani ya mkopo	• Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka cha Wastani • Gharama halisi ya chini zaidi ya mkopo
Wepesi wa kufikia mkopo / masharti	• Inawezekana, lakini ndio mkopo ghali zaidi	• Inawezekana tu ikiwa atakuwa mwanachama na kuhudhuria mafunzo kwa miezi 3	• Haiwezekani, kwa sababu uwezo wa Otieno wa kufanya malipo hautoshi.
Kiasi cha pesa anachoweza kukopa	• Kiasi cha kutosha	• Kiasi cha kutosha	• Kiasi cha kutosha
Matukizi ya kulipa	• Kwa mwezi	• Kwa mwezi	• Kwa mwezi
Usaidizi na upatikanaji wa huduma zisizo za kifedha	• La	• Ndiyo	• La
HITIMISHO	• Huu ni mkopo ambapo atalipa pesa nyingi zaidi, lakini hii ni kwa sababu anaweza kuulipa kwa miaka 3. Ndio wenye malipo ya chini zaidi kwa mwaka. Ataweza kuthibitisha uwezo wake wa kulipa	• Mkopo huu una Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka cha chini zaidi. Anaweza kupata usaidizi. Anahitajika kuwa mwanachama na kusubiri siku 30. •	Huu ndio mkopo wenye muda mfupi zaidi wa kufanya malipo. Kwa jumla angelipa pesa kidogo kwa jumla. Kiwango cha Asilimia kwa Mwaka ni cha Wastani. Malipo kwa mwezi yako juu sana kwa uwezo wake wa kulipa.

E

KUCHAGUA MBINU YA MALIPO NA YA KUTUMA PESA

E1. Kadi ya kutoa pesa ni kadi ambayo ninaweza

- ☐ **a.** Kutoa pesa na kufanya malipo.
- ☐ **b.** Kutoa pesa pekee.
- ☐ **c.** Kutoa pesa, hata wakati sina pesa katika akaunti yangu.

E2. Mtu ameiba kadi yangu ya benki, napaswa kufanya nini?

- ☐ **a.** Mwizi hana nywila yangu, kwa hivyo sina wasiwasi. Sitafanya chochote.
- ☐ **b.** Nitawasiliana haraka na benki izuie kadi hiyo.
- ☐ **c.** Nitawasiliana haraka na benki inipe kadi mpya.

E3. Utumaji wa pesa unaruhusu

- ☐ **a.** Kufungua akaunti ya benki.
- ☐ **b.** Kutuma pesa kutoka sehemu moja hadi nyingine.
- ☐ **c.** Kufikia kadi ya malipo ya kulipia ununuzi wako

E4. Ni mbinu gani salama zaidi ya kutuma pesa nyumbani?

- ☐ **a.** Kumuomba mwenzangu kupeleka pesa nyumbani
- ☐ **b.** Kupitia njia rasmi ya kutuma pesa au pochi la kidijitali.
- ☐ **c.** Kumuomba mtu wa familia,

Majibu: E1:a; E2:b; E3:b; E4:b

1. TUMIA MBINU ZA MALIPO ZENYE USALAMA

Katika somo lililotangulia, tulieleza jinsi ya kuchagua mpango wa mkopo na kuweka akiba unaofaa kwa mahitaji yako. Sasa tutaangazia njia bora zaidi ya kutumia mbinu tofauti za malipo, kwa mfano kwa kulipia vitu unavyonunua.

Ikiwa unataka kulipia ununuzi wako, je, ni mbinu gani unazoweza kutumia kulipa?

Mbinu tofauti za malipo na kufanya malipo

- Pesa taslimu
- Kadi ya Benki
- Malipo kupitia mtandaoni
- Utumaji kupitia benki na malipo ya moja kwa moja
- Pochi la Kidijitali
- Mamlaka ya kielektroniki
- Malipo kupitia simu za mkononi (ikiwa huduma inapatikana katika nchi husika)
- Kubadilishana mali

Mwishoni mwa somo hili, katika Majibu kwa mazoezi utapata jedwali lenye manufaa na hasara za kila mbinu ya malipo.

Uchunguzi Kifani N°1

NJAMBI AMEFURAHIA SANA KADI YAKE YA KWANZA

Tangu aliporejea Kenya, Gloria na Njambi wamekuwa marafiki wazuri. Njambi amekuwa akifanya kazi katika hoteli kwa miaka kadhaa.

Jana, walizungumza kwa simu na Njambi akamweleza Gloria kwamba alikuwa amepata njia bora ya kudhibiti matumizi yake kwa kutumia aina mpya ya kadi.

Njambi alikuwa na furaha sana kwa sababu kadi hii ilimruhusu kutoa pesa kupitia mashine ya ATM, kukagua salio lake, na kulipia bidhaa. Muhimu zaidi, anaweza kutumia tu pesa ambazo ameweka katika salio lake. Kwa njia hii, anaweza kudhibiti matumizi yake vyema zaidi.

Uchunguzi Kifani N°2

KYALO, BABAKE MUTUA, ANATUMIA KADI YAKE

Miezi michache iliyopita, dobi ambapo babake Mutua, Kyalo anafanya kazi iliwafahamisha wafanyakazi wake kwamba ingebadilisha namna wanavyopokea mishahara yao. Kuanzia mwezi huu, Kyalo atakuwa anapokea mshahara wake kupitia benki. Ili kutumia pesa zake, benki ilimtumia Kyalo kadi ya benki na mmoja wa wenzake anaomba amweleze jinsi ya kuanza kuitumia.
Kwanza, anaenda kwa mashine ya ATM na kutumia kadi hiyo kutoa pesa. Pia anakagua salio lake. Akiwa njiani kurudi nyumbani, anaingia katika duka jipya ambalo limefunguliwa na kununua mboga na matunda. Anapofika nyumbani, anamwambia Mutua na Kalekye yote ambayo ameweza kufanya na kadi yake. Amefurahi sana!

Uchunguzi Kifani N°3

WANGI, RAFIKIYE WANGARI, ANATUMIA KADI YAKE

Wangari na Wangi ni marafiki wazuri sana. Ingawa Wangi amekuwa Qatar kwa miaka miwili, wao hupata muda wa kuzungumza kwa simu na kushiriki habari.
Jana, Wangari alipokea arafa kutoka kwa Wangi akimuomba ampigie simu.
Wangari alikuwa na wasiwasi, kwa hivyo alimpigia Wangi simu punde tu alipofika nyumbani. Wangi alikuwa amekata tamaa. Alimweleza Wangari kwamba alikuwa amepokea kadi kutoka kwa benki yake ambapo mwajiri wake humlipia mshahara. Alikuwa anaitumia kadi hiyo sana mwanzoni, kwa vile alikuwa na matumizi mengi. Siku zinapita na anazidi kutumia kadi yake bila kuwa makini sana kuhusu matumizi yote anayofanya. Anafikiri kwamba atakagua matumizi yake wikendi, lakini hapati muda wa kufanya hivyo. Mwishoni mwa mwezi wa kwanza, anagundua kwamba hana pesa za kutosha kulipia matumizi aliyofanya na kadi yake ya benki. Pia atahitajika kulipa riba na ikiwa hatalipa, kutakuwa na madhara makubwa. Wangari anajaribu kumtuliza, lakini Wangi anajilaumu kwa kukosa uangalifu.

UJELEZI

Kadi ya Malipo ya Awali au Kadi ya Pesa

Hii ni kadi inayokuruhusu kutoa pesa kutoka kwenye akaunti yako kwa kuitia ndani ya mashine ya ATM. Kando na uwezekano wa kutoa pesa, unaweza kukagua salio la akaunti yako. Unaweza kununua chakula, mafuta, na nguo, alimradi mtu au duka unapolipa linakubali malipo ya kadi. Pesa unazotumia zinakatwa moja kwa moja kutoka kwa salio lako. Baadhi ya kadi zinaweza kukuruhusu ulipie bili na muda wa maongezi katika simu yako ya mkononi. Kila benki iko na mtandao wake wa mashine za ATM lakini mara nyingi unaweza kutumia kadi yako ya benki kutoa pesa katika mashine yoyote ya ATM iwe ni ya benki yako au la. Hata hivyo, benki yako huenda ikakutoza ada kila mara unapotumia mashine ya ATM ambayo ni ya mtandao wa benki tofauti. Unaweza tu kutumia pesa ambazo zipo katika salio lako. Unaweza kuongeza pesa mara nyingi uwezavyo kupitia kwa mashine za ATM, utumaji wa benki au hata kwa kutumia mtandao wa mawakala. Baadhi ya pochi za kidijitali hutoa uwezo wa kuweka pesa katika kadi yako ya pesa kupitia kwa programu ya simu mahiri.

Kadi ya Malipo

Kadi ya malipo inaruhusu miamala ya benki ya kielektroniki Mbali na kuitumia kutoa pesa katika mashine za ATM, unaweza kutumia kadi ya malipo kulipia bidhaa unazonunua dukani.

Lazima uwe na pesa katika akaunti yako wakati wa ununuzi. Kiasi cha ununuzi wako kinatolewa kutoka akaunti yako mara moja. Unaweza kukagua salio lako mara kwa mara kupitia kwa huduma za benki kwenye simu au mtandaoni au rununu. Katika baadhi ya hali, unaweza kupokea taarifa kutoka benki au taasisi ya kifedha, ikionyesha kiasi cha jumla kilichokatwa kutoka kwa akaunti yako pamoja na salio lako.

Kadi ya Mkopo

Kwa jumla, kadi ya mkopo inakuruhusu kufanya miamala kama ilivyo kwa kadi ya pesa na kadi ya Malipo. Tofauti kuu ni kwamba inaruhusu kupata mkopo wa papo hapo. Hii ni iwapo huna pesa katika akaunti yako, bado unaweza kununua katika duka kwa kuchukua mkopo kutoka kwa taasisi ya kifedha ambayo ilikuuziwa kadi ya mkopo (taasisi ya kifedha, duka la jumla...).

Kwa mujibu wa masharti ya kununua kadi ya mkopo, kiasi cha ununuzi/mkopo kitakatwa kutoka kwenye akaunti yako (mara moja au mara nyingi, kwa kiwango cha riba ambacho kwa kawaida huwa juu kuliko mipango ya kawaida ya mikopo). Utapokea taarifa za mara kwa mara kutoka kwa taasisi ya kifedha ambayo ilikuuzia kadi ya mkopo, ikionyesha jumla ya kiasi kilichokatwa kwenye kadi yako ya mkopo, kiasi ulicholipa na kiwango cha riba. Siku hizi pia unaweza kukagua taarifa hii mtandaoni.

u POCHI ZA KIDIJITALI

Uchunguzi Kifani N°4

KALEKYE, MAMAKE MUTUA, ANALIPA KUPITIA POCHI LA KIDIJITALI

Mutua anataka kumfunza mamake jinsi ya kutumia pochi la kidijitali. Anajua kwamba, wakati atakapokuwa Kuwait, itakuwa rahisi zaidi kwake kumtumia pesa ikiwa atakuwa na pochi la kidijitali. Hata hivyo, Kalekye hajawahi kupendezwa na teknolojia licha ya marafiki wake wengi kutumia vifaa hivi kufanya ununuzi na kupokea pesa. Anafikiri ni changamano sana kwake.

Alasiri moja, Mutua na Kalekye wanaenda sokoni pamoja kununua mboga na matunda. Inapofika wakati wa kulipa, mwanaume anayepokea malipo anamwambia Kalekye kwamba anaweza kulipa kutumia pesa taslimu au pia kupitia kwa pochi la kidijitali. Kalekye alikuwa amepakua pochi la kidijitali na kuweka Shilingi 3,000, lakini hajawahi kuitumia na anaogopa kufanya makosa Mutua anamkumbusha kwamba kutumia pochi la kidijitali ni rahisi na salama kuliko kutumia pesa taslimu. Mwishowe, Kalekye anafungua pochi hilo la kidijitali, analeta simu yake karibu na kituo cha malipo katika duka hiyo (kituo ambacho wanatumia pia kwa malipo ya kadi mara nyingi) na ujumbe wa “Malipo Yamefanyika” unatokea kwenye simu yake. Amefurahi sana, ilikuwa rahisi zaidi ya alivyofikiri. Akielekea nyumbani, Mutua na Kalekye wanazungumza kuhusu matumizi mengine ya pochi la kidijitali.

Uchunguzi Kifani N°5

WANGARI ANALIPA KWA KUTUMIA MSIMBO WA QR

Wangari anaandaa kila kitu kwa safari yake ya Qatar. Mojawapo wa vitu ambavyo bado anahitaji kununua ni chaja mpya ya kisasa kwa simu yake mahiri Anapoenda jijini, anapata duka la jumla linalouza aina zote za bidhaa za kielektroniki. Baada ya kupata chaja inayofaa, anaenda kulipia na anaona kibandiko kikionyesha kuwa duka hilo linakubali malipo kwa kutumia msimbo wa QR Wangari anakumbuka kuwa kuna programu mpya ya pochi la kidijitali kwenye simu yake na anaamua kuijaribu. Mwanamke anayepokea malipo anamweleza kwamba anahitajika kufungua pochi la kidijitali na kuchanganua msimbo wa QR. Baada ya kuuchanganua, anahitajika kuthibitisha jina la duka hilo na thamani ya muamala kabla ya kukubali ombi la malipo. Mwishowe, Wangari anathibitisha muamala huo kwa kuweka nambari ya siri. Na anakuwa ameshalipa! Malipo yamekamilika. Wangari anapokea ujumbe wa arafa kwenye programu hiyo ya simu mahiri ukithibitisha kwamba pesa zimetolewa kutoka kwenye pochi lake la kidijitali. Wangari anafurahia sana kutumia mbinu hii ya kufanya malipo kwa mara ya kwanza na anatazamia kumweleza rafiki yake kuhusu hili.

UJELEZI

Pochi la kidijitali linarejelea kifaa cha kielektroniki, huduma za mtandaoni, au programu ambayo inaruhusu mtu kufanya miamala ya kielektroniki na wahusika wengine wanaobadilishana vizio vya sarafu za kidijitali kulipia bidhaa na huduma.

	Manufaa	Hasara
Pochi la Kielektroniki	• Unaweza kutoa pesa dukani: hakuna haja ya kupanga foleni kwenye mashine za ATM au benki. • Hauhitaji kubeba pesa wakati unapolipia bili au kumlipa mtu mwingine. • Pochi lako la kielektroniki limelindwa kwa nambari ya siri: pesa zako ziko salama. • Hauhitaji kujaza fomu zozote ili kutoa au kuweka pesa, kama unavyofanya unapoenda benki. • Wauzaji huwa hawakosi pesa. • Huhitaji kuwa na akaunti ya benki. • Miamala inafanyika papo hapo. • Inakuruhusu kulipa boli na kutuma pesa kwa urahisi, na kwa njia inayoweza kufuatiliwa na salama.	• Unaweza kusahau nambari yako ya siri. • Simu yako ya mkononi inaweza kuibiwa. • Ikiwa hutafuatilia matumizi yako, huenda ikawa vigumu kuzingatia bajeti yako.

VIDOKEZO VYA USALAMA KWA POCHI ZA KIDIJITALI

- Usishiriki nambari yako ya siri na mtu yeyote.
- Usiweke rekodi ya nambari yako ya siri karibu au pamoja na kadi yako ya simu.
- Usihifadhi nambari yako ya siri katika simu yako.
- Kila mara dai kuangalia gharama za miamala mbalimbali, hasa wakati unapotumia wakala.
- Unapomtumia mtu pesa, thibitisha jina na kiasi kabla ya kutia nambari yako ya siri.



Uchunguzi Kifani N°6

KYALO, BABAKE MUTUA ANASAHAU NAMBARI YAKE YA SIRI

Imekuwa wiki kadhaa tangu Kyalo alipopata kadi mpya ya benki. Amefurahia sana kila kitu anachoweza kufanya na kadi hii. Asubuhi, Kalekye anamkumbusha kwamba anahitajika kutoa pesa fulani ili walipie ada ya bima ya afya ya kitaifa. Akielekea kazini, anaingia mahali palipo na mashine ya ATM na kuanza mchakato wa kutoa pesa. Anaweka nambari ya siri kama ilivyoagizwa na mashine ya ATM lakini msimbo si sahihi. Kwa mshangao, Kyalo anaandika upya nambari yake ya siri lakini tema mashine inakataa muamala. Anatafakari kwa muda, lakini amechanganyikiwa sana. Anajuwa kwamba amechelewa kazini, lakini anajaribu mara ya tatu kwa kubadilisha nambari yake ya siri. Mashine ya ATM inakataa shughuli hiyo na kubakiza kadi.

Kyalo anakasirika sana, anashindwa kutoa pesa na zaidi ya hayo kadi yake imesalia kwenye mashine!

VIDOKEZO VYA USALAMA KWA MBINU YA MALIPO

- Tumia mbinu yako ya malipo kwa makini, kila mara ukifikiria kuhusu kusalia ndani ya bajeti yako.
- Weka kadi yako, kitabu cha hundi, pochi na rununu mahali salama.
- Usiwahi mpa mtu kadi yako ya mkopo au kitabu cha hundi.
- Usiwahi tia sahihi kwenye hundi tupu (bila kuandika kiasi cha pesa).
- Usiwahi kuandika msimbo wa siri kwenye kadi yako ya benki au kuuacha karibu.
- Usiwahi tuma taarifa ya siri kwa njia ya barua pepe, arafa, faksi...
- Kuwa makini unapofanya muamala mtandaoni. Kagua usalama wa tovuti unazotumia (anwani ya tovuti inastahili kuanza kwa “https”, na kunapaswa kuwa na ishara ya kufuli upande wa kulia sehemu ya chini ya skrini...)
- Kagua taarifa yako ya benki kwa makini na kila mara.
- Ripoti haraka kwa benki yako kuhusu pesa zozote zinazotolewa kutoka akaunti yako na ambazo huwezi kueleza.



MUHIMU: Kusimamia pesa zako, hasa wakati unatumia mbinu tofauti za malipo, huenda ikawa changamano. Inaweza pia kuwa shughuli ya kuchosha. Fuata vidokezo vya usalama vilivyopo hapo juu kwa utulivu wako wa akili.

UJUMBE MUHIMU

- Kuna njia mbalimbali za malipo: pesa taslimu, kadi ya malipo au shughuli ya malipo: utumaji wa benki, agizo la kukata pesa, malipo ya simu ya mkononi au kupitia intaneti...
- Kila mbinu ya malipo ni tofauti. Kama ilivyo kwa mipango ya kifedha, kila moja inahusisha gharama na iko na manufaa na hasara, ambazo mara nyingi zinategemea aina ya matumizii ambayo unataka kulipia.
- Kadi ya pesa inakuruhusu kutoa pesa, kukagua salio lako, na katika baadhi ya hali, pia kulipa bidhaa, bila kuwa na akaunti ya benki. Kadi ya malipo ni kadi iliyounganishwa kwa akaunti yako ya benki na inakuruhusu kutumia mashine za ATM kulipia chakula na huduma.
- Pamoja na kukuruhusu kutoa pesa na kulipia ununuzi, kadi ya mkopo inakuwezesha kufikia mkopo wa papo hapo Ikiwa pesa zinazohitajika hazipo katika akaunti yako wakati wa ununuzi).
- Pochi za Kidijitali ni njia nzuri ya kutumia teknolojia katika jinsi unavyotumia pesa zako na kutumia pesa taslimu kwa kiasi kidogo. Inaweza kuwa njia kuu ya kuanza kutumia taasisi za kifedha.
- Matumizi ya mbinu za malipo yanaleta hatari! Tumia mbinu yako ya malipo kwa uangalifu kila mara ukifikiria jinsi ya kusalia ndani ya bajeti yako.

2. PATA KUFAHAMU WATOAJI WA HUDUMA ZA KUTUMA PESA

Sasa tutaangazia chaguzi zako wakati unataka kutuma na kupokea pesa, katika nchi huu na ughaibuni. Tutazingatia manufaa na hasara za kila mbinu.

Uchunguzi Kifani N°7

WANGARI HAJUI PESA ZIKO WAPI

Wangari amepanga kila kitu ili kwenda Qatar, anahitaji tu pesa kidogo zaidi. Kwa kuwa hataki kusubiri zaidi, anaamua kumuuliza rafiki yake, Wangi, ambaye anaishi Qatar, amsaidie pesa fulani. Wangi anaamua kumsaidia na anamweleza kuwa rafiki ya rafiki yake anasafiri kuja Kenya wiki ijayo, kwa hivyo anaamuwa kumpa pesa mwanamke anayeishi katika jiji la karibu na anakoishi Wangari.

Siku chache baadaye, Wangari anazungumza na Wangi kwa sababu bado hakuwa amepokea pesa hizo. Wangi anafikiri mwanamke huyo ni mwaminifu lakini anaanza kuwa na wasiwasi. Wangari pia amesikia visa kama hivi ambapo pesa hazifiki kamwe. Anatumai kwamba hali haitakuwa hivyo kwa sababu hiyo inamaanisha huenda pesa hizo zisiwahi kumfikia.

Uchun guzi Kifani N°8

GLORIA ANATUMIA MTOAJI RASMI

Baada ya mazungumzo marefu, Gloria na Gitau ameamua kwamba ni ghali mno kwa wanne hao kusafiri kwenda Nakuru kuwatembelea wazazi wa Gitau. Badala yake, wanaamua kuwalipia Mumo na Musau tikiti, ili wao waje kuwatembelea huko Syokimau.
Kwa kuwa mashemeji zake hawana akaunti ya benki au pochi la kidijitali, Gloria anatumia wakala wa kutuma pesa ili kuwatumia pesa. Amekuwa akitumia mtoaji huyu kila mara, lakini rafiki kutoka kazini alimweleza hivi majuzi kwamba kulikuwa na mtoaji moja wa huduma za kutuma pesa ambaye ni nafuu zaidi mkabala na saluni ambapo wanafanya kazi. Gloria aliamua kujaribu na kwenda kwa mtoaji mpya. Alijaza fomu ya kutuma pesa.

Mwanaume aliye kwenye kaunta anampa orodha ndefu ya mawakala ambapo Mumo na Musau wangeweza kupokea pesa hizo. Gloria alimpigia simu Mumo na kumpa anwani ya wakala aliye karibu na eneo lake. Gloria alihitajika kulipa ada ndogo kuwatumia Mumo na Musau pesa, na ilikuwa nafuu kuliko alivyokuwa akilipa kwa mtoaji huyo mwingine. Baadaye siku hiyo, Mumo alienda kwa wakala huyo. Habari njema! Mumo amempigia Gloria simu na kumueleza kwamba alionyesha Kitambulisho chake na akapokea pesa hizo!

UJELEZI

Watoaji wasio rasmi wa huduma za kutuma pesa
Taasisi hizi na watu binafsi hawadhibitiwi au kusimamiwa na Serikali.

Watoaji rasmi wa huduma za kutuma pesa
Taasisi hizi zinadhibitiwa na kusimamiwa na Serikali.

WATOAJI RASMI WA HUDUMA ZA KUTUMA PESA	WATOAJI WASIO RASMI WA HUDUMA ZA KUTUMA PESA
•Posta (kupitia ofisi ya ndani au mtandaoni) •Watoaji wa huduma za Kutuma Pesa •Benki (kupitia matawi ya benki au mtandaoni) •Pochi za kidijitali	•Wenye maduka na wafanyabiashara •Madereva wa teksi na malori •Marafiki na Jamaa

Licha ya mtoaji wa huduma utakayechagua kutuma pesa, iwe ni rasmi au sio rasmi, unahitaji kupitia msururu wa vigezo kabla ya kufanya uamuzi wako:

- Gharama ya kutuma pesa (kulipwa na mtumaji).
- Gharama ya kupokea pesa (kulipwa na mpokeaji).
- Umbali kijiografia lkwa mtumaji na mpokeaji).
- Usalama.
- Kasi.
- Mrabaha wa ubadilishaji pesa (ikiwa unahusika)

MASWALI

- Na wewe? Je, unawatumia watu pesa, au kutuma ughaibuni?

☐ Ndiyo ☐ La

- Ikiwa ndiyo, kwa sababu gani?
- Unatumia mbinu gani?

HALI YA KIBINAFSI

Kwa kuangalia hali yangu ya kibinafsi, mbinu inayonifaa zaidi kutuma pesa ni

Hii ni kwa sababu :

UJUMBE MUHIMU

- Ni muhimu kufahamu taratibu za kutuma pesa (hati zinazohitajika, gharama, mtandao wa watoaji huduma...).
- Kuna njia mbalimbali za kutuma pesa: pesa taslimu kwa pesa taslimu, akaunti ya benki kwa pesa taslimu, pesa taslimu kwa akaunti ya benki, akaunti ya benki hadi akaunti ya benki, simu ya mkononi hadi simu ya mkononi...
- Chagua mbinu ya kutuma na mtoa huduma kulingana na hali yako na ya mtu ambaye unatumia pesa. Kwa kuangalia sifa kama vile gharama ya kutuma, mrabaha wa kubadilisha, gharama ya kupokea pesa, umbali wa kijiografia, n.k.) hukusaidia kufanya uamuzi ambao unafaa zaidi kwa mahitaji yako.
- Tuma pesa kwa njia salama, tumia mbinu rasmi na uwezeshe utoaji kwa jamaa zako!

KISAIDIZI CHA MAFUNZO E.2.1

Watoaji wasio rasmi wa huduma za kutuma pesa



KISAIDIZI CHA MAFUNZO E.2.2

Watoaji rasmi wa huduma za kutuma pesa

KISAIDIZI CHA MAFUNZO E.2.3

Mbinu za utumaji zilizochaguliwa na wahusika

Mbinu ya Gloria

Gloria anatuma pesa kwa wazazi wa Gitau kupitia kwa Mtoaji wa huduma za kutuma pesa.

Mbinu ya Otieno

Otieno analipa malipo ya mkopo kupitia utumaji wa benki. Kwa njia hii, anaweza kuweka rekodi za malipo yake na anaweka ushahidi wa kutuma.

Mbinu ya Mutua

Mutua alimfunza mamake Kaleyke jinsi ya kutumia pochi la kidijitali. Sasa akiwa Kuwait, itakuwa rahisi zaidi kwake kumtumia pesa kwa kutumia pochi la kidijitali.

Mbinu ya Wangari

Baada ya tajriba mbaya, Wangari alianza kutumia pochi la kidijitali kutuma na kupokea pesa. Ni haraka na salama.

3. JINSI YA KUTUMA NA KUPOKEA PESA

KISAIDIZI CHA MAFUNZO E.3.1

Hatua katika kutuma na kupokea pesa

MBINU YA 1: Kupitia kwa mtoaji wa huduma za kutuma pesa

- Wasiliana au utemblee benki au taasisi ya kifedha (wewe mwenyewe au mtandaoni);
- Jaza fomu sahili ya kutuma pesa;
- Mwendee karani na umpe taarifa ifuatayo;
  1. Jina na nambari ya akaunti ya anayepokea pesa (ikiwa anayepokea, k.m. mtu unayemtumia pesa, yuko na akaunti ya benki),
  2. Jina na nambari ya kitambulisho au hati nyingine ya utambulisho ya anayepokea (ikiwa anayepokea hana akaunti ya benki);
- Mfahamishe anayepokea kuhusu kiasi cha pesa ambacho umetuma na, kulingana na muda ulioonyeshwa na benki/wakala (ambao unaweza kuwa kuanzia dakika chache hadi siku kadhaa), mpokeaji ataweza kupokea pesa kutoka kwa benki au wakala, ikiwa pesa taslimu au kulipwa ndani ya akaunti yake (kama ulivyobainisha).

- Nenda kwa benki au wakala na umpe karani taarifa inayohitajika kuhusu kiasi cha pesa ambacho umetumiwa na jina la mtu aliyetuma.
- Muonyeshe karani wa benki kitambulisho chako au hati nyingine ya kuthibitisha utambulisho wako.
- Baada ya kukagua kwenye mfumo wa tarakilishi, karani au wakala atakupa pesa hizo.
-

MBINU YA 2: Kupitia kwa benki yangu kwa kutumia huduma za simu/mtandaoni

- Weka anwani ya tovuti ya benki yako. Jaza jina lako la matumizi na nywila yako.
- Baada ya kuingia kwenye mfumo, chagua akaunti ambapo unataka kutoa pesa.
- Bonyeza kwenye Hamisha Pesa/Tuma Pesa Wakati mwingine utendaji huu unaweza kupatikana kwenye kichupo cha Malipo.
- Ukishafika kwenye kitengo cha Utumaji, utaweza kujaza taarifa ifuatayo:
  - Tarehe ya kutambua.
  - Unakotuma: Hapa utaweza kujaza Lakabu na/au nambari ya akaunti ya benki ya anayepokea
  - Sarafu: kwa kawaida, sarafu ya ndani lakini pia inaweza kuwa sarafu ya kimataifa.
  - Kiasi: Jaza kiasi unachotaka kutuma.
  - Maelezo: chagua maelezo ya malipo (Mali, Mengineyo, Kodi au maelezo mengine yanayotokea kwenye paneli kunjuzi).
  - Ufafanuzi: huu ni ujumbe unaotumwa kwa anayepokea.
  - Barua pepe ya anayepokea: ili taarifa imfikie anayepokea.
- Bonyeza Endelea ili Kutuma na pesa zitatumwa tarehe uliyochagua. Baadhi ya benki huenda zikahitaji hatua ya ziada ya usalama (huenda ikawa arafa inayotumwa kwenye simu yako ambayo unahitaji kujumuisha katika kuthibitisha muamala, pia huenda ikawa nambari ya siri ya ziada inayozalishwa kwa ajili ya shughuli hizi). Kwa jumla, utapokea uthibitisho kwenye tovuti hiyo hiyo au kupitia barua pepe kwamba pesa zimetumwa kwa ufanisi.

- Weka anwani ya tovuti ya benki yako. Jaza jina lako la matumizi na nywila yako.
- Baada ya kuingia kwenye mfumo, chagua akaunti ambapo umetumiwa pesa. Ukishaingia na unapoangalia taarifa za akaunti hiyo, unapaswa kuona mapato mapya ya kiasi ulichotumiwa na maelezo yanayoonyesha nani ametuma pesa hizo na alizituma lini.

MBINU YA 3: Kupitia pochi langu la kidijitali

- Fungua programu katika simu yako. Lazima iwe programu sawa na ile inayotumiwa na anayepokea.
- Bonyeza kwenye menyu na uchague “Tuma Pesa”.
- Katika sehemu ya “Kwa” unaweza kuchagua mwasiliani kutoka kwa simu yako, nambari ya simu au anwani ya barua pepe.
- Weka kiasi unachotaka kutuma, chagua sababu ya kutuma pesa (kwa mfano, kurejesha pesa zilizokopwa au pesa za chajio ya jana) na ubofye kitufe cha ‘endelea’.
- Chagua mbinu ya kulipa. Inaweza kuwa salio la pochi yako ya kidijitali au pia njia zozote za malipo ambazo tayari umeunganisha kwenye pochi yako ya kidijitali (kadi ya malipo, kadi ya mkopo au akaunti ya benki). Ikiwa unataka kufanya hivi kupitia kadi mpya, programu itakuomba utie taarifa za kadi hiyo. Kwa kubonyeza endelea, programu itathibitisha utumaji wa pesa hizo.
-

- Unaweza kupokea taarifa kutoka kwa programu yako moja kwa moja kwenye simu yako kwamba umepokea pesa.
- Ukifungua programu hiyo, utagundua kwamba malipo yameonyeshwa mara moja katika salio lako na muamala wa mwisho. Pesa ulizopokea zinapatikana mara moja, yaani kwa wakati ule ule ambapo aliyekutumia pesa anakamilisha muamala huo.

MUHTASARI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO E.3.2

Fomu ya kutuma pesa (fomu ya mtoaji wa huduma za kutuma pesa)

FOMU YA KUTUMA PESA

Tarehe

Kiasi

Sarafu

TAARIFA YA ANAYETUMA

Jina la Ukoo:

Jina:

Anwani:

Nambari ya simu:

Tarehe na mahali pa kuzaliwa:

TAARIFA YA ANAYEPOKEA

Jina la Ukoo:

Jina:

Swali la majaribio ikiwa mpokeaji hata kitambulisho halali:

Huduma za hiari zinapatikana kwa gharama zaidi. Kagua huduma unazotamani:

- ☐ Nataka hundi itumwe kwenye anwani ifuatayo
- ☐ Nataka umpigie simu mpokeaji Ujumbe
- ☐ utakaotumwa

SAHIHI YA MJETA

KISAIDIZI CHA MAFUNZO E.3.3

Fomu ya kutuma pesa
(Fomu ya kutuma pesa kimataifa)

FOMU YA KUTUMA PESA

Tarehe

Kiasi

TAARIFA YA ANAYETUMA

Jina la Ukoo:

Jina:

Anwani:

Nambari ya akaunti:

TAARIFA YA ANAYEPOKEA

Jina la Ukoo:

Jina:

Anwani:

Nambari ya IBAN (Nambari ya Akaunti ya Benki ya Kimataifa, herufi zisizozidi 34):

Nambari ya BIC (Nambari ya Utambulisho wa Benki, baina ya herufi 8 na 11) au Msimbo wa SWIFT:

SAHIHI YA MJETA

UJUMBE MUHIMU

- Ni muhimu kufahamu taratibu za kutuma pesa (hati zinazohitajika, gharama, mtandao wa watoaji huduma...).

- Kuna njia nyingi tofauti za kutuma pesa: pesa taslimu kwa pesa taslimu, akaunti ya benki kwa pesa taslimu, pesa taslimu kwa akaunti ya benki, akaunti ya benki hadi akaunti ya benki, kadi ya pesa hadi pesa taslimu, kadi ya benki hadi akaunti ya benki, kadi ya benki hadi kadi ya benki, kadi ya benki hadi simu ya mkononi, simu ya mkononi hadi simu ya mkononi. Teknolojia inazidi kubadilika kila wakati. Hakikisha una taarifa kuhusu mbinu mpya, kwa kuwa huenda zikawa faafu zaidi kwako kuliko zile za awali.

- Kwa kuzingatia hali yako ya kibinafsi ya mtu ambaye unatumia pesa wakati wa kuchagua mbinu ya kutuma na mtoaji wa huduma (gharama ya kutuma, mrabaha wa kubadilisha sarafu, gharama ya kupokea, umbali wa kijiografia...), utaweza kufikia uamuzi ulio bora zaidi.

VIAMBATISHO NA HATI MUHIMU

Maswali ya kuuliza mtoaji rasmi wa huduma za kutuma pesa

- *Je, nitaweza kutuma pesa kwa jamaa?*
- *Ni fomu zipi ambazo nahitaji kujaza ili kutuma pesa?*
- *Ni fomu gani ambazo anayepokea pesa atahitajika kujaza?*
- *Ni hati gani za utambulisho ambazo zinahitajika kutuma pesa?*
- *Ni hati gani za utambulisho ambazo zitahitajika kupokea pesa?*
- *Je, nahitaji kuwa na akaunti ya benki na benki ya ndani ili niweze kutuma pesa?*
- *Je, inachukua muda gani kwa mtu aliyetumiwa pesa kuzipokea?*
- *Ikiwa nitatuma pesa kupitia kwa programu kwenye simu yangu, mtu ambaye atazipokea anahitaji kuwa na programu sawa?*
- *Je, nini gharama ya kutuma pesa?*
- *Je, mtu anayepokea pesa atapokea pesa zote zilizotuma, au kutakuwa na ada za ziada anapozipokea?*
- *Nitawezaje kukagua iwapo mtu anayepokea pesa kwa hakika amezipata?*
- *Je, mtu anayepokea pesa atafahamishwa kwamba pesa zimefika?*
- *Je, ninaweza kubatilisha au kubadilisha muamala?*
- *Je, ni kiwango gani cha ubadilishaji kinatumika kubadilisha pesa zangu kuwa sarafu ya nchi inayopokea (ikiwa ninatuma pesa ughaibuni)? Nini gharama ya ubadilishaji?*
- *Ikiwa nitatuma pesa katika Dola, je, mtu anayepokea atazipata pesa hizo katika sarafu gani?*
- *Je, nahitajika kuja kwenye benki mimi mwenyewe au kuna huduma za mbali za kutuma pesa (mtandao, barua...)?*
- *Je, mko na matawi au mawakala wa benki katika (mahali pa makazi ya jamaa ambaye unamtumia pesa)?*
- *Je, ninaweza kutuma pesa kupitia simu yangu ikiwa mtu huyo mwingine hana pochi la kidijitali? Ikiwa ndiyo, ni wapi wanaweza kutoa pesa nitakazotuma?*

MAJIBU KWA MAZOEZI

Manufaa, hasara na matumizi ya mbinu za malipo

Mbinu ya malipo	Manufaa	Hasara	Matumizi
Pesa taslimu	• Rahisi kutumia • Inakubalika na wengi (halali) • Hakuna ada • Ununuzi wa papo hapo unawezekana	• Hatari ya wizi au kupotea • Hakuna kitulizo ikiwa zitaibiwa au kupotea • Kuna udhibiti wa kiasi kinachoruhusiwa kwa miamala (si kila kitu kinaweza kulipiwa kwa pesa taslimu, Hasa wakati kiasi kikubwa cha pesa kinahusika) • Hazina ushahidi wa muamala (zinaweza kuwa tatizo kwa usimamizi wa bajeti)	• Kwa ununuzi wa kila siku wakati pesa ndogo zinahusika • Ili kupunguza kile unachoweza kutumia katika kipindi fulani au tukio fulani • Kuweza kununua kitu papo hapo
Kadi ya Benki	• Usalama (kwa jumla) • Huacha ithibati ya mahali na kiasi kwa kila muamala, na kitu kilichonununuliwa • Ulinzi dhidi ya wizi (nambari ya siri, kadi inaweza kubatilishwa ikiwa itaibiwa) • Inawezekana kufanya ununuzi unaohusisha kiasi kikubwa cha pesa • Zinaweza kuunganishwa na akaunti za benki katika nchi zingine (sio lazima mahali ninapoishi) • Inaweza kutoa ufikiaji kwa mipango ya upili: k.m. Msaada wa kisheria, bima wakati unanunua tikiti za ndege Kufikia huduma nyingine za kifedha (bima, msaada wa kisheria) • Zinaweza kuunganishwa na mipango ya kutuza uaminifu ambayo inaweza kuleta manufaa/vipunguzo	• Wakati mwingine huwa na ada za juu: ada kwa mwaka, ada kwa kutoa pesa, malipo yanayofanywa ughaibuni... • Hatari ya kukosa kufuatilia matumizi yako • Hatari ya kusahau unaposimamia bajeti yako • Haziwezi kutumiwa kila mahali: hutegemea muuzaji kuwa na kituo kinachofanya kazi	• Kwa kufanya malipo ya kila siku yanayohusisha kiasi kikubwa cha pesa • Kwa kufanya ununuzi mkubwa mara kwa mara • Kwa kununua bidhaa na huduma zikiwemo mipango inayohusika " (k.m. Kulipia tikiti za ndege ikiwa kadi inatoa bima)

Mbinu ya Malipo	Manufaa	Hasara	Matumizi
Utumaji wa Benki na utozaji wa moja kwa moja	•Haina haja ya kwenda popote wala kubeba pesa taslimu •Ununuzi unaweza kufanywa saa 24 kwa kila siku ya wiki •Aghalabu hukuwezesha kufikia mikataba mizuri	•Hakuna mtu wa kuwasiliana naye moja kwa moja (ikiwa tatizo litatokea) •Hatari ya utapeli ikiwa unanunua kutoka kwa tovuti ambazo sio salama •Uwezekano wa matatizo ya kufikisha bidhaa ulizonunua mtandaoni •Hatari ya kusahau matumizi katika usimamizi wa bajeti •Hatari ya kukosa kufuatilia matumizi	• Kupata mikataba mizuri •Kwa ununuzi wa haraka unaotoa faida kubwa (nguo, vitabu, DVD, tikiti za hafla, tikiti za ndege...) •Kwa vitu nadra vinavyopatikana tu kupitia mtandaoni •Kwa malipo ya bili (rununu) ikiwa huna akaunti ya benki
Pochi za kidijitali	•Hakuna haja ya kuwa na akaunti ya benki, unahitaji tu nambari ya simu na kadi ya simu •Njia rahisi ya kutuma pesa kwa mtu mwingine •Rahisi kulipa bili •Huweka rekodi ya matumizi yako kiotomatiki •Inakuruhusu kushughulikia pesa zako kwa njia salama •Huenda ikakufungulia njia ya kufikia huduma zingine za kifedha.	•Hatari ya simu kuibiwa •Hatari ya kusahau nambari ya siri/ nywila •Inaweza kuleta matatizo katika kufuata bajeti yako	• Kutuma pesa kwa watu wengine •Kulipa bila mtagusano wa moja kwa moja •Kulipa bili

MUHTASARI

JEDWALI LINGANISHI BAINA YA KADI TOFAUTI ZA BENKI (E1)

KADI	KADI YA PESA	KADI YA MALIPO	KADI YA MKOPO
Je, unaweza kutumia kadi hii wapi?	•Mashine za ATM kutoka benki yako na za mitandao mingine. •Katika maduka yanayokubali malipo ya kadi	•Mashine za ATM kutoka benki yako na za mitandao mingine. •Katika maduka yanayokubali malipo ya kadi	• Mashine za ATM kutoka benki yako na za mitandao mingine. • Katika maduka yanayokubali malipo ya kadi
Je, unaweza kufanya nini na kadi hii?	•Kukagua salio lako •Kutoa pesa. •Lipia bidhaa alimradi una pesa katika salio lako.	•Kukagua salio lako. •Kutoa na kuweka pesa. •Lipia bidhaa alimradi una pesa katika akaunti yako. •Kutuma pesa kwa akaunti nyingine. •Kuongeza muda wa maongezi kwenye simu yako.	•Kukagua salio lako. •Kutoa na kuweka pesa. •Lipia bidhaa alimradi una pesa katika akaunti yako. •Kulipia bidhaa hata ikiwa huna pesa katika akaunti yako kwa sasa. •Kulipia bidhaa kwa awamu. •Kutuma pesa kwa akaunti nyingine. •Kuongeza muda wa maongezi kwenye simu yako.
Je pesa zinakatwa papo hapo au baadaye?	•Papo hapo	•Papo hapo	• Ya baadaye, utalipa mwishoni mwa mwezi jumla ya ununuzi wako. Hutatozwa malipo ya riba alimradi utalipa kwa wakati na hutakopa salio
Je, kuna gharama/ada zipi kwa matumizi ya kadi hii?	Inategemea masharti ya kila mtoa huduma. Unastahili kupata taarifa zote na ulinganishe.		

MANUFAA NA HASARA YA WATOAJI WA HUDUMA ZA KUTUMA PESA (E2)

WATOAJI WA HUDUMA ZA KUTUMA PESA	MANUFAA	HASARA
RASMI	• Usalama (pesa ziko salama, na utumaji uko salama) • Mikopo ya muda mrefu na kiasi kikubwa cha pesa • Uhakika • Usiri • Chaguo la bidhaa • Hutenda kazi ndani ya mfumo wa udhibiti wa benki, ikiwa imetangazwa rasmi • Inakusaidia kujenga rekodi ya muamana na kubainisha uwezo wako wa kulipa • Kufikia ushauri wa kifedha na mipango mingine ya kifedha • Kasi (kutegemea mbinu husika) • Usiri (wakati mwingine nambari ya simu ndiyo kitu cha pekee unachohitaji kupokea pesa)	• Umbali, kwa watu wanaoishi mbali na miji au majiji • Hatari ya kuibiwa ukitoka kwenye tawi/kwa wakala • Saa zilizodhibitiwa za ufunguzi • Kiasi cha chini kinachohitajika wakati mwingine huwa cha juu sana • Gharama huenda ikawa juu • Kuhitajika kusubiri kwenye kaunta • Ni vigumu zaidi kutumia kwa watu ambao hawajui kusoma na kuandika • Wakati mwingine, kukosa pesa za kuwezesha utumaji wa kiasi kikubwa cha pesa.
ISIYO RASMI	• Gharama (kutegemea mbinu husika) • Ufikiaji • Upatikanaji wa ndani • Kasi (kutegemea mbinu husika) • Uaminifu (unaweza kutuma pesa kupitia kwa mwenye duka ambaye unamjua kwa muda mrefu) • Hakuna taratibu nyingi za kiutawala fomu za kujaza	• Hakuna huduma nyingine za kifedha ambazo utumaji wako wa pesa unaweza kukufanya ustahiki • Hatari ya mpokeaji kuhitajika kuchukua pesa katika mahali pasipo salama (duka, eneo la umma...): hatari ya wizi au kushambuliwa • Ukiukaji wa sheria wa kubeba kiasi kikubwa cha pesa ndani au nje ya nchi (hatari ya mtu anayebeba pesa hizo kukamatwa) • Hatari ya kuibiwa • Pesa ghushi

F



UZIFAHAMU TAASISI ZA KIFEDHA NA UZITUMIE KWA KUJIAMINI

F1. Taasisi ya kifedha ni huduma ya umma au ya kibinafsi ambayo inashughulikia uendeshaji wa kifedha kama vile uwekaji akiba, miamana na malipo.

- ☐ a. Ni kweli
- ☐ b. Si kweli

F2. Nimegundua kwamba kuna benki nyingi zaidi katika eneo hili:

- ☐ a. Nastahili kwenda kuomba taarifa; huenda wako na mipango mizuri ya kuweka akiba au muamana.
- ☐ b. Ina haja gani, benki hizi ziko na haja tu na matajiri na kampuni kubwa.
- ☐ c. Ningependa kwenda kuangalia lakini naogopa watanifukuza kwa kuwa sina pesa nyingi.

F3. Je, ni sentensi gani ambayo si kanuni ya ulinzi wa mteja ambayo taasisi za fedha zinatakiwa kuheshimu?

- ☐ a. Kuzuia kuingia katika madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa
- ☐ b. Kuwatendea wateja kwa njia ya haki na yenye heshima
- ☐ c. Uwazi
- ☐ d. Kuwapa wateja zawadi
- ☐ e. Utozaji ada wenye uwajibikaji
- ☐ f. Mbinu za kutatua malalamishi

Majibu: F1:a; F2:a; F3:d

1. ZIFAHAMU TAASISI ZA KIFEDHA

UJELEZI

Taasisi ya kifedha: Huduma ya umma au ya kibinafsi ambayo inashughulikia uendeshaji wa kifedha kama vile uwekaji akiba, miamana na malipo.

Benki ni mashirika yaliyoidhinishwa na Serikali kama taasisi za miamana kuendesha shughuli za benki: hasa kupokea fedha kutoka kwa umma, kuendesha shughuli za uwekaji akiba na utoaji mikopo pamoja na huduma za malipo. Benki zinaweza kumilikiwa na umma au kibinafsi, zinajikita katika amana au uwekezaji, kutengeneza bidhaa au kuwa kama vyama vya ushirika au vyama vya pamoja.

Taasisi ndogo za kifedha: ni taasisi ya kifedha inayojihusisha na huduma za benki kwa vikundi au watu wenye mapato ya chini. Taasisi ndogo za kifedha hutoa huduma za akaunti kwa akaunti zenye salio ndogo ambazo kwa kawaida hazingekubalika na benki za kawaida, na hutoa huduma za miamala kwa kiasi cha pesa ambacho huenda kikawa kidogo kuliko kiasi kinachoshughulikiwa kwa wastani na taasisi kubwa za kifedha.

Kampuni za fedha: ni mashirika ya kibiashara yaliyoidhinishwa na Serikali kuwa taasisi za kutoa muamana. Haziwezi kuchukua pesa kutoka kwa umma wala kutoa mipango ya kuweka akiba.

Teknolojia ya kifedha (Fintech): ni istilahi inayotumiwa kueleza teknolojia yoyote ambayo inawasilisha huduma za Kifedha kupitia kwa programu, kama vile huduma za benki mtandaoni, programu za malipo kupitia simu na *cyptocurrency*. Teknolojia ya kifedha kwa kawaida hutumiwa kama istilahi ambayo inajumuisha kampuni zinazotoa huduma za Kifedha kupitia kwa teknolojia.

VIDOKEZO

Ili kuchagua taasisi yako ya kifedha, unapaswa kuzingatia:

- Sifa za taasisi hiyo ya kifedha
- Sifa za mipango ambayo unahitaji kulingana na malengo yako ambayo taasisi hii inaweza kukupa: aina ya akaunti, mbinu za malipo, mipango ya kuweka akiba na miamana, mipango ya kutuma pesa...

KISAIDIZI CHA MAFUNZO

F.1.1 Maswali ya kuuliza taasisi ya kifedha

SIFA ZA KUZINGATIA KATIKA KUCHAGUA TAASISI YA KIFEDHA	MASWALI YA KUULIZA
Sifa za taasisi ya kifedha • Umbali kijiografia • Sifa na uaminifu wa taasisi hiyo ya kifedha • Utoaji na ubora wa huduma zisizo za kifedha (mafunzo ya kibiashara, elimu ya kifedha...) • Huduma za mbali (kukagua salio kupitia mtandao, taarifa za matumizi kupitia arafa, huduma za benki kupitia kwa simu...) na gharama • Ubora wa huduma na wafanyakazi (muda wa kusubiri, heshima kwa wateja, lugha zinazozungumzwa, kasi ya utoaji huduma...) • Ikiwa inahitajika, masharti ya kujiunga na taasisi hiyo (ada za usajili, marudio ya mikutano, uwezo wa wafanyakazi kufanya maamuzi...) • Uwazi kuhusu ada na sheria na masharti, ubora wa taarifa inayotolewa kwa wateja • Mipango iliyoundwa mahususi kwa vikundi maalum vya wateja (wanafunzi, wafanyakazi wa mshahara, waliostaafu...) • Kazi za hisani zilizofanywa (hazina ya msaada, ufadhili, wakfu...) • (Kwa watu wanaotuma au kupokea pesa kwa/kutoka kwa jamaa), uwepo wa taasisi hiyo katika eneo la jamaa zako na umbali kijiografia kutoka mahali wanapoishi	
Sifa za mipango ya taasisi ya kifedha (katika hali hii, uwekaji akiba) • Ufikivu wa akiba / uwezekano wa kutoa pesa • Wepesi wa kutumia • Masharti ya kufungua akaunti ya akiba • Usalama • Kiasi cha riba • Uwezekano wa kufikia mipango na huduma nyingine zinazotolewa na taasisi ya kifedha • Gharama ya kuweka akiba (ada, ada za adhabu) • Uwezo wa kupata pesa • Maadili ya bidhaa (ufadhili endelevu, kimazingira, Kiislamu...)	

KISAIDIZI CHA MAFUNZO

F.1.2 Maswali ya kuuliza taasisi ya kifedha (na majibu yanayopendekezwa)

SIFA ZA KUZINGATIA KATIKA KUCHAGUA TAASISI YA KIFEDHA	MASWALI YA KUULIZA
SIFA ZA TAASISI YA KIFEDHA	
Umbali kijiografia	• Je, kuna tawi la taasisi hiyo ya kifedha karibu nami (karibu na nyumba yangu, mahali pangu pa kazi au eneo lingine faafu Kama vile shule ya chekechea ya mtoto wangu)? • Niko na kadi ya malipo, je, kuna mashine ya ATM karibu (karibu na nyumba yangu, mahali pa kazi au eneo lingine faafu, kama vile ukumbi wa mazoezi...)?
Sifa na uaminifu wa taasisi hiyo (maswali ya kujiuliza au kuwauliza marafiki zako/familia)	• Je, taasisi hii ya kifedha iko na sifa nzuri? • Familia yangu inafikiri nini kuhusu taasisi hii? • Je, sifa ya taasisi hii ya kifedha inanitia moyo kujiamini? • Je, nimesikia matatizo yanayohusiana na taasisi hii katika vyombo vya habari au kupitia kwa marafiki na familia? • Je, najua mtu yeyote ambayo ana shida na taasisi hii ya kifedha? Ni shida ya aina gani? Ilitatuliwa vipi?
Utoaji na ubora wa huduma zisizo za kifedha (mafunzo ya kibiashara, elimu ya kifedha...)	• Je, mnatoa huduma za mafunzo kwa wateja/wanachama? Ikiwa ndiyo, yanahusu mada zipi? Nani anaweza kunufaika na mafunzo haya? Je, ni ya bila malipo? • Je, mnahusika katika shughuli za kusaidia au ufadhili? • Je, mnahusika katika shughuli za kusaidia kibinadamu? • Je, mko na washauri wa kuwasaidia wateja kusimamia akaunti na uwekezaji wao?
Huduma za mbali (kukagua salio kupitia mtandao, taarifa za matumizi kupitia arafa, huduma za benki kupitia kwa simu...) na gharama	• Je, mnatoa huduma za mbali? • Je, mteja anaweza kujua salio lake mtandaoni? • Ikiwa ndiyo, je, huduma hii inatolewa bila malipo wakati mtu anafungua akaunti? Ikiwa la, huduma hii itagharimu pesa ngapi? • Je, ninaweza kupata taarifa za malipo niliyofanya kupitia arafa?

SIFA ZA KUZINGATIA KATIKA KUCHAGUA TAASISI YA KIFEDHA	MASWALI YA KUULIZA
SIFA ZA TAASISI YA KIFEDHA	
Ubora wa huduma na wafanyakazi (muda wa kusubiri, heshima kwa wateja, lugha zinazozungumzwa, kasi ya utoaji huduma...)	• Je, benki hufunguliwa saa ngapi? • Je, inachukua muda gani kwa wastani kabla ya mteja kushughulikiwa na mfanyakazi? • Je, mko na mtandao wa mashine za ATM kote nchini? • Je, nitatozwa ada ikiwa nitatoa pesa kutoka kwa mashine nyingine ya ATM (katika eneo lingine, ughaibuni, au ya benki nyingine)?
IAMULIWE WAKATI WA ZIARA Ikiwa inahusika (vyama vya pamoja), masharti ya uanachama	• Je, kuna masharti ya kuwa mwanachama wa taasisi yenu ya kifedha? Masharti hayo ni yapi? • Je, inagharimu pesa ngapi kwa usajili? Inalipiwa kwa wiki, kwa mwezi, kwa mwaka...? • Je, mikutano ya wanachama hufanyika mara ngapi? • Je, ni lazima mtu ahudhurie mikutano hii? Ikiwa ndiyo, kuna adhabu gani ikiwa mtu atakosa kuhudhuria? • Je, wanachama wako na mamlaka gani ya kufanya uamuzi?
Uwazi kuhusu ada na sheria na masharti, ubora wa taarifa inayotolewa kwa wateja (maswali ya kujiuliza)	• Je, kuna ada na masharti yanayoonyeshwa katika majengo ya taasisi ya kifedha? • Je, taasisi inatoa brosha za maelezo au mbinu nyingine ya taarifa (tovuti...)? Ikiwa ndiyo, je, nilipata taarifa zote zilizohitaji kwa kusoma brosha/kurejelea taarifa hiyo? • Je, hati zilizotolewa ni rahisi kuelewa? • Je, mtu anafungua au kufunga akaunti vipi? Yatagharimu kiasi gani? •
Mipango iliyoundwa mahususi kwa vikundi maalum vya wateja (wanafunzi, wafanyakazi wa mshahara, waliostaafu...)	• Je, mko na mipango yoyote au huduma za kifedha zilizoundwa mahususi kwa watu kama mimi? (Vijana, wenye duka, wafanyakazi, wanawake, wafanyabiashara...)
Kazi za hisani zilizofanywa (hazina ya msaada, ufadhili...)	• Je, taasisi yako inahusika katika kazi za hisani? Ikiwa ndiyo, ni kama zipi? Nani Wananufaika (watoto walio na ulemavu, wagonjwa...)?
Uwepo wa taasisi hiyo ughaibuni au katika eneo na umbali wa kijiografia kutoka mahali anapoishi jamaa anayetuma au kupokea pesa	• Je, kuna tawi la taasisi ya kifedha karibu na mahali ambapo familia yangu inaishi (nyumbani, mahali pa kazi au eneo lingine faafu), kwa kuwa nitakuwa nikituma na kupokea pesa kwao/kutoka kwao?

SIFA ZA KUZINGATIA KATIKA KUCHAGUA TAASISI YA KIFEDHA	MASWALI YA KUULIZA
SIFA ZA MIPANGO YA TAASISI YA KIFEDHA (KATIKA HALI HII, UWEKAJI AKIBA)	
Ufikivu wa akiba / uwezekano wa kutoa pesa	Ninaweza kutoa pesa mara ngapi? • Je, kuna kiasi cha chini kwa kila utoaji? • Je, nitalipa ada za adhabu ikiwa nitatoa pesa kutoka kwa akaunti hii ya akiba?
Wepesi wa kutumia	• Je, wateja hupokea taarifa kuhusu akaunti yao ya akiba? Mara ngapi? • Je, mnatoa huduma za simu na/au za benki mtandaoni?
Masharti ya kufungua akaunti ya akiba Usalama	• Nahitaji kiasi gani cha chini zaidi kufungua akaunti ya akiba? • Ninahitajika kuwaonyesha hati gani? • Kuna bima au dhamana gani ya kulinda fedha za wateja?
Kiasi cha riba	• Je, akaunti hii ya akiba inazaa kiwango gani cha riba? • Kiwango hiki kinalingana vipi na kile cha taasisi nyingine? • Je, riba inalipwa mara ngapi? • Je, riba inahesabiwa vipi? Je, kiasi cha riba ni cha kudumu au kinabadilika?
Uwezekano wa kufikia mipango na huduma nyingine zinazotolewa na taasisi ya kifedha	• Kwa kutumia mpango wa kifedha, je nitaweza kufikia mipango au huduma zingine? Ikiwa ndiyo, ni kama zipi? Kwa kiwango kizuri zaidi?
Gharama ya kuweka akiba (ada, ada za adhabu)	• Itagharimu nini? (Mnatoza ada gani kwa utumaji pesa, utoaji wa pesa kupitia mashine za ATM) • Je, mnatoza ada gani ya usimamizi kwa akaunti ya akiba?
Uwezo wa kupata pesa	• Je, ni rahisi kutoa pesa? Utaratibu ni upi? • Je, ninaweza kutoa pesa zote ikiwa ninataka kufanya hivyo? • Je, kuna ada za kulipwa ikiwa pesa zitatolewa kabla ya tarehe fulani?
Maadili ya bidhaa (ufadhili endelevu, kimazingira, Kiislamu...)	• Je, mpango wa kifedha unatimiza viwango vya kimaadili? Viwango gani? • Je, mpango umewekewa nembo ya kuthibitisha uzingativu wa viwango hivi?

ZAMU YAKO!

Kwa mujibu wa malengo yangu, hali yangu ya kibinafsi, na mahitaji yangu ya kifedha, nachagua taasisi ya kifedha yenye sifa zifuatazo:

Mfano: kufikia huduma kupitia mtandaoni

1. . .. .
2. . .. .
3. . .. .

UJUMBE MUHIMU

- Ili kuchagua taasisi ya kifedha, unahitaji kukagua sifa na mipango yake na kuchagua ile inayofaa mahitaji yako zaidi.
- Unaweza kupata taarifa kwenye brosha za taasisi za kifedha na unaweza pia kuwauliza wafanyakazi wa taasisi hiyo maswali.
- Unapochagua mpango wa kuweka akiba au muamana, zingatia kwamba viwango vya riba ni kipengele kimoja tu cha kuzingatiwa miongoni mwa vingine vingi.

MUHTASARI

2. TUMIA TAASISI ZA KIFEDHA KWA KUJIAMINI

Uchunguzi Kifani N°1

MUTUA NA RAFIKI YAKE OPIYO WANAZUNGUMZA KUHUSU TAASISI ZA KIFEDHA

Mutua anakunywa kahawa na rafiki yake Opiyo. Opiyo alikuwa na tajriba mbaya na benki fulani: Alienda kuomba taarifa na akashawishia na mfanyakazi kufungua akaunti na baadaye akagundua kuwa akaunti hiyo ilikuwa na ada za juu. Pia aligundua kwamba alikuwa analipia huduma ambazo hakuwa anatumia. Anajuta kufanya uamuzi wa haraka. Mutua anaeleza kwamba kufikia miezi michache iliyopita, alikuwa na pochi la simu, lakini baada ya kupata mafunzo ya elimu ya kifedha alitembelea benki mbalimbali na kuuliza taarifa za kufungua akaunti ya akiba ya kawaida. Ilikuwa rahisi kusema la kwa wafanyakazi, lakini aliweza kupata taarifa nyingi kutokana na majadiliano nao. Mwishowe, aliamua kufungua akaunti na mojawapo wa benki ambayo alikuwa ametembelea na ikampa akaunti ya msingi isiyotoza ada na ambayo haihitaji salio la msingi. Ataenda kwenye benki hiyo wiki ijayo na anamkaribisha Opiyo kuandamana naye, ili apate taarifa zaidi. Opiyo anaamua kupata taarifa kuhusu jinsi anavyoweza kufunga akaunti yake, na kuzunguka kama alivyofanya Mutua ili apate akaunti ambayo ni faafu zaidi kwa mahitaji yake.

MASWALI

Je, kwa nini Opiyo hana imani na taasisi za kifedha?

Lazima ujue kwamba kama mteja wa taasisi ya kifedha, una wajibu, lakini pia una haki zako!

Hebu tujifunze kuhusu haki hizi!

MUHIMU: Ikiwa umewahi kuwa na tajriba mbaya na taasisi za kifedha, kuna uwezekano kwamba kuwaamini na pesa zako kunaweza kukusababishia wasiwasi au mfadhaiko. Jifahamishe kabla ya kufanya uamuzi. Kumbuka: una haki.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO F.2.1

Kadi za Maelezo

KADI ZA MAELEZO **N ° 1**

Nahitaji kujazwa ikiwa unataka kufungua akaunti ya benki. Ukishanijaza, lazima uwasilishe hati zako za utambulisho kwa mhudumu ili kukamilisha mchakato. Ukishanijaza na kuwasilisha hati muhimu, unaweza kwenda kwenye kaunta na kuweka pesa katika akaunti yako.

KADI ZA MAELEZO **N ° 2**

Naketi kwenye dawati karibu na kiingilio cha duka la wakala. Kazi yangu ni kuwasaidia wateja kufungua akaunti za benki. Ninaweza kukupa fomu ya kufungua akaunti ya benki. Pia ninaweza kukusaidia kuamua ni akaunti gani ya benki inayotimiza mahitaji yako vyema zaidi. Niulize maswali kuhusu mipango tunayotoa na fomu unayohitajika kujaza. Niulize ni hati gani unahitaji kufungua akaunti. Usiniombe kuchukua pesa au kukupa pesa.

KADI ZA MAELEZO **N ° 3**

Nawasimamia wafanyakazi wote na kuhakikisha kwamba wanafanya kazi vizuri. Pamoja na wafanyakazi unaowaona, nasimamia wale ambao wanafanya kazi bila kuonekana wakiwa katika ofisi zao, kusimamia akaunti za watu na kufanya mambo mengine. Njoo uone kama una tatizo ambalo wafanyakazi hao wengine hawakuweza kusuluhisha. Usije kuniona ili kufungua akaunti.

KADI ZA MAELEZO **N ° 4**

Kazi yangu ni kusika pesa na kurekodi miamala. Nachukua pesa ambazo wateja wanaweka kwenye akaunti zao na kuwakabidhi pesa wanapotoa pesa katika akaunti zao. Wateja lazima wanipe uthibitisho wa utambulisho wao na kujaza fomu kwa njia sahihi kabla niweze kuwahudumia. Unaweza kuniuliza kuhusu salio kwenye akaunti yako au iwapo malipo yamefika. Usiniombe kukufungulia akaunti ya benki.

KADI ZA MAELEZO **N ° 5**

Kazi yangu ni kulinda benki, wafanyakazi wa benki na wateja wetu. Ili kufanya hivyo, nahitaji kuwa mwangalifu kwa kila kitu kinachoendelea katika benki. Usiniulize taarifa kuhusu jinsi ya kufungua akaunti au kujaza fomu.

KADI ZA MAELEZO **N ° 6**

Ninaonyesha taarifa kuhusu mipango tofauti inayotolewa na benki na gharama ya kila mpango.

KADI ZA MAELEZO N 7

Ninashikilia fomu zote zinazohitajika kwa ajili ya kufanya miamala. Utahitaji fomu zangu ikiwa unataka kufanya shughuli za benki na wafanyakazi kwenye kaunta.

KADI ZA MAELEZO N ° 8

Utahitajika kunijaza kwa kina na kutia sahihi ikiwa unataka kutoa pesa kwenye akaunti yako.

KADI ZA MAELEZO N ° 9

Unaweza kunitumia kumlipa mtu bila haja ya pesa taslimu (k.m. noti au mapeni). Unapoijaza na kutia sahihi, unaipa benki ruhusa ya kumlipa mtu ambaye jina lake limeandikwa juu yangu. Benki itamlipa mtu huyo kwa pesa zinazotolewa kwenye akaunti yako.

KADI ZA MAELEZO N ° 1 1

Utahitajika kunijaza kwa kina, ikiwemo nambari ya akaunti, ikiwa unataka kuweka pesa katika akaunti yako.

U **kufikia mwishoni mwa somo hili, utapata majibu sahihi katika Majibu kwa mazoezi.**

UJUMBE MUHIMU

- Ili kuchagua taasisi ya kifedha, unahitaji kukagua sifa na mipango yake na kuchagua ile inayofaa mahitaji yako zaidi.
- Ili kukagua sifa na mipango ya taasisi ya kifedha, ni muhimu kusoma brosha, vipeperushi pamoja na kuuliza maswali sahihi kwa wafanyakazi: kuwa huru, ni kazi yao kujibu maswali yako!
- Kuingia katika benki au taasisi nyingine ya kifedha haimaanishi umejitolea kufungua akaunti; unaweza kuanza kwa kukusanya taarifa.
- Kila mtu anaweza, kinadharia, kufikia huduma kutoka kwa taasisi za kifedha (ikiwa unaweza kutoa hati zinazohitajika!): unahitaji kupata taasisi ambayo inatimiza mahitaji yake vyema zaidi.
- Kama mteja wa taasisi ya kifedha, una haki!

Sasa tutafanya mazoezi ya kujaza fomu ya kufungua akaunti ya benki. Tutatumia fomu ya maombi ya jumla.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO F.2.2

Fomu ya maombi ya kufungua akaunti

YOURBANK

KISANDUKU KIMEHIFADHIWA

MAOMBI YA KUFUNGUA AKAUNTI

MWENYE AKAUNTI 1	MWENYE AKAUNTI2
HALI YA KIBINAFSI	**HALI YA KIBINAFSI**
Hali ya ndoa: ☐ Bw. ☐ Bi. ☐ Bi.	Hali ya ndoa:
Jina la Ukoo:	Jina la Ukoo:
Majina:	Majina:
Anwani ya makazi: Msimbo wa Posta:	Anwani ya makazi: Msimbo wa Posta:
Mji:	Mji:
Nchi:	Nchi:
Hali ya Familia: ☐ Katika ndoa ☐ Nimetengana ☐ Talaka ☐ Mjane ☐ sijaoa/sijaolewa	Hali ya Familia: Katika ☐ ndoa Talaka ☐ Sijaoa/Sijaolewa ☐
Jina asili la ukoo:	Jina asili la ukoo:
Tarehe na mahali pa kuzaliwa:	Tarehe na mahali pa kuzaliwa:
Uraia:	Uraia:
Simu (nyumbani):	Simu (nyumbani):
Simu (rununu):	Simu (rununu):
Barua pepe:	Barua pepe:
HALI YA KIKAZI	**HALI YA KIKAZI**
Mapato halisi kwa mwezi:	Mapato halisi kwa mwezi:
☐ Nafanya kazi ☐ Nasaka kazi ☐ Mwanafunzi ☐ Nimestaafu	☐ Nafanya kazi ☐ Nasaka kazi ☐ Mwanafunzi ☐ Nimestaafu

AKAUNTI

☐ Akaunti ya matumzi ya mtu binafsi ☐ Akaunti ya matumzi ya Ushirika ☐ Akaunti ya akiba

KADI NA HUDUMA ZA BENKI

☐ Kadi ya ATM Kadi ya
☐ malipo Kadi ya
☐ mkopo

☐ Huduma za benki mtandaoni
☐ Bima kwa mbinu ya malipo

SAHIHI

MWENYE AKAUNTI 1	MWENYE AKAUNTI 2	MENEJA WA BENKI

Tarehe:

KISAIDIZI CHA MAFUNZO F.2.3

Kutumia mashine ya ATM kutoa pesa

Sasa tutafanya mazoezi ya kutumia mashine ya ATM kuonyesha utoaji wa pesa kwenye akaunti ya akiba

HATUA YA 1: TIA KADI KWENYE ATM

Tia ndani kadi yako ya ATM kwenye mashine ya ATM (huenda ukaona mpenyo wenye rangi ya kijani au mpenyo mwingine).

HATUA YA 2: WEKA NAMBARI YA SIRI YA ATM YENYE NAMBARI NNE

Kwa kutumia kicharazio weka nambari ya siri yenye nambari nne. Lakini kumbuka kila wakati kwamba hakuna mtu anayeweza kuona nywila yako unapoitia na pia usishiriki nywila hii na mtu yeyote. Ukitia nywila isiyo sahihi zaidi ya mara tatu, kadi yako ya ATM inaweza kuzuiwa.

HATUA YA 3: CHAGUA MUAMALA

Katika sehemu hii, unaweza kuona chaguzi kwenye skrini kama vile kutoa pesa, kutuma pesa, kukagua salio n.k. Katika hali hii, unahitajika kuchagua kutoa pesa.

HATUA YA 4: CHAGUA AKAUNTI YAKO



Ikiwa kadi yako ya ATM imeunganishwa na akaunti tofauti za benki, utahitajika kuchagua ni akaunti gani ya benki unataka kutoa pesa.

HATUA YA 5: WEKA KIASI



Katika sehemu hii, unahitajika kutia kiasi unachotaka kutoa kisha ubonyeze ingiza.

Lakini hakikisha kwamba kiasi unachotoa hakizidi salio katika akaunti yako vinginevyo muamala hautafaulu.

HATUA YA 6: CHUKUA PESA

Katika sehemu hii, utachukua pesa zako kutoka kwa mpenyo wa chini wa mashine hiyo.

HATUA YA 7: CHAGUA MUAMALA MWINGINE AU UTAMATISHE SHUGHULI

Wakati huu unaweza kuchagua iwapo unataka kufanya muamala mwingine au kutamatisha shughuli. Baada ya kubonyeza kamilisha shughuli yako, hakikisha unachukua kadi yako ya ATM.

Lazima ujue kwamba kama mteja wa taasisi ya kifedha, una wajibu, lakini pia una haki zako! Hebu tujifunze kuhusu haki hizi!

MUHTASARI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO F.2.4

Kadi za Maelezo - Kanuni za ulinzi wa mteja

KADI ZA MAELEZO N ° 1

Nina duka ndogo la kuuza bidhaa za kuagiza kutoka nje.
Nimepata mkopo wa biashara kutoka kwa taasisi ndogo ya mikopo iliyo karibu. Kiasi nilichopewa ni kiasi kamili ambacho nilihitaji. Katika muda wa miezi mitatu, nitakuwa ninauza bidhaa nyingi kwa mteja muhimu na nitakua na kiasi kikubwa cha pesa.
Hata hivyo, sasa nahitajika kulipa mkopo kwa taasisi ndogo ya mikopo kila mwezi na sina mapato kwa kusasa kutokana na biashara yangu kuniwezesha kufanya malipo hayo. Sasa naona kwamba mkopo huo haukuwa faafu kwa mahitaji yangu.

Je, ni kawaida?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA MAELEZO N ° 2

Tayari nimechukua mikopo miwili kutoka benki: mmoja wa kununua nyumba, na mwingine wa kulipia gharama za hafla ya kidini mwaka uliopita.

Sasa ningependa kununua pikipiki ndogo ili niweze kusafiri kwa urahisi zaidi. Benki yangu inakataa kunipa mkopo wa tatu.

Je, ni kawaida?
Je, ninaweza kufanya nini kuhusu hali hii?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA MAELEZO N ° 3

Mimi ni mteja katika taasisi ya kifedha.

Nimejaribu kuelewa sheria na masharti na ada zinazohusika na mpango wa kuweka akiba, lakini brosha waliyonipa imeandikwa kwa herufi ndogo sana na sielewi istilahi zote zilizotumika.

Napaswa kufanya nini?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA MAELEZO N ° 4

Niko na akaunti ya matumizi na akaunti ya akiba katika taasisi ya kifedha.
Sifurahi kwa kuwa nahitajika kulipa ada nyingi za usimamizi wa akaunti yangu ya matumizi, na akaunti yangu ya akiba inalipa kiwango cha chini sana cha riba.

Nahisi kwamba hii si haki.

Je, ni kawaida?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA MAELEZO N ° 5

Niko na madeni mengi na ninashindwa kufanya malipo ya mkopo kwa sababu nimepoteza kazi.

Nahofia kile benki inaweza kufanya nikishindwa kufanya malipo hayo.

Je, wanaweza kuja nyumbani kwangu na kuchukua mali yangu au ya familia yangu?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA MAELEZO N ° 6

Ninatofautiana vikali na benki yangu kuhusu jambo ambalo limetendeka.

Naweza kumwendea nani? Je, kuna yeyote katika benki ambaye anaweza kunisaidia?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA MAELEZO N ° 7

Mfanyakazi wa benki ambaye anashughulikia akaunti yangu ya matumizi ya kibinafsi anajua kwamba nilipokea kiasi kikubwa cha pesa mwezi uliopita.

Je, anaweza kujadili taarifa hii na mtu wa familia yangu bila ruhusa yangu?

ELIMU YA KIFEDHA

Usanifu na utoaji wa mpango unaofaa

Taasisi za kifedha zinapaswa kuhakikisha kwamba mipango yake na mifumo ya usambazaji imeundwa kwa njia ambayo haitadhuru maslahi ya wateja wake. Zitahitajika kuzingatia sifa za wateja wake wakati wa kusanifu mipango yake na mbinu za usambazaji.

Kuzuia kuingia katika madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa

Ndiyo, ni kawaida kabisa Hakuna kitu kinachoitwa haki ya kuomba pesa. Kwa kuwazuia wateja wake kuingia katika madeni mengi, benki inakulinda wewe. Kanuni hii inahitaji taasisi za kifedha kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba mikopo inatolewa tu kwa wakopaji ambao wanaweza kuthibitisha kwamba wanaweza kulipa, na kwamba mikopo haitawatia wakopaji katika hatari ya kuwa na madeni mengi kuliko wanavyoweza kulipa.

Uwazi

Unastahili kuuliza wafanyakazi wa benki taarifa zaidi. Hii ni haki yako, na taasisi za kifedha zinastahili kuzingatia kanuni ya kutoa mfumo wazi na wenye uwajibikaji wa kutoza ada. Yaani, ada na masharti yanayohusiana na mipango ya kifedha lazima yawe yameandikwa kwa uwazi na kuelezwa katika lugha ambayo ni rahisi kwa wateja kuelewa.

Utozaji ada wenye uwajibikaji

Muulize mshauri wako katika benki kwa taarifa zaidi. Taasisi za kifedha lazima zihakikishe kwamba ada zake, masharti, na taratibu ni nafuu kwa wateja, huku zikiwawezesha kupata faida ya kutosha kama biashara. Taasisi za kifedha zinapaswa kufanya kila juhudi kuhakikisha kwamba pesa zilizowekwa kwao zinazaa kiwango cha riba cha haki

Kuwatendea wateja kwa njia ya haki na yenye heshima

Taasisi za kifedha zina wajibu wa kuwatendea wateja kwa haki na heshima. Lazima zisiendeleze ubaguzi wa aina yoyote. Lazima zihakikishe kwamba mikakati ya kutosha imewekwa kutambua na kurekebisha matukio ya ufisadi na mienendo yoyote ya vurugu au udhalilishaji kwa mawakala na wafanyakazi wake, hasa wakati wa kufuatilia mikopo ambayo haijalipwa.

Mbinu za kutatua malalamishi

Taasisi za kifedha lazima ziwe na mikakati ya kuingilia kwa wakati unaofaa ikiwa kutatokea tatizo na malalamishi kutoka kwa wateja wake. Lazima zitumie mikakati hii kusuluhisha matatizo ya kibinafsi na kuboresha mipango na huduma zake.

Faragha ya data ya wateja

Usiri kuhusu data ya kibinafsi ya mteja lazima uheshimiwe kwa mujibu wa sheria na masharti ya mifumo ya sheria katika nchi husika. Data kama hivyo huenda ikatumiwa tu kwa azma zilizobainishwa wakati ilipotolewa na kama inavyoruhusiwa kisheria, isipokuwa kama mteja ataeleza vinginevyo.



KISAIDIZI CHA MAFUNZO F.2.5

Kadi zenye hali za mahitaji ya mipango wa kuweka akiba

KADI ZA HALI

HALI YA 1

Gloria na Gitau wamehudhuria kipindi cha elimu ya kifedha iliyopangwa na shirika la kujitolea kutoka mtaani kwao. Mada ilikua “Kuweka akiba kwa ajili ya siku yenye dharura”

Wamekuwa wakizungumza kuhusu kutenga pesa fulani kila mwezi, hata kama ni kiasi kidogo, ili kuanza kujenga hazina yao ya dharura.

Gloria na Gitau wanataka kufungua akaunti ya akiba ya kawaida.

› Ni maswali gani unapaswa kuuliza taasisi za kifedha ili kupata ile ambayo ina mpango unaofaa zaidi kwa Gloria?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA HALI

HALI YA 2

Otieno na Mwende wamekuwa wakifikiria kuhusu maisha ya baadaye ya watoto wao. Jabali anataka kufanya nao kazi katika duka la kuoka, lakini Kariuki na Adhra wanataka kwenda chuoni.

Wanaamini wakati umefika wa kuanza kuweka akiba polepole ya kuwawezesha kwenda chuoni. Wameweza kuweka akiba fulani, na wanataka wapate riba fulani kwenye pesa yao kwa muda mrefu hata kama hawataweza kutoa pesa hizo kwa muda mrefu.

Mwende alisikia kwamba akaunti ya amana ya muda inaweza kusaidia kuweka akiba kwa ajili ya lengo hili.

›› Ni maswali gani unapaswa kuuliza taasisi za kupata ile yenye mpango faafu zaidi kwa Otieno na Mwende?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA HALI

HALI YA 3

Mutua ameamua kufungua akaunti na mojawapo wa benki ambayo alikuwa ametembelea na ikampa akaunti ya msingi isiyotoza ada na ambayo haihitaji salio la msingi.

Ni muhimu kwake kwamba akaunti hii imruhusu kutoa pesa wakati anazihitaji, kwa kuwa anatazamia kuhamia Kuwait hivi karibuni.

› Ni maswali gani unapaswa kuuliza taasisi za kifedha ili kupata ile ambayo ina mpango unaofaa zaidi kwa Mutua?

ELIMU YA KIFEDHA

KADI ZA HALI

HALI YA 4

Wangari anataka kuwa na uhakika kwamba wazazi wake wataweza kutimiza malengo yao wakati hatakuwepo. Mojawapo ya malengo ya familia ni kuboresha nyumba yao. Ili afanye hivi, anataka kuweka akiba ya kiasi fulani cha pesa kila mwezi kwa mwaka mmoja. Hataki kushawishika kutumia pesa hizo na anawaza kuhusu akaunti ya akiba ambayo itamwezesha kufikia malengo ya familia.
Babake hafikiri wanastahili kufungua akaunti ya akiba kwenye taasisi ya kifedha.
Ingawa hivyo, baada ya kujadili suala hili mara kadhaa na wazazi wake, Wangari ameamua kufungua akaunti ya akiba ya kimkataba ambayo itawawezesha kuweka amana iliyobainishwa kila mwezi ili kuweka akiba kwa muda maalum.

›› Ni maswali gani ambayo unapaswa kuuliza Ili upate ile yenye mpango faafu zaidi kwa Wangari na wazazi wake?

ELIMU YA KIFEDHA

KISAIDIZI CHA MAFUNZO F.2.6

Fomu ya kuripoti unapotembelea taasisi ya kifedha

1 / 3

TAASISI ULIYOTEMBELEA: WADHIFA WA MTU ULIYOFANYA MAHOJIANO NAYE:

Jaza jedwali lifuatalo kwa kila mpango unaotolewa na taasisi ya kifedha uliyotembelea.

MIPANGO:

SIFA ZA KUZINGATIA KATIKA KUCHAGUA TAASISI YA KIFEDHA	MAJIBU ULIYOPOKEA WAKATI WA ZIARA HIYO
SIFA ZA TAASISI YA KIFEDHA	
Umbali kijiografia	
Sifa na uaminifu wa taasisi hiyo ya kifedha	
Utoaji na ubora wa huduma zisizo za kifedha (mafunzo ya kibiashara, elimu ya kifedha...)	
Huduma za mbali (kukagua salio kupitia mtandao, taarifa za matumizi kupitia arafa, huduma za benki kupitia kwa simu...) na gharama	
Ubora wa huduma na wafanyakazi (muda wa kusubiri, heshima kwa wateja, lugha zinazozungumzwa, kasi ya utoaji huduma...)	
Ikiwa inafaa, masharti ya kujiunga (ada za usajili, marudio ya mikutano, uwezo wa wafanyakazi kufanya maamuzi...)	
Uwazi kuhusu ada na sheria na masharti, ubora wa taarifa inayotolewa kwa wateja	

ELIMU YA KIFEDHA

SIFA ZA KUZINGATIA KATIKA KUCHAGUA TAASISI YA KIFEDHA	MAJIBU ULIYOPOKEA WAKATI WA ZIARA HIYO
SIFA ZA TAASISI YA KIFEDHA	
Mipango iliyoundwa mahususi kwa vikundi maalum vya wateja (wanafunzi, wafanyakazi wa mshahara, waliostaafu...)	
Kazi za hisani zilizofanywa (hazina ya msaada, ufadhili...)	
Uwepo wa taasisi hiyo ughaibuni au katika eneo na umbali wa kijiografia kutoka mahali anapoishi jamaa anayetuma au kupokea pesa	
SIFA ZA MIPANGO YA TAASISI YA KIFEDHA (KATIKA HALI HII, UWEKAJI AKIBA)	
Ufikivu wa akiba / uwezekano wa kutoa pesa	
Wepesi wa kutumia	
Masharti ya kufungua akaunti ya akiba	
Usalama	

ELIMU YA KIFEDHA

SIFA ZA KUZINGATIA KATIKA KUCHAGUA TAASISI YA KIFEDHA	MAJIBU ULIYOPOKEA WAKATI WA ZIARA
SIFA ZA MIPANGO TYA TAASISI YA KIFEDHA (KATIKA HALI HII, UWEKAJI AKIBA)	
Kiasi cha	
Uwezekano wa kufikia mipango na huduma nyingine zinazotolewa na taasisi ya kifedha	
Gharama ya kuweka akiba (ada, ada za adhabu)	
Uwezo Maadili ya bidhaa (ufadhili endelevu, kimazingira, Kiislamu...)	

ELIMU YA KIFEDHA

MUHTASARI

MAJIBU KWA MAZOEZI

KISAIDIZI CHA MAFUNZO F.2.1

Kadi za Maelezo

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°1

Fomu ya maombi ya kufungua akaunti

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°2

Wakala wa huduma kwa wateja

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°3

Meneja wa benki

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°4

Karani wa benki

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°5

Mlinzi

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°6

Ubao wa maonyesho

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°7

Rafu za maonyesho ya hati

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°8

Karatasi ya kutoa pesa

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°9

Hundi

MAJIBU KADI ZA MAELEZO N°10

Karatasi ya kuweka pesa

MAJIBU KWA MAZOEZI

Kisaidizi cha mafunzo F.2.4: Kadi za Maelezo - Kanuni za ulinzi wa mteja

KADI ZA MAELEZO No 1

Nina duka ndogo la kuuza bidhaa za kuagiza kutoka nje.
Nimepata mkopo wa biashara na taasisi ndogo ya mikopo iliyo karibu. Kiasi nilichopewa ni kiasi kamili ambacho nilihitaji. Katika muda wa miezi mitatu, nitakuwa ninauza bidhaa nyingi kwa mteja muhimu na nitakua na kiasi kikubwa cha pesa. Hata hivyo, sasa nahitajika kulipa mkopo kwa taasisi ndogo ya mikopo kila mwezi na sina mapato kwa kusasa kutokana na biashara yangu kuniwezesha kufanya malipo hayo.

Sasa naona kwamba mkopo huo haukuwa faafu kwa mahitaji yangu.

Je, ni kawaida?

ELIMU YA KIFEDHA

KANUNI ZA ULINZI WA MTEJA ZILIZOTUMIKA

Usanifu na utoaji wa mpango unaofaa

Taasisi za kifedha zinapaswa kuhakikisha kwamba mipango yake na mifumo ya usambazaji imeundwa kwa njia ambayo haitadhuru maslahi ya wateja wake. Zitahitajika kuzingatia sifa za wateja wake wakati wa kusanifu mipango yake na mbinu za usambazaji.

KADI ZA MAELEZO N O 2

Tayari nimechukua mikopo miwili kutoka benki: mmoja wa kununua nyumba, na mwingine wa kulipia gharama za shughuli ya kidini mwaka uliopita.

Sasa ningependa kununua pikipiki ndogo ili niweze kusafiri kwa urahisi zaidi.

Benki yangu inakataa kunipa mkopo wa tatu. Je, ni kawaida? Je, ninaweza kufanya nini kuhusu hali hii?

Je, ninaweza kufanya nini kuhusu hali hii?

ELIMU YA KIFEDHA

KANUNI ZA ULINZI WA MTEJA ZILIZOTUMIKA

Kuzuia kuingia katika madeni mengi kuliko unavyoweza kulipa

Ndiyo, ni kawaida kabisa Hakuna kitu kinachoitwa haki ya kuomba pesa. Kwa kuwazuia wateja wake kuingia katika madeni mengi, benki inakulinda wewe. Kanuni hii inahitaji taasisi za kifedha kuchukua hatua za kuhakikisha kwamba mikopo inatolewa tu kwa wakopaji ambao wanaweza kuthibitisha kwamba wanaweza kulipa, na kwamba mikopo haitawatia wakopaji katika hatari ya kuwa na madeni mengi kuliko wanavyoweza kulipa.

KADI ZA MAELEZO N O 3

Mimi ni mteja katika taasisi ya kifedha.

Nimejaribu kuelewa sheria na masharti na ada zinazohusika na mpango wa kuweka akiba, lakini brosha waliyonipa imeandikwa kwa herufi ndogo sana na sielewi istilahi zote zilizotumika.

Napaswa kufanya nini?

ELIMU YA KIFEDHA

KANUNI ZA ULINZI WA MTEJA ZILIZOTUMIKA

Uwazi

Unastahili kuuliza wafanyakazi wa benki taarifa zaidi. Hii ni haki yako, na taasisi za kifedha zinastahili kuzingatia kanuni ya kutoa mfumo wazi na wenye uwajibikaji wa kutoza ada. Yaani, ada na masharti yanayohusiana na mipango ya kifedha lazima yawe yameandikwa kwa uwazi na kuelezwa katika lugha ambayo ni rahisi kwa wateja kuelewa.

KADI ZA MAELEZO N o 4

Niko na akaunti ya matumizi na akaunti ya akiba katika taasisi ya kifedha.

Sifurahi kwa kuwa nahitajika kulipa ada nyingi za usimamizi wa akaunti yangu ya matumizi, na akaunti yangu ya akiba inalipa kiwango cha chini sana cha riba.

Nahisi kwamba hii si haki. Je, ni kawaida?

ELIMU YA KIFEDHA

KANUNI ZA ULINZI WA MTEJA ZILIZOTUMIKA

Utozaji ada wenye uwajibikaji

Muulize mshauri wako katika benki kwa taarifa zaidi. Taasisi za kifedha sharti zihakikishe kwamba ada zake, masharti na taratibu zao ni nafuu kwa wateja, huku zikiwawezesha kupata faida ya kutosha kama biashara. Taasisi za kifedha zinapaswa kufanya kila juhudi kuhakikisha

KADI ZA MAELEZO N O 5

Niko na madeni mengi na ninashindwa kufanya malipo ya mkopo kwa sababu nimepoteza kazi.

Nahofia kile benki inaweza kufanya nikishindwa kufanya malipo hayo.

Je, wanaweza kuja nyumbani kwangu na kuchukua mali yangu au ya familia yangu?

ELIMU YA KIFEDHA

KANUNI ZA ULINZI WA MTEJA ZILIZOTUMIKA

Kuwatendea wateja kwa njia ya haki na yenye heshima

Taasisi za kifedha zina wajibu wa kuwatendea wateja kwa haki na heshima. Lazima zisiendeleze ubaguzi wa aina yoyote. Lazima zihakikishe kwamba mikakati ya kutosha imewekwa kutambua na kurekebisha matukio ya ufisani na mienendo yoyote ya vurugu au udhalilishaji kwa mawakala na wafanyakazi wake, hasa wakati wa kufuatilia mikopo ambayo haijalipwa.

KADI ZA MAELEZO N o 6

Ninatofautiana vikali na benki yangu kuhusu jambo ambalo limetendeka. Nafaa kumwendea

Je, kuna mtu katika benki ambaye anaweza kunisaidia?

ELIMU YA KIFEDHA

KANUNI ZA ULINZI WA MTEJA ZILIZOTUMIKA

Mbinu za kutatua malalamishi

Taasisi za kifedha lazima ziwe na mikakati ya kuingilia kwa wakati unaofaa ikiwa kutatokea tatizo na malalamishi kutoka kwa wateja wake. Lazima zitumie mikakati hii kusuluhisha matatizo ya kibinafsi na kuboresha mipango na huduma zake.

KADI ZA MAELEZO No 7

Mfanyakazi wa benki ambaye anashughulikia akaunti yangu ya matumizi ya kibinafsi anajuwa kwamba nilipokea kiasi kikubwa cha pesa mwezi uliopita.

Je, anaweza kujadili ukweli huu na mtu wa familia yangu bila ruhusa yangu?

ELIMU YA KIFEDHA

KANUNI ZA ULINZI WA MTEJA ZILIZOTUMIKA

Faragha ya data ya wateja

Usiri kuhusu data ya kibinafsi ya mteja lazima uheshimiwe kwa mujibu wa sheria na masharti ya mifumo ya sheria katika nchi husika. Data kama hivyo huenda ikatumiwa tu kwa azma zilizobainishwa wakati ilipotolewa na kama

MUHTASARI

G

USIMAMIZI WA HATARI NA BIMA

G1. Ni sentensi ipi kati ya zifuatazo ambayo haihusiani na hatari?

- ☐ **a.** Kufilisika.
- ☐ **b.** Kukasirika.
- ☐ **c.** Kuwa na ajali kazini.
- ☐ **d.** Kuwa mwathiriwa wa moto.

G2. Orodha ifuatayo inaonyesha mikakati ya ulinzi dhidi ya hatari, isipokuwa moja, ni ipi?

- ☐ **a.** Kuwa na akiba.
- ☐ **b.** Kuwa na bima.
- ☐ **c.** Kutuma pesa
- ☐ **d.** Kutumia chandarua cha kukinga mbu.

G3. Bima hutoa ulinzi dhidi ya uwezekano wa hasara. ☐ **a.** Kweli ☐ **b.** Si kweli

G4. Nini maana ya kizuio?

- ☐ **a.** Hati anayopewa Mmiliki wa mkataba wa bima na kampuni ya bima ambao unaeleza sheria na masharti ya mkataba husika wa bima.
- ☐ **b.** Masharti maalum au hali ambazo kwa kawaida huorodheshwa katika mkataba kuwa hazishughulikiwi.
- ☐ **c.** Ombi la fidia kwa hasara ambayo haishughulikiwi na mkataba wa bima.

Majibu: G1:b; G2: c.; G3: a; G4:b

1. KUSIMAMIA HATARI

Hatari inaweza kuchukuliwa kuwa hali inayotazamiwa na ambayo inaweza kuwa na athari mbaya kwetu au kwa familia yetu. Hatari huwa na uwezekano tofauti wa kutukia na madhara yake ni tofauti, kutoka madhara madogo hadi makubwa, kutegemea aina ya hatari na sifa za watu au maeneo yaliyoathirika.

UJELEZI

Hatari ni hali ambayo kuna uwezekano au tishio kwamba jambo mbaya au lisilopendeza litafanyika.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO G.1.1

Kadi za hatari

Kutokuwa na kazi

Ajali ya kazini

Ugonjwa



Kifo

Moto

Kwa kuzingatia hatari ambazo zinakukumba wewe na familia yako, andika hatari katika visanduku kulingana na matukizi yake (uwezekano wa kutukia) na gharama zake. Kwa mfano, kifo ni kitu ambacho hutokea kwa nadra sana (mara moja!) lakini kina gharama kubwa sana kwa familia.

		GHARAMA		
		Sio muhimu sana	Ni muhimu kwa kiasi fulani	Ni muhimu sana
MATUKIZI	Nadra			Mfano: kifo
	Wastani			
	Mara kwa mara			

Kama unavyoona, hatari mbalimbali zina uwezekano mkubwa au mdogo na zinaweza kusababisha matokeo tofauti, kuanzia kwa madhara madogo hadi madhara makubwa zaidi, kutegemea aina ya hatari na sifa za watu au maeneo yaliyoathirika.

KUMBUKA

Kuna mikakati tofauti ya kujilinda ambayo unaweza kuchukua:

- Kuondoa/kuepuka hatari husika (k.m. kusugua meno yako)
- Kuhamisha hatari kwa mshirika wa nje (chama cha manufaa ya pamoja au kampuni ya bima)
- Kutabiri athari ya hatari na kujiandaa dhidi yake (kwa mfano, kwa kuweka akiba)

Kuna hatua tofauti ambazo unaweza kuchukua kujikinga wewe na familia yako dhidi ya hatari hii. Andika hatua hizi chini ya mwavuli!

KISAIDIZI CHA MAFUNZO G.1.2

Mwavuli wangu

UJUMBE MUHIMU

- Hatari ni sehemu ya maisha.
- Baadhi ya hatari zinaweza kutazamiwa, na unahitajika kuchukua hatua ili upunguze athari zake.
- Ni muhimu kuwa na hazina ya dharura ili kukitokea dharura ndogo zisikuathiri sana; kuweka akiba ni muhimu katika kupunguza uwezekano wako wa kudhurika.
- Kwa baadhi ya dharura, huenda akiba ya kibinafsi isitoshe: unahitaji kutumia bima.
- Unapaswa kuchukua hatua za kujilinda na kuilinda familia yako.
- Kwa wamiliki wa biashara, zingatia kwamba kuna hatari nyingi za kazi na za kiafya mahali pa kazi. Unastahili kuzingatia gharama hizi.

2. VIDOKEZO VYA KUUNDA HAZINA YAKO YA DHARURA

- Anza kutenga pesa kwa dharura za kibinafsi kila siku au kila wiki, hata kama ni kiasi kidogo tu. Kidogo, hazina yako itakua.
- Weka pesa zako mahali salama, ikiwezekana nje ya nyumba yako, ili mtu asizipate. Kufungua akaunti ya akiba, ikiwa inawezekana, huenda ikawa wazo nzuri.
- Hifadhi kiwango tofauti, kulingana na kiasi ambacho unalipwa katika hali yoyote. Si lazima uweke akiba ya kiasi sawa kila wakati,
- Fanya kila uwezalo kupunguza matumizi yasiyo ya msingi. Kila mtu anaweza kuweka akiba, licha ya kiasi kidogo unacholipwa, hata kama ni pesa kidogo.

Uchunguzi Kifani N°1

HAZINA YA DHARURA YA GLORIA

Gloria ameamua kujenga hazina yake ya dharura. Ili kufanya hivi, anaamua kuandaa jedwali ambalo linaonyesha mapato ya familia zao katika mwaka uliopita. Jedwali hilo liko hivi:

Mapato ya familia ya Gloria kwa mwaka mmoja

Mwezi	Kiasi (Shilingi)
Januari	19,000
Februari	17,800
Machi	17,000
Aprili	18,600
Mei	19,000
Juni	19,200
Julai	18,750
Agosti	19,000
Septemba	17,800
Oktoba	19,200
Novemba	19,500
Desemba	20,300
Jumla	225,150

Maswali kuhusu Gloria na Familia yake:

- Je, familia ya Gloria inapata Kiasi gani cha mapato katika kipindi cha miezi 12 (zingatia huenda kukawa na mapato yaliyobainishwa na mapato yanayobadilika)
- Je, nini kiasi cha wastani cha mapato ya familia hii kwa mwezi?
- Je, wanahitaji kutenga jumla ya kiasi gani kwa hazina ya dharura?

KUMBUKA

Hazina yako ya dharura inalenga kushughulikia matumizi katika dharura ndogo. Wengi wenu hamtaweza kutenga pesa nyingi kwa dharura kubwa, kama vile kipindi kirefu cha matibabu au kifo katika familia.

Ikiwa utapangia dharura, una uwezekano mkubwa zaidi wa kutimiza malengo yako. Ikiwa una hazina ya dharura, utaepuka kutumia akiba ambayo umeweka ya kuanzisha biashara, kuimarisha nyumbani kwako, kuwekeza katika elimu (yako au ya watoto wako). Na utaepuka kuhitajika kukopa na kulipa viwango vya juu vya riba.

3. ELEWA MKATABA WA BIMA YAKO

BIMA: Wazo ni lipi?

Kanuni ya bima ni kujikinga dhidi ya hatari ambazo zinatukumba (ajali, maradhi, wizi...) na kutenga pesa fulani za kiupokea fidia siku yenye tukio husika litatokea.

UJELEZI

Bima ni aina ya ulinzi, kwa yeyote ambaye amejisajili kwa mkataba wa bima, katika mfumo wa fidia ya kifedha kutokana na ajali au tukio lolote linaloshughulikiwa na bima hiyo.

Chama cha manufaa ya pamoja: ni shirika lisilo la kibiashara ambalo linamilikiwa kwa pamoja na wanachama wake. Huwa kinatoa bima kwa wanachama wake na huchunga maslahi yao.

Kampuni ya bima: ni biashara ambayo inatoa huduma za bima. Lengo lake ni kupata faida.

Uchunguzi Kifani N°2

OTIENO ANAJERUHI MKONO WAKE

Otieno alipata ajali jana. Alipokuwa anatia mkate katika tanuri, alikosa makini kwa muda na akachomeka mkono. Kwa bahati nzuri, hakujeruhiwa vibaya. Mwanzoni, mkono wake haukuuma sana, lakini kufikia jioni ulikuwa umefura sana.

Kwa bahati nzuri, Otieno na familia yake yote wamejisajili kama wanachama wa Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF). Bima hii inashughulikia gharama zinazohusiana na dawa, ushauri wa daktari, na ziara za hospitali. Wanahitajika kulipa pesa kidogo kila mwezi kwa bima hii. Hii ndiyo mara ya kwanza Otieno anapata ajali kama hii na anapata afueni kujua kwamba bima inasimamia gharama zinazohusiana na ajali hii

Uchunguzi Kifai N°3

MUTUA ANAJERUHIWA MGUU

Wazazi wa Mutua, Kalekye na Kyalo, wamekuwa wakilipa ada za NHIF kwa muda sasa. Kwa vile Mutua anaondoka kwenda Kuwait hivi karibuni, anafikiria ni kupoteza pesa kulipia bima yake, kwa kuwa yeye ni kijana na hakuna kitu kitamfanyikia.

Alasiri moja, akimsaidia mamake kupanga masanduku fulani, anateleza na kuandika kutoka kwenye ngazi na kuvunja kidole cha mguu. Anafanya kadri awezavyo kusitisha uvujaji wa damu na kukifunga kidonda hicho. Alijaribu kupuuza maumivu, lakini jioni hiyo kidole hicho kinafura vibaya. Alikuwa nahitajika kufanya kazi na Opiyo siku iliyofuata, lakini alikuwa na maumivu makali.

Anahofia kwamba, ikiwa atahitajika kupata ushauri na matibabu ghali, huenda asiwe na pesa za kutosha kugharamia. Usiku, maumivu yanazidi na kwa hivyo Mutua anaenda hospitalini.

Daktari anamweleza kwamba anahitaji eksirei na dawa, lakini hana pesa za kutosha kulipia gharama hizi zote. Wazazi wake walimwambia mara nyingi kwamba hastahili kuacha kulipia bima, lakini alifikiri ni kupoteza pesa. Sasa, Mutua atahitajika kukopa pesa ili kulipa gharama hizi na kupata matibabu. Angependa kuepuka kuhitajika kukopa pesa ikiwa tukio sawa litatokea tena.

MUHIMU: Wakati mwingine, mfadhaiko wetu unaweza kuathiri mwili wetu. Ikiwa usimamizi wa pesa unakutia wasiwasi, hii inaweza kusababisha matatizo ya afya ya mwili.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO G.2.1

Kadi za kucheza mchezo wa chungu cha hazina

MCHEZO WA CHUNGU CHA HAZINA

Vikasha 3

DAWA

ELIMU YA KIFEDHA

MCHEZO WA CHUNGU CHA HAZINA

Vikasha 7

HOSPITALI

ELIMU YA KIFEDHA

MCHEZO WA CHUNGU CHA HAZINA

AFYA NJEMA

ELIMU YA KIFEDHA

MCHEZO WA CHUNGU CHA HAZINA

Vikasha 4

DAKTARI

ELIMU YA KIFEDHA

Huwezi kujua ni lini au kiasi gani utahitajika kulipia afya yako. Wakati mwingine gharama za matibabu ni kubwa sana kiasi kwamba zinazidi uwezo wako wa kifedha. Hii ndiyo maana ni muhimu kujumlisha hatari kwa kujiunga na bima.

Siri ya kujumlisha hatari ipo katika hali kwamba sote tunachangia sehemu ya rasilimali zetu katika chungu kimoja. Hatuhitaji kutoa pesa kwenye chungu hiki kwa wakati sawa. Hata hivyo, bima inafaulu tu iwapo sote tutachanga kwa pamoja.

Unahitaji kulipa mapema ili uwe na uhakika wa kupata huduma za matibabu, kwa wale wanaokingwa na bima hiyo. Kiwango cha huduma za matibabu ambazo unaweza kupokea kinategemea kiwango unachochangia. Kadri unavyochangia zaidi, ndivyo unapata huduma zaidi.

UJUMBE MUHIMU

- Bima: kifaa cha kuhifadhi mapato na ulinzi wa kijamii
- Kuwa na bima ni kuzuia hatari.
- Bima: kuunganisha hatari.



TANBIHI: Baadhi ya wafanyakazi, hasa wafanyakazi ambao hupokea mshahara kutoka taasisi rasmi (k.v. Kampuni iliyosajiliwa na serikali na ambayo hulipa ushuru), huwa na bima lakini mara nyingi hawajui inashughulikia nini au namna ya kuitumia. Wakati mwingine, wafanyakazi wa kampuni ya bima hawaelezi mipangilio ya bima, na hutumia istilahi changamano. Kumbuka pia kwamba kwa sasa Bima ya Afya ya Jamii ni njia nzuri sana ya kuwa na mkataba wa bima ambao unakulinda katika masuala ya afya.

KUMBUKA

Ufahamu ni uwezo. Unastahili kujua maana ya bima (matukio yanayoshughulikiwa, malipo, jinsi ya kufanya madai). Kila mara kuwa na kadi ya bima, ikiwa unayo

4. TUMIA MKATABA WAKO WA BIMA

Watu hukumbwa na hatari nyingi katika maisha yao na kila kipindi cha maisha yao huwa na hatari zake tofauti. Baadhi ya hatari ni za jumla na zinaweza kutokea kwa yeyote. Hatari zingine huenda zikawa mahususi kwa kategoria za watu.

Hebu tuangazie hatari maalum zinazowakumba wahamiaji.

HATARI ZA JUMLA	HATARI MAALUM KWA WAHAMIAJI
• Kifo • Ugonjwa • Ajali • Wizi • Nyumba yako kuchomeka • Kukosa kazi/kufutwa kazi • Dhuluma za kimwili, kisaikolojia na/au kingono	• Hatari ya msongo wa mawazo kwa kuwa mbali na wapendwa wako • Hatari ya kuachishwa kazi • Hatari ya unyanyasaji wa kimwili, kisaikolojia na/au kingono/unyanyasaji, hasa kwa wahamiaji wasio halali. • Hatari ya kutolipwa mshahara • Hatari ya kifo, ugonjwa, ajali katika nchi ya kigeni • Hatari ya kukosa ajira • Hatari ya ajali kazini • Ajali ya magonjwa yanayotokana na kazi • Hatari ya mkataba kubatilishwa • Hatari ya matatizo ya kisheria

KISAIDIZI CHA MAFUNZO G.3.1

Kadi za hatari







MASWALI

- Je, una mkataba wa bima? Ikiwa huna, je ungependa kuwa nao?

☐ **Ndiyo** ☐ **La**

- Je, unafahamu istilahi za msingi za bima?

☐ **Ndiyo** ☐ **La**

Hebu tupitie istilahi muhimu na ujelezi

ISTILAHI ZA KIMSINGI ZA BIMA	
Fidia au Malipo	*Kiasi ambacho kampuni ya bima hulipa kwa mwenye bima wakati tukio lililoandikishiwa bima (mara nyingi hurejelewa kama hatari: ajali, moto, ugonjwa...) limetokea, baada ya kuwasilisha madai halali.*
Mkataba	*Makubaliano baina ua mwenye bima (mteja) na kampuni ya bima. Mkataba hueleza sheria, masharti, muda, hatari zinazoshughulikiwa na vizuio.*
Malipo ya bima	*Bei au gharama ya mkataba wa bima, aghalabu kwa malipo ya kila mwezi au kila miezi mitatu.*
Mwenye bima (mtu) / mwanachama /	*Mtu ambaye hupokea malipo ya bima wakati hatari iliyoandikishwa katika mkataba inatoka.*
mnufaika Madai	*Ombi la fidia kutokana na hasara inayolindwa na mkataba wa bima.*
Kadi ya bima	*Kadi inayotolewa na mtoaji wa bima kama ithibati kwamba mwenye bima amelipa ada husika.*

Ili kufanya madai kwa ufanisi unastahili kufuata hatua fulani. Kumbuka utahitajika kujaza fomu ya madai na kutuma hati zote zinazohitajika.



KISAIDIZI CHA MAFUNZO G.3.2

Hatua katika kufanya madai ya bima

HATUA YA 1

Jaza fomu ya madai haraka iwezekanavyo baada ya uharibifu/hasara kutokea (ndani ya miezi 12, kulingana na masharti ya mkataba).

ELIMU YA KIFEDHA

HATUA YA 2

Wasilisha hati zinazohitajika: barua ya madai iliyotiwa sahihi na mwenye bima, kadi ya bima, nakala ya kitambulisho chako...

ELIMU YA KIFEDHA

HATUA YA 3

Ikiwa utalipwa kiasi kidogo kuliko ulivyotarajia, wasilisha malalamishi yako, jua kwa nini na ujaribu kushughulikia.

ELIMU YA KIFEDHA

HATUA YA 4

Thibitisha kwamba fidia iliyolipwa inalingana na manufaa unayostahili kulipwa

ELIMU YA KIFEDHA

HATUA YA 5

Ikiwa hutalipwa ndani ya siku saba (au katika muda uliobainishwa katika mkataba wa bima), wasiliana na kampuni ya bima tena ili kukagua hatua iliyofikia.

ELIMU YA KIFEDHA

UJUMBE MUHIMU

- Ili kupata mpango wa bima ambao ni bora na unaolingana vyema na mahitaji yako, kwanza unahitaji kutambua hatari zinazokukabili wewe na watu unaotaka kuwakinga.
- Bima hutumia istilahi maalum - Unapaswa kujifunza vyema ili kuelewa mipango ya bima iliyopo na kufanya uamuzi wa busara.
- Kila hatari iliyosajiliwa kwa bima inahitaji hati tofauti wakati wa kuandikisha madai.

4. CHAGUA MPANGO WA BIMA UNAOKUFAA

Sasa tutawasaidia wahusika wetu kusuluhisha baadhi ya tashwishi walizonazo kuhusu mikata ya bima ya ajali ambayo wameandikisha.

KISAIDIZI CHA MAFUNZO G.4.1

Uchunguzi Kifani wa bima ya ajali

UCUNGUZI KIFANI #1 - Gloria

Gloria na familia yake wamekuwa wakilipia Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF) kwa muda sasa.

Katika msimu wa kiangazi, Mumo na Musau wanakuja kumtembelea Gloria na familia yake. Baada ya siku chache, Musau anapata homa na maumivu ya kichwa. Gloria na Gitau wako na wasiwasi na wanawaza jambo bora zaidi la kufanya ni kumpeleka hospitalini.

Je, bima ya Gitau itasimamia gharama za matibabu ya babake? Kwa nini?

UCHUNGUZI KIFANI #2 - Mutua

Baada ya ajali ya ngazi ambapo Mutua alivunja kidole chake cha mguu, alijiunga na Hazina ya Kitaifa ya Bima ya Afya (NHIF). Kwa miezi 6 iliyopita, hajapata ajali nyingine.

Mutua anafikiri anapaswa kurejesha angalau baadhi ya ada alizolipa, kwa kuwa hajatumia bima yake kupata huduma za kiafya baada ya ajali.

Je, Mutua anastahiki kurejeshewa ada alizolipa? Kwa nini?

UCHUNGUZI KIFANI #3 - Wangari

Wangari anahofia kwamba hataweza kulipia ada za mkataba mpya wa bima ya afya ambayo amepewa. Lakini amekuwa na maumivu ya goti kwa miezi michache iliyopita na huenda akahitaji kufanyiwa upasuaji hivi karibuni, kabla ya kusafiri kwenda Qatar. Ingawa ada hizo zinatoa bima ya afya kwa mwaka mmoja, Wangari anataka kujisajili kwa mkataba wa miezi mitatu pekee, kuanzia mwezi mmoja kabla ya upasuaji wa goti na kuisha miezi miwili baada ya upasuaji.

Je, Wangari anaweza kulipia mkataba wa bima kwa miezi mitatu pekee? Kwa nini?

UJUMBE MUHIMU

- Bima huenda ikaonekana kuwa changamano. Lakini, kwa kuwa sasa umeelewa masuala ya msingi, unaweza kutathmini ikiwa ulinzi unaotolewa na bima yako unakupa thamani kwa gharama.
- Ikiwa unataka kulipia mkataba wa bima ya afya, utahitajika kuamua ni watu gani wa familia utawajumuisha katika sera hiyo. Baadhi ya sera hutoza ada ya ziada kwa kila mtu wa familia unayeongeza katika mkataba huo. Baadhi hutoa mpango wa kimsingi kwa familia ya watu wanne, na ada za ziada kwa watu zaidi wa familia.
- Ni muhimu sana kujifunza kanuni ambazo kila sera inatumia ili kuhesabu malipo ya kuwekea familia yako bima.
- Mikataba ya bima haifanani. Ni muhimu kuelewa mkataba na masharti yake kabla ya kujisali katika mkataba husika. Jiamini kuzungumza na wakala wa bima, mwajiri wako au chama chako cha wafanyakazi ikiwa una tashwishi zozote.
- Ikiwa ungependa kulipia mkataba wa bima, au ikiwa una maswali yoyote, wasiliana mara moja na wakala wa bima, mwajiri wako, au mwakilishi wako wa chama cha wafanyakazi

MUHTASARI

VIAMBATISHO NA HATI MUHIMU

CHANGAMOTO	USHAURI
Napendelea kutoa mapato yangu yote kwa wazazi na familia yangu (majukumu ya kifamilia yenye mashiko hasa kwa vijana na wahamiaji)	• Weka akiba kwa ajili ya dharura za kibinafsi ili uweze kujitunza wakati familia yako haiwezi kukusaidia (hasa kwa wale wanaoishi mbali na nyumbani). • Anza kutenga pesa kwa dharura za kibinafsi kila siku au kila wiki, hata kama ni kiasi kidogo tu. Kidogo kidogo, hazina yako itakua.
Ninapoweka pesa katika chumba changu, ninaogopa kwamba huenda zitaibiwa au zikapotea.	• Weka pesa zako mahali salama, ikiwezekana nje ya nyumba yako, ili mtu asizipate. • Fungua akaunti ya akiba (kwa hazina ya dharura, suluhu bora zaidi ni kuwa na akaunti yenye unyumbufu, yaani unaweza kutoa pesa zako wakati wowote).
Mapato yangu si thabiti (k.m. ni ya msimu).	• Hifadhi kiwango tofauti, kulingana na kiasi ambacho unalipwa katika hali yoyote.
Lazima nitumie mapato yangu yote ya ziada kulipa madeni.	• Andaa ratiba ya kulipa madeni yako, ukianza kwa yale ambayo unalipa riba ya juu zaidi. • Kwa wakati huo huo, anza kutenga pesa kwa dharura za kibinafsi kila siku au kila wiki, hata kama ni kiasi kidogo tu. Akiba yako itazidi kuongezeka.
Siwezi kugharamia mahitaji yangu ya kimsingi.	• Fanya kila uwezalo kupunguza matumizi yasiyo ya msingi. • Kila mtu anaweza kuweka akiba, licha ya kiasi kidogo unacholipwa, hata kama ni kiasi kidogo kidogo tu (taja kiasi kidogo katika sarafu ya ndani ambacho kinaweza kutengwa kila siku, wiki au mwezi).

MAJIBU KWA MAZOEZI:

Uchunguzi Kifani wa bima ya ajali (KISAIDIZI CHA MAFUNZO G.4.1)

SULUHU KWA CHUNGUZI KIFANI #1

Je, bima ya Gitau itasimamia gharama za matibabu ya babake? Kwa nini

La, mkataba wa Gitau hauwezi kumshughulikia Musau. Bima ya afya ya aina hii inashughulikia watu wa familia tu ambao wakandikisha mkataba (Gloria, Gitau na watoto wao).

SULUHU KWA CHUNGUZI KIFANI #2

Je, Mutua anastahiki kurejeshewa ada alizolipa? Kwa nini

Mutua hastahiki kurejeshewa ada alizolipa, kwa sababu azma ya bima yake ni kumkinga dhidi ya hatari. Hata kama hahitaji usaidizi kwa miaka mingi, ada zake hazitarejeshwa.

SULUHU KWA UCHUNGUZI KIFANI #3

Je, Wangari anaweza kulipia mkataba wa bima kwa miezi mitatu pekee? Kwa nini?

Mhusika hawezi kulipia mkataba wa miezi mitatu kwa sababu ada zimewekwa kwa mwaka mmoja. Hawezi kubadilisha idadi ya miezi, lazima alipe ada za bima kwa mwaka mzima.

UJELEZI

JUMLA

LENGO
Lengo ni kitu ambacho ungependa kufanya katika siku zijazo.

RASMI/ISIYO RASMI
Kwa ujumla, kitu ambacho ni rasmi huheshimu muundo, kumaanisha kwamba kinajikita katika mfumo, muundo, au sheria fulani. Pia ni kitu ambacho ni halali na kinatambuliwa na mamlaka fulani.

Kwa upande mwingine, kitu ambacho sio rasmi hakidhibitiwi na kanuni kali au mfumo rasmi. Kwa mfano, sekta isiyo rasmi inajumuisha biashara ambazo hazijasajiliwa na hazilipi ushuru.

BAJETI
Bajeti ni kifaa cha kuamua, kupanga na kutumia pesa ili kufikia malengo yako.

MKATABA WA AJIRA
Ni makubaliano (ya kisheria) baina ya mwajiri na mfanyakazi ambayo yanaeleza majukumu na wajibu na manufaa kwa wahusika wote wawili.

Mkataba unapaswa kujumuisha maelezo ya majukumu, wajibu na haki. Unafafanua masharti ya ajira na utendakazi, kama vile malipo, saa za kazi.

Mkataba ni makubaliano baina ya wahusika wawili ambayo wahusika wote wawili hutia sahihi kwa hiari yao wenyewe. Mkabata wa ajira ikiwezekana unapaswa kuwa katika maandishi, katika lugha inayoeleweka na wahusika wote wawili, utiwe sahihi na pande zote mbili na nakala kutolewa kwa kila mhusika.

TAASISI YA KIFEDHA
Taasisi ya kifedha ni huduma ya umma au ya kibinafsi ambayo inashughulikia uendeshaji wa kifedha kama vile uwekaji akiba, miamana na malipo.

VYAMA VYA USHIRIKA VYA AKIBA NA MIKOPO
Chama cha Ushirika cha Akiba na Mikopo ni chama cha kipekee cha ushirika ambacho ni cha kidemokrasia, cha kipekee kinachoongozwa na wanachama ambacho hujizatiti kutimiza mahitaji ya kifedha ya wanachama wake. Kinamilikiwa, kutawaliwa na kusimamiwa na wanachama wake.

AKAUNTI YA AKIBA

AKAUNTI YA AKIBA YA KAWAIDA
Akaunti ya akiba ya kawaida (pia inajulikana kama akaunti ya amana ya mahitaji) katika taasisi ya kifedha humruhusu mwenye akaunti kuweka amana au kutoa pesa wakati wowote. Kiasi na muda hakibainishwi mapema. Akiba huzaa riba kwa mujibu wa kiwango kilichobainsihwa (kwa kawaida kwa mwaka) Akaunti hii ya akiba kwa kawaida haiwezi kutumiwa kufanya malipo ya moja kwa moja.

AKAUNTI YA AKIBA YA KIMKATABA
Akaunti ya akiba ya kimkataba katika taasisi ya kifedha humruhusu mwenye akaunti kuunganisha amana zake na utimizaji wa malengo maalum. Mwenye akaunti huweka kiasi kilichobainishwa cha pesa mara kwa mara kwa muda uliobainishwa. Baada ya tarehe ya kutimia kwa mkataba mteja anaweza kutoa pesa zote pamoja na riba (kiwango cha riba huwa kimebainishwa mapema. Kutoa pesa kabla ya muda kutimia huwa imekatazwa au hutozwa ada ya adhabu.

AKAUNTI YA AMANA YA MUDA MAALUM
Akaunti ya amana ya muda maalum katika taasisi ya kifedha humruhusu mwenye akaunti kuweka kiasi kikubwa cha pesa, ambazo anaahidi kutogusa kwa kipindi maalum. Mteja anaweza kuchagua kutoka kwa masharti mbalimbali yanayowezekana. Kwa kuwa aina hii ya akaunti inatoa vizuizi (muda na kiasi kilichowekwa) kwa mteja, kwa kawaida huwa inalipa riba ya juu zaidi kwa mpango wowote wa akiba.

UJELEZI

MKOPO

KIASI CHA RIBA
Kiasi cha pesa ambacho mkopaji anamlipa mkopeshaji, pamoja na kiasi cha mkopo, kwa matumizi ya pesa za mkopeshaji.

KIASI CHA MKOPO
Kiasi asili cha mkopo, bila riba.

MUDA WA MKOPO
Ni muda ambao mkopaji atatumia pesa za mkopo na kuzilipa.

DHAMANA
Kitu cha thamani ambacho mkopaji humpa mkopeshaji ikiwa mkopaji atashindwa kulipa mkopo wake (huenda ikawa ardhi, gari, akiba, n.k.).

KIPINDI CHA NYONGEZA
Kipindi baada ya kupokea mkopo na kabla ya kufanya malipo ya kwanza.

KUTAFAKARI UPYA
Ubatilishaji wa mkataba wa muamana. Katika baadhi ya nchi makubaliano ya mkopo hayana mashiko kisheria hadi siku au wiki kadhaa baada ya kutia sahihi. Katika kipindi hiki hakuna malipo yanaweza kufanywa na mkopeshaji au na mkopaji. Hii huhakikisha ulinzi wa kutosha dhidi ya ununuzi wa kiholela.

MALIPO YA MAPEMA
Mkopaji daima ana uhuru wa kulipa mkopo wote au sehemu ya mkopo wake kabla ya tarehe ya mwisho ya makubaliano ya mkopo, na bila kutozwa ada za adhabu.

MDHAMINI
Mtu ambaye atalipa mkopo wako ikiwa utashindwa kulipa; mtu huyu anaweza kuhitajika kutia sahihi makubaliano yako ya mkopo na mkopeshaji.

KUWA NA MADENI MENGI KULIKO UNAVYOWEZA KULIPA
Ukosefu wa uwezo wa mtu kulipa madeni yake ya kibinafsi.

MBINU ZA MALIPO

KADI YA PESA
Kadi ya pesa hutolewa kwako na benki yako na inakuruhusu kupata pesa kutoka kwenye akaunti yako kwa kutumia mashine maalum inayoitwa ATM. Mbali na kutoa pesa kwenye akaunti yako, unaweza kutumia mashine ya ATM kukagua salio la akaunti, kutuma pesa kutoka akaunti moja hadi nyingine, na kuweka amana kwenye akaunti yako. Baadhi ya mashine za ATM huuza stempu za posta au mjazo wa muda wa maongezi au kuruhusu kulipa bili fulani (umeme...). Kila benki iko na mtandao wake wa mashine za ATM lakini mara nyingi unaweza kutumia kadi yako ya benki kutoa pesa katika mashine yoyote ya ATM iwe ni ya benki yako au la. Hata hivyo, benki yako huenda ikakutoza ada kila mara unapotumia mashine ya ATM ambayo ni ya mtandao wa benki tofauti.

KADI YA MALIPO
Kadi ya malipo ni njia nyingine ya kufanya miamana ya benki kielektroniki. Mbali na kuitumia kutoa pesa katika mashine za ATM, unaweza kutumia kadi ya malipo kulipia bidhaa unazonunua katika maduka mengi. Lazima uwe na pesa katika akaunti yako wakati wa ununuzi. Kiasi cha ununuzi wako kinatolewa kutoka akaunti yako mara moja. Utapokea taarifa mara kwa mara kutoka benki, ikionyesha kiasi cha jumla kilichotolewa kwenye akaunti yako na salio lako.

KADI YA MKOPO

Kwa jumla, kadi ya mkopo inakuruhusu ufanye miamala kama ilivyo kwa kadi ya pesa na ya malipo. Tofauti kuu ni kuwa kadi hii pia inakuwezesha kupata mkopo wa papo hapo. Yaani, iwapo huna pesa katika akaunti yako, bado unaweza kufanya ununuzi kwa kuchukua mkopo kutoka kwa taasisi iliyokuuzia kadi ya mkopo (taasisi ya kifedha, lakini pia duka la jumla, nyingine).

Kulingana na vipengele vya mkataba wa kadi yako ya mkopo, kiasi cha ununuzi wako kitakatwa kutoka kwa akaunti yako (kwa awamu moja au zaidi, kwa kiwango cha riba ambacho mara nyingi huwa cha juu zaidi kuliko mipango ya kawaida ya mkopo...). Utapokea taarifa ya mara kwa mara kutoka kwa taasisi iliyotoa kadi hiyo ya mkopo, ikionyesha jumla ya kiasi kitakacholipwa, kiasi ambacho tayari kimelipwa na kiwango cha riba.

UTUMAJI WA PESA

WATOAJI WASIO RASMI WA HUDUMA ZA KUTUMA PESA

Mashirika haya hayadhibitiwi na serikali. Watoaji wa aina hii wanajumuisha maduka ya rejareja, marafiki na wasafirishaji.

WATOAJI RASMI WA HUDUMA ZA KUTUMA PESA

Mashirika haya hudhibitiwa au kusimamiwa na serikali. Watoaji wa aina hii wanajumuisha watoaji wa huduma za kutuma pesa (MTOs), benki, taasisi ndogo za kifedha, vyama vya ushirika vya akiba na mikopo, na watoaji wa huduma za simu za mkononi.

HATARI NA BIMA

HATARI

Hatari ni uwezekano wa hasara au jeraha.

BIMA

Bima ni aina ya ulinzi, kwa yeyote ambaye amejisajili kwa mkataba wa bima, kwa njia ya fidia ya kifedha kutokana na ajali au tukio lolote linaloshughulikiwa na bima hiyo.

KAMPUNI YA BIMA

Kampuni ya bima ni biashara (huwa na mwelekeo wa kupata faida) ambayo inatoa huduma za bima.

CHAMA CHA MANUFAA YA PAMOJA

Chama cha manufaa ya pamoja ni shirika la pamoja lisilokuwa la kibiashara, ambalo hutoa bima kwa wanachama wake.

MKATABA

Hati anayopewa mmiliki wa mkataba wa bima na kampuni ya bima ambayo inaeleza sheria na masharti ya mkataba husika wa bima.

MALIPO YA BIMA

Pesa ambazo mwenye bima hulipa kwa kampuni ya bima ili kuamilisha mkataba wa bima na kulinda uhalali wake

MANUFAA

Pesa ambazo kampuni ya bima hulipa ama kwa mtu anayewasilisha madai au kwa mnufaika wake.

MNUFAIKA

Mtu ambaye anapokea pesa za bima wakati tukio lililowekewa bima linatokea.

MADAI

Ombi la fidia kwa hasara ambayo inashughulikiwa na mkataba wa bima.

KADI YA BIMA

Kadi inayotolewa na mtoaji wa bima kama ithibati kwamba mwenye bima amelipa ada husika.

VIZUIO

Masharti maalum au hali ambazo kwa kawaida huorodheshwa katika mkataba kuwa hazishughulikiwi.

KIJITABU CHA MKURUFUNZI

ELIMU YA KIFEDHA YA ILO

Kijitabu cha mkurufunzi kwa wahamiaji wanaotarajiwa na waliorejea

Mpango wa Elimu ya Kifedha wa ILO unashughulikia suala zima la ufinyu wa elimu ya kifedha, kwa kutambua kuwa ni kikwazo kikubwa katika miktadha mbalimbali ya maendeleo na sababu inayokwaza na kuchangia kupungua kwa mapato ya makundi yaliyo katika mazingira magumu. Malengo ya mpango huu ni:

- Kuendeleza mamlaka ya ILO ya kukuza kazi zenye staha kwa kuwapa watu maarifa muhimu, ujuzi na mitazamo inayohitajika kwa usimamizi bora wa fedha, hivyo basi kuwatayarisha vyema kufikia fursa za kazi zinazostahili.
- Kuwapa wakufunzi wa elimu ya kifedha wa siku za usoni maarifa na ujuzi wa kutosha katika fedha na mbinu shirikishi za uendeshaji, kuwapa vidokezo vya kusaidia vikundi vilivyo hatarini katika kufanya maamuzi ya kifedha yenye busara.
- Kuimarisha ustahimilivu wa vikundi vilivyo hatarini kwa kuboresha viwango vyao vya elimu ya kifedha na kuwahimiza kutumia mipango na huduma, na hivyo kukidhi mahitaji yao ipasavyo, katika safari yao ya kifedha.

Kupitia mkakati wa kuzidisha ikiwemo Mafunzo ya Wakufunzi na mchakato wa kutoa vyeti kwa wakufunzi wanaotahiniwa, mpango ya Elimu ya Kifedha ya ILO unasaidia kuanzishwa kwa mafunzo ya Elimu ya Kifedha ya ILO katika ngazi za chini kabisa. Walengwa wa moja kwa moja na wasio wa moja kwa moja ni pamoja na wakufunzi watarajiwa na walioidhinishwa, pamoja na makundi yaliyo hatarini kama vile watu binafsi wenye mapato ya chini, wanawake, vijana, wahamiaji, wakimbizi, wajasiriamali, biashara ndogo ndogo, pamoja na wafanyakazi wa mijini na vijijini.

Programu ya Elimu ya kifedha unasifiwa kwa nyenzo zake za mafunzo ya elimu ya kifedha zilizoundwa kwa uangalifu na ambazo zimetafsiriwa kwa uangalifu na kurekebishwa kwa miktadha tofauti, maeneo ya kijiografia na vikundi vinavyolengwa, ikiwemo wanawake na wanaume wenye mapato ya chini, vijana, wahamiaji, wakimbizi, wajasiriamali, biashara ndogo ndogo, wakulima, wavuvi na wafanyakazi wanaolipwa mishahara. Inafaa kwa wanafunzi wazima na wale walio na elimu rasmi ndogo. Nyenzo za mafunzo zimesanifiwa kwa kufuata mwelekeo shirikishi unaowezeshwa kupitia mtaala unaoshirikisha, ikiwemo kubuni wahusika, uigizaji, uchunguzi kifani unaohusiana na hadhira, kupeana mawazo na mijadala ya vikundi vidogo. Nyenzo hizo zimeundwa kwa ajili ya mazingira mbalimbali ya kujifunza, iwe vipindi vya mtu binafsi, madarasa au majukwaa ya mtandaoni. Kwa kutambua mazingira yanayobadilika ya elimu, mpango huu unatoa mweleko wa masomo, unaowaruhusu washirika kutayarisha mipango ya mafunzo kulingana na mahitaji maalum. Nyenzo za mafunzo zinajumuisha mada mbalimbali za kiutendaji, ikiwemo upangaji wa bajeti, usimamizi wa akiba, matumizi ya busara, ukopaji wa busara na usimamizi mzuri wa hatari, ambao ni muhimu katika kujenga msingi thabiti wa stadi za kifedha zinazohusiana na aina zote za makundi yaliyo katika hatari.

Kijitabu hiki cha Mkurufunzi Kimeandaliwa kwa ajili ya vikundi maalum teule. Kama nyongeza kwa mwongozo wa kawaida wa mkufunzi, kijitabu cha mkurufunzi kinatoa taarifa zote zinazohusiana na wahusika wa kubuni, uchunguzi kifani, mazoezi na marejeleo maalum kwa kundi lengwa. Kijitabu hiki pia kinajumuisha hoja muhimu za mafunzo na nyenzo zinazohitajika kwa kutumia na kusimamia pesa za kibinafsi kwa busara. Kimeandikiwa wanaume na wanawake wanaoshiriki katika masomo ya mafunzo haya. Kinapaswa kutumiwa kama kitabu cha mazoezi wakati wa somo na baadaye kama mwongozo wa marejeleo.

ISBN: 9789220409114 (chapisho)

ISBN: 9789220409121 (PDF mtandaoni)

International Labour Organization

UKaid from the British people